Nipashe

Ijumaa Julai 12, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579968

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Serikali yaahidi kuboresha mfumo vitambulisho taifa

UKURASA 4




UKURASA 13

# Aliyekataliwa na baba aongoza kidato cha 6

UKURASA 2 & 3

### SHULE 10 BORA

- KISIMIRI, ARUSHA
- FEZA BOYS, DAR ES SALAAM
- AHMES, PWANI
- MWANDET, ARUSHA
- TABORA BOYS, TABORA
- KIBAHA SEKONDARI, PWANI
- FEZA GIRLS, DAR ES SALAAM
- ST. MARRY MAZINDE JUU, TANGA
- CANOSSA, DAR ES SALAAM
- KEMEBOS, KAGERA



Faith Nicholous Matee

### SHULE 10 MKIANI

- NYAMUNGA, MARA
- HAILE SALASSIE MJINI MAGHARIB UNGUJA
- TUMEKUJA, MJINI MAGHARIB UNGUJA
- BUMAANGI, MARA
- BUTULI, MARA
- MPENDAE, MJINI MAGHARIB UNGUJA
- ECKERNFORD, TANGA
- MSIMBO, KATAVI
- MONDO, DODOMA
- KIEMBE SAMAKI A MJINI MAGHARIB

### WANAFUNZI 10 BORA SAYANSI

1. Faith Nicholous Matee (ST. Mary's Mazinde Juu Tanga)
2. Herman Pauline Kamugisha (Kisimiri Arusha)
3. Levina Calist Chami (ST. Coreti ya Kilimanjaro)
4. Benius Eustace (Mzumbe ya Morogoro)
5. Augostino Issaya Omari (Ilboru ya Arusha)
6. Satrumin Arbogast Shirima (Temeke Dar Es Salaam)
7. Khalid Hussein Abdalla, (Feza Boys Dar Es Salaam)
8. Assad Y.Msangi (Feza Boys Dar Es Salaam)
9. Peter Jovenal Riima (Kibaha Pwani)
10. Augustine J. Kamba (Feza Boys Dar Es Salaam)

## Meneja madini mbaroni tuhuma za uchakachuaji

UKURASA 4

## Utata utekaji msaidizi Membe

UKURASA 4

MICHEZO SIMBA KWENDA SAUZI JUMAPILI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

# Ufaulu kidato cha sita 2019 wapanda

## ■Wasichana wang'ara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BARAZA la Mitihani ya Taifa Tanzania limetangaza matokeo ya kidato cha sita kwa mwaka 2019 kupanda ufaulu kwa asilimia 0.74 kutoka asilimia 97.58 ya mwaka 2018 hadi asilimia asilimia 98.32 ya mwaka huu.

Wasichana katika matokeo hayo wameng'ara zaidi katika masomo ya Sayansi.

Vile vile, ubora wa ufaulu huo umezidi kuimarika kwa kuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu vizuri katika daraja la kwanza, pili na tatu umeongezeka kwa asilimia 1.09 kutoka asilimia 95.52 mwaka 2018 na kuwa na asilimia 96.61 mwaka huu.

Akitangaza matokeo hayo katika Ofisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Mazizini, nje kidogo ya mji wa Zanzibar, Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Charles Enock Msonde, alisema ubora wa ufaulu wa wasichana kwa mwaka huu umezidi wa wavulana kwa asilimia 1.07.

Katika matokeo hayo wanafunzi 14 walifutiwa matokeo yao kutokana na kubainika kufanya udanganyifu katika mitihani hiyo na kati ya hao tisa ni wa shule na watano ni wakujitegemea.

"Baraza la Mitihani linapenda kuchukua fursa hii kuzipongeza kamati zote za uendeshaji mitihani, wakuu wa shule na wasimamizi wa mitihani iliyofanyika Mei 2019 kwa kuzingatia na kusimamia taratibu za uendeshaji mitihani na hivyo kuzuia kwa kiasi kikubwa udanganyifu kufanyika," alisema Msonde.

Kadhalika, alisema shule zote zilizofanya mitihani hiyo kwa mwaka huu zimefanya vizuri, lakini zimepishana katika ubora.

**SHULE 10 BORA**

1. KISIMIRI, ARUSHA
2. FEZA BOYS, DAR ES SALAAM
3. AHMES, PWANI
4. MWANDET, ARUSHA
5. TABORA BOYS, TABORA.
6. KIBAHA, PWANI.
7. FEZA GIRLS, DAR ES SALAAM.
8. ST. MARRY MAZINDE JUU, TANGA
9. CANOSSA, DAR ES SALAAM
10. KEMEBOS, KAGERA

**SHULE 10 ZA MWISHO**

1. NYAMUNGA, MARA
2. HAILE SALASSIE, MJINI MAGHARI UNGUJA.
3. TUMEKUJA, MJINI MAGHARIB UNGUJA
4. BUMAANGI, MARA
5. BUTULI, MARA
6. MPENDAE, MJINI MAGHARIB UNGUJA
7. ECKERNFORD, TANGA
8. MSIMBO, KATAVI
9. MONDO, DODOMA
10. KIEMBE SAMAKI A, MJINI MAGHARIB UNGUJA

**10 BORA KITAIFA MASOMO YA SAYANSI**

1. Faith Nicholous Matee, (St. Mary's Mazinde Juu Tanga)
2. Herman Pauline Kamugisha, (Kisimiri Arusha)
3. Levina Calist Chami, (St. Coreti ya Kilimanjaro)
4. Benius Eustace, (Mzumbe ya Morogoro)
5. Augostino Issaya Omari, (Ilboru ya Arusha)
6. Satrumin Arbogast Shirima, (Temeke Dar es Salaam)
7. Khalid Hussein Abdalla, (Feza Boys Dar es Salaam)
8. Assad Y. Msangi, (Feza Boys Dar es Salaam)
9. Peter Jovenal Riima, (Kibaha Pwani)
10. Augustine J. Kamba (Feza Boys ya Dar es Salaam).

**WASICHANA 10 BORA SAYANSI**

1. Faith Nicholous Matee, (St. Mary's Mazinde Juu Tanga)
2. Levina Calist Chami, (St. Coreti ya Kilimanjaro)
3. Wahida Janguo, (Feza Girls Dar es Salaam)
4. Vanessa R. Rutabana, (Tabora Girls ya Tabora)
5. Pielina M. Figowole, (Tabora Girls, Tabora)
6. Loveness Samson Mloge, (St. Mary's, Mazinde Juu)
7. Wahida Mbaraka Uzia, (Zanzibar Feza Mjini Magharibi)
8. Beatrice Martin Mwella, (St. Mary's Mazinde Juu)
9. Consolata Seraphin Matee, (St. Mary's Mazinde Juu)
10. Maimuna A. Mshana, (Marian Girls ya Pwani).

**WAVULANA 10 BORA SAYANSI**

1. Herman Pauline Kamugisha, (Kisimiri Arusha)
2. Benius Eustace, (Mzumbe ya Morogoro)
3. Augostino Issaya Omari, (Ilboru ya Arusha)
4. Satrumin Arbogast Shirima, (Temeke Dar es Salaam)
5. Khalid Hussein Abdalla, (Feza Boys Dar es Salaam)
6. Assad Y. Msangi, (Feza Boys Dar es Salaam), Peter
7. Jovenal Riima, (Kibaha Pwani)
8. Augustine J. Kamba, (Feza Boys ya Dar e Salaam)
9. Shedrack Leonartus Siame, (UWATA Mbeya)
10. Noel Godwin Maro (St. Mary Goreti Kilimanjaro)

**10 BORA WAVULANA LUGHA YA SANAA**

Vile vile akitanga matokeo hayo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani, Msonde, aliwataja watahiniwa 10 bora wa masomo ya Lugha ya Sanaa kuwa namba moja ilishikwa na Victor G. Mtuli (Fedha Boys, Dar es Salaam), Paula Nelson Lujwangana (St. Mary's Mazinde Juu, Tanga), Blandina Kessy Nyange (St. Mary's Mazinde Juu, Tanga) na Eva J. Shitindi (Machame Girls, Kilimanjaro).

Wengine ni Ruhinda Benedicto Machimu (Geita Adventist, Geita), Anita Zacharia Massawe (St. Mary's Mazinde Juu, Tanga), Karim Kassimu Muhimu (Nyangao, Lindi), Anold Andrea Msuya (Dareda, Manyara), Latifa Mohammed Mrosso (Ahmes, Pwani) na Elibariki Desidery Balinyanga (Lukole, Kagera).

**10 BORAWA SICHANA SANAA**

Kwa upande wa wasichana walioshika 10 bora kwenye masomo ya Lugha ya Sanaa, alimtaja, Paula Nelson Lujwangana (St. Mary's, Mazinde Juu, Tanga) kushika namba moja, akifuatiwa na Blandina Kessy Nyange (St. Mary's, Mazinde Juu, Tanga) na Eva J Shitindi (Machame Girls, Kilimanjaro), aliyeshika nafasi ya tatu.

Wengine ni Anita Zacharia Massawe (St. Mary's Mazinde Juu, Tanga), Latifa Mohammed Mrosso (Ahmes, Pwani), Mwanakombo Yusuph Ramadhani (Mtwara Girls, Mtwara) na Katarina Damasi Shao (Kisimiri, Arusha).

Wengine ni Pakusana Henry Chaula (St. Mary's Mazinde Juu, Tanga), Minnah K. Mtingwa (Fedha Girls, Mtwara) na Jasinntar R Deogratias.

**10 WAVULANA SANAA**

Alitaja 10 bora wavulana Lugha ya Sanaa kuwa ni Victor G Mtuli (Feza Boys Dar es Salaam), Ruhinda Benedicto (Machimu, Geita Adventist Geita), Doreen Lipambila (Bemjamin William Mkapa Dar es Salaam), Gift Mwakikusi (Tusiime, Dar es Salaam), Emmanuel Chila (Alpha,

INAENDELEA UK. 8



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Charles Msonda, akizungu cha sita. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Aliyekatali aongoza ki

**Na Mary Geofrey**

MTOTO aliyekataliwa na baba yake tangu akiwa mchanga, ameshika namba moja kitaifa katika matokeo ya mtihani wa kidato cha sita uliofanyika Mei, mwaka huu.

Mwanafunzi huyo, Faith Matee, ambaye ni mhitimu wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Mazinde Juu, mkoani Tanga, amepata daraja la kwanza pointi tatu baada ya kupata A katika masomo ya Fizikia, Kemia na Baiolojia (PCB).

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo bora kitaifa wa masomo ya sayansi, Sara Simon, ameeleza alivyomlea mwanawe huyo ambaye alikataliwa na baba yake toka akiwa na umri wa miezi miwili.

Akizungumza na Nipashe, Sara anayefanya kazi ya ukutubi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Mwenge, mkoani Kilimanjaro, alisema alimlea mwanawe kwa kutumia kipato kidogo alichokipata kwa kazi yake na hakupata ufadhili wowote.

"Faith ni mtoto wangu wa pekee. Baba yake tuliachana tangu akiwa na umri wa miezi miwili na sikuwa na fedha nyingi za kumsomesha bali nilijibana kwa ajili mtoto wangu apate elimu bora na hasa ukizingatia baba yake hajawahi kumsaidia kitu chochote," alisema Sara.

Alisema hata hivyo mtoto huyo alikuwa hapendi kwenda kwa baba yake wala kuzungumza naye lakini alikuwa akimsihi kumsalimia ingawa baba yake hakuonyesha kumjali.

Sara alisema alitarajia binti yake angefaulu lakini si kwa kiwango cha kuwa mwanafunzi wa kwanza kitaifa.

Alisema tangu akiwa shule ya msingi alikuwa akifanya vizuri katika masomo yake, licha ya kuwa alikuwa akipenda michezo, kuangalia luninga na kutembea.

HABARI KITAIFA




umnza na waandishi wa habari mjini Zanzibar jana, wakati akitoa matokeo ya kidato

# wa na baba dato cha 6

Sara alisema binti yake ambaye alisoma katika Shule ya Msingi Kiborloni Manispaa ya Moshi, Kilimanjaro ambayo ni ya serikali, baadae iligawanywa na kuwa Shule ya msingi Mnazi.

Kuhusu maendeleo ya kitaaluma, alisema Faith alikuwa akishika nafasi ya kwanza hadi ya tatu tangu akiwa shule ya msingi.

"Namshukuru Mungu, nina furaha ambayo siwezi kuieleza. Nimefurahi mpaka nimeishiwa nguvu. Sikuwahi kufikiria kuwa siku moja binti yangu atanitangaza kitaifa," alisema Sara.

Alisema binti yake ambaye yuko katika mafunzo ya kijeshi katika Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Kambi ya Maramba mkoani Tanga, mara nyingi amekuwa akimweleza kuwa ana ndoto za kuwa daktari.

**ALIVYOMPA TAARIFA**

Alisema kwa sababu hayupo naye, baada ya kupata taarifa hizo kutoka kwa uongozi wa shule, alituma ujumbe mfupi wa maneno kwa Mkuu wa kambi ya JKT Maramba kuwapa taarifa hiyo. "Wakati natuma ujumbe sikuwa nafahamu kuwa kumbe kaongoza kitaifa kawa mwanafunzi wa kwanza wa masomo ya sayansi ila naamini atapewa taarifa na kufurahi kama mimi," alisema Sara.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mazinde Juu, Mtawa Evetha Kilamba, aliiambia Nipashe kuwa sababu za kufanya vizuri katika matokeo hayo na kutoa mwanafunzi aliyeongoza kitaifa ni kufanya sala kila siku asubuhi kabla ya masoko kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi kisaikolojia.

Alisema jambo lingine ni mazingira rafiki ya wanafunzi kusoma katika shule hiyo, nidhamu ya kutosha na walimu kujituma kwa bidii.

"Nachoweza kusema wanafunzi bora katoka katika shule yetu ni sala tu wala si kukesha. Tunawafundisha watoto kusali ambako kunawaandaa kisaikolojia katika kuongeza bidii katika masomo yao, kuhakikisha wanajituma na kumtegemea Mungu. Lakini jambo la pili ni mazingira rafiki ya shule," alisema.

# Jangwani yajinasua kutoka mkiani

**Na Mary Geofrey**

SHULE ya Sekondari Jangwani, imejitoa kimasomaso kufuta historia mbaya ya kuburuza mkia katika matokeo ya kidato cha sita mwaka huu, baada ya mwaka jana kushika nafasi ya mwisho kati ya shule 10 zilizofanya vibaya.

Katika matokeo ya kidato cha sita mwaka huu, wanafunzi wake sita wamepata daraja la kwanza, 39 daraja la pili, 89 daraja la tatu, wawili daraja la nne na watatu daraja sifuri.

Kutokana na matokeo hayo ya mwaka jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alilazimika kubadili uongozi wa shule hiyo kwa madai ya kushindwa kusimamia ufaulu wa wanafunzi hao.

Pia Waziri Jafo aliwahamisha baadhi ya walimu wa shule hiyo na kuwapeleka katika shule zingine ndani na nje ya mkoa wa Dar es Salaam kwa kile alichoeleza kuwa walikuwa chanzo cha matokeo hayo mabaya,

Alisema shule hiyo iliyopo katikati ya Jiji la Dar es Salaam, yenye walimu wakutosha haikuwa na sababu ya kufanya vibaya katika matokeo hayo ila ni kwa sababu ya utovu wa nidhamu ulioshindwa kudhibitiwa na uongozi uliokuwapo.

Katika matokeo ya mwaka jana, mbali na Jangwani, shule zingine tisa zilizoshika nafasi 10 za mwisho ni Forest Hill (Morogoro), Jang' ombe (Zanzibar), St. James Kilolo (Iringa), White Lake (Dar), Aggrey (Mbeya), Nyailigamba (Kagera), Musoma Utalii (Mara), Ben Bella (Zanzibar) na Golden Ridge (Geita).

Hata hivyo, shule hizo zote zimejinasua katika kundi hilo na kupanda ngazi zaidi baada ya wanafunzi wao kufanya vizuri kulinganisha na mwaka jana.

Katika matokeo ya mwaka huu, shule 10 za mwisho zilizoshika mkia na mikoa zinakotoka ni Nyamunga (Mara), Haile Salassie (Mjini Magharibi, Unguja), Tumekuja (Mjini Magharibi), Bumaangi (Mara), Butuli (Mara), Mpendae (Mjini Magharibi), Eckernford (Tanga), Msimbo (Katavi), Mondo (Dodoma) na Kiembe Samaki (Mjini Magharibi).

Matokeo yaliyotangazwa jana na Baraza la Mitihani ya Taifa (Necta), yalionyesha ufaulu umepanda kidogo kwa asilimia 0.74 ikilinganishwa na mwaka jana ambao ulikuwa 97.58 huku wasichana waking'ara zaidi katika masomo ya sayansi kuliko wavulana.

Aidha, ubora wa ufaulu huo umezidi kuimarika kwa kuwa idadi ya watahiniwa waliofaulu vizuri katika daraja la kwanza, pili na tatu imeongezeka kwa asilimia 1.09 kutoka asilimia 95.52 mwaka jana hadi asilimia 96.61 mwaka huu.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Charles Msonde, akitangaza matokeo hayo, alisema ubora wa ufaulu wa wasichana kwa mwaka huu umezidi ule wa wavulana kwa asilimia 1.07.

# Mwanafunzi bora wa pili Sayansi aeleza siri ufaulu

**Na Romana Mallya**

MWANAFUNZI bora wa pili kitaifa katika masomo ya Sayansi, Herman Kamugisha, amesema matokeo hayo aliyopata yametokana na ushawishi mkubwa kutoka kwa walimu wake ambao wakati wote walimtaka asome zaidi ili aingie kwenye 10 bora kitaifa.

Akielezea historia ya Herman ambaye baada ya kupokea simu ya mwandishi alisema alipomaliza darasa la saba, baba yake mzazi ambaye mara ya mwisho kuwasiliana naye ilikuwa Desemba mwaka 2012, alitaka aende kidato cha kwanza shule ya seminari.

"Lakini matokeo yalipotoka nilichagua kwenda shule niliyochaguliwa ambayo ni Mpwapwa iliyopo Dodoma, kitendo hicho kilimfanya baba anitamkie kuwa kuanzia siku hiyo nitambue kuwa yeye siyo baba yangu mzazi. Nilipofika kidato cha tatu alipiga simu kuomba msamaha kwa kauli aliyotoa, baada ya hapo hajawahi kuwasiliana tena nasi, alisema.

Herman ambaye wakati akizungumza na Nipashe alikuwa nyumbani kwa baba yake mdogo Kihonda Morogoro, alisema aliendelea na masomo na alipomaliza shuleni hapo alichaguliwa kuingia kidato cha tano katika Shule ya Kisimiri, Arusha.

"Matokeo haya ya kuingia kwenye ushindi kitaifa niwe mkweli sikuyatarajia. Nilichotarajia ni kupata daraja la kwanza, lakini siyo kuingia kitaifa kwa sababu somo la Kemia lilikuwa gumu...ila walimu wangu kwa sababu walikuwa wanajua uwezo wangu mara kwa mara walinitaka nisome zaidi ili niwe miongoni mwa wanafunzi bora kitaifa...nimefurahi ndoto za walimu wangu wa Kisimiri zimetimia, ninashukuru Mungu sana na nawashukuru walimu, mama, baba mdogo," alisema.

Herman alisema alipokea matokeo hayo mara tu alipoamka na kuingia kwenye kundi la wanafunzi wenzake lililopo WhatsApp.

"Nimepokea pongezi nyingi kutoka kwa watu mbalimbali na wanafunzi wenzangu. Wito wangu kwa wanafunzi wasikatishwe tamaa na matokeo ya shuleni, mara nyingi huwa tunakata tamaa unapofanya mtihani shuleni ukapata ambacho hukutarajia, kazeni msuli, mumuombe Mungu hakuna kinachoshindikana hajalishi unapita katika mitihani gani ya maisha," alisema Herman.

Mwanafunzi huyo alisema matarajio yake baada ya kumaliza chuo kikuu ni kuwa mhandisi wa ndege.

Alisema wakati akisubiri matokeo amekuwa akifundisha wanafunzi kidato cha tatu na cha nne nyumbani kwao.

# Mfumo utoaji vitambulisho taifa kuboreshwa

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema inafanyia kazi uboreshaji wa mifumo ya utoaji wa vitambulisho vya taifa vinavyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) ili wananchi wengi zaidi wapate haki yao ya utambulisho.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe, iliyotaka kujua hatua zinazochukuliwa katika kuhakikisha Watanzania wanapata vitambulisho vya taifa kwa wakati na bila usumbufu.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha Mtanzania halisi anatambulika ndiyo maana wameanza kusambaza na kutoa vitambulisho hivyo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Suala la kasi inategemea kukamilika kwa uhakiki wa taarifa maana hatuwezi kutoa tu kitambulisho hata kwa ambao si Watanzania. Pia tunaendelea kufanyia kazi changamoto ya mifumo," alisema.

Kwa sasa, ili Mtanznaia asajiliwe namba ya simu ni lazima kwa mfumo wa elektroniki, kupata pasi ya kusafiria na kufungua biashara ya pesa kielektroniki, ni lazima awe na kitambulisho cha utaifa au namba ya uraia.

Aidha, kwenye ofisi mbalimbali za Nida, kuna foleni ndefu za wananchi wanaotafuta vitambulisho, kufuatilia namba za uraia baada ya kujiandikisha, kupata vitambulisho vipya kwa waliopoteza au kuibua na kupata vitambulisho halisi kwa waliojiandikisha.

Nipashe ilishuhudia wananchi wakiwa kwenye mistari mrefu na foleni kwa muda mrefu katika ofisi za Nida eneo la Kawe na utaratibu wa kupata namba ya uraia ni kuanzia wiki tatu na kuendelea huku uwezekano wa kupata kitambulisho kamili ukiwa haujulikani.

Baadhi ya wananchi waliiambia Nipashe kuwa ni vyema serikali ikaboresha mchakato huo katika kipindi hiki ambacho kitambulisho cha taifa ndicho kinatumiwa

INAENDELEA UK. 8



Kundi la wafanyakazi wa moja ya kampuni za udalali wakimnyang'anya pikipiki mwendesha bodaboda aliyekuwa anapita eneo la Ilala Mchikichini na abiria wake jijini Dar es Salaam kwa madai kuwa hakuwa na kibali cha kuvuka eneo hilo kuingia Kariakoo. Hata hivyo vurugu hizo zilitulizwa na polisi baada ya kufyatua mabomu ya machozi. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Bosi Tume ya Madini mbaroni madai wizi dhahabu ya mil. 500/-

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, linamshikilia Meneja wa Maabara wa Tume ya Madini, Dornald Njonjo (30), kwa tuhuma za kuiba madini ya dhahabu mali ya serikali kilogramu 6.244 yenye thamani ya Sh. 507,347,000.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa madini hayo yalikuwa yamehifadhiwa kwenye kasiki katika ofisi za Wakala wa Madini Masaki jijini Dar es Salaam.

Alisema Juni 29, mwaka huu Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa Ofisa Madini Mkoa wa Dar es Salaam, Ally Sadick, baada ya kugundua kuibiwa madini hayo ya dhahabu.

"Jeshi la Polisi baada ya kupata taarifa hizi lilianza uchunguzi mara moja na kubaini kuwa madini hayo yaliibiwa na Dornald. Alianza kuiba tangu Desemba 2018," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema baada ya mtuhumiwa kuhojiwa, alikiri kuiba madini hayo kidogo kidogo ambayo yalikuwa yamehifadhiwa kwenye chumba katika jengo la ofisi hizo za Masaki.

"Mtuhumiwa alieleza kuwa madini hayo aliyauza katika duka la kuuzia vito vya dhahabu kisha kuhifadhi madini bandia yenye uzito wa kilo 6.001 nyuma ya jengo la Tume ya Madini ili kuyapeleka katika chumba walichoiba madini hayo halisi kwa lengo la kuyabadilisha," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema madini hayo halisi ya dhahabu yalikamatwa mwaka 2017 maeneo ya bandarini Zanzibar yakiwa yanasafirishwa kinyume cha sheria kisha kutaifishwa na serikali na kuhifadhiwa katika ofisi za Tume ya Madini.

"Jeshi la Polisi lipo katika hatua za mwisho kukamilisha utaratibu wa kupeleka jalada kwa mwendesha mashtaka wa serikali ili mtuhumiwa afikishwe mahakamani," alisema. Kamanda Mambosasa alitoa onyo kwa watumishi waliopewa madaraka na serikali halafu wanageuka kuiibia, kuwa hawana nafasi na kila mmoja ajionye kwenye nafasi yake.






# Utata kutekwa kwa msaidizi wa Membe

**Na Romana Mallya**

KAMANDA wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, amesema tukio la madai ya kutekwa kwa Allan Kiluvya, msaidizi wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bernard Membe, lina shaka kubwa.

Allan anadaiwa kutekwa na watu wasiojulikana siku tano zilizopita na kujitokeza polisi Jumatatu kuripoti kuwa waliomteka wamemuachia huru.

Akizungumzia jana kuhusu tukio hilo, Kamanda Mambosasa alisema ingawa Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi, lakini kauli ya Allan kuwa aliwaelekeza watekaji mahali pa kumshusha linawatia shaka.

"Tunaendelea na uchunguzi ili kubaini hicho kinachosemwa na mhusika kuwa alitekwa. Ukiangalia `clip' baba anasema mtoto alipigwa sana. Mtoto anasema yeye ni mzima hajateswa."

"Ukienda zaidi anatoa ushirikiano kwa watekaji wamshushe wapi? Wamshushe karibu na nyumbani. Kwa hiyo ni watu marafiki wanaongea lugha moja, ndiyo maana hili sikutaka kulisemea leo kwenye taarifa zangu ila tunaendelea na upelelezi," Kamanda Mambosasa alisema akijibu swali la mwandishi wa habari.

Aliongeza: "Mashaka ni makubwa, nimekupa tu vionjo, tunaendelea na upelelezi, mtu aliyekuteka huwezi kumchagulia pa kukushusha, lakini mtekaji hawezi kuwa rafiki kukupeleka karibu na nyumbani. Mtakumbuka tukio lililopita (mfanyabiashara Raphael Ongangi) alitekwa akapelekwa Kenya karibu na nyumba ya shangazi yake."

Tukio la Ongangi, raia wa Kenya aliyedaiwa kutekwa maeneo ya Oysterbay jijini Dar es

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Shahidi adai kubaini kuhamishwa fedha kwenda akaunti ya Aveva

**Na Hellen Mwango**

MCHUNGUZI wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Frank Mukilanya, amedai mahakamani katika kesi dhidi ya vigogo wa Klabu ya Simba, akiwamo aliyekuwa Rais Evance Aveva kwamba alibaini Dola za Marekani 300,000 zilitolewa katika akaunti ya klabu kwenda akaunti binafsi ya Aveva.

Kadhalika, amedai kuwa katika uchunguzi wake, alibaini fedha hizo zilihamishwa kutoka akaunti ya klabu iliyoko benki ya CRDB kwenda akaunti ya Aveva, benki ya Barclays baada kupitia nyaraka mbalimbali za klabu hiyo.

Shahidi huyo alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo.

Akiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Leonard Swai, shahidi alidai kuwa aliagizwa na bosi wake kufanya uchunguzi wa Dola za Marekani 300,000 za klabu ya Simba.

Alidai kuwa uchunguzi huo unahusu kuhamishwa fedha hizo kutoka benki ya CRDB akaunti ya klabu kwenda Barclays, kwenye akaunti ya Aveva.

Mukilanya alidai kuwa alichukua nyaraka mbalimbali kwa lengo la kuona kama fedha kweli zilikuwapo na zilihamishiwa kwa nani.

Alidai kuwa kwa mujibu wa nyaraka hizo zilionyesha kwamba Machi 15, 2016 fedha zilitoka CRDB kwenda Barclays na wahusika wakuu ni Aveva na aliyekuwa Makamu wa Rais wa Simba, Godfrey Nyange, maarufu kama Kaburu, na maombi yaliandikwa na klabu hiyo.

INAENDELEA UK.8



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa tuzo za awamu ya tisa za kuonyesha hadithi za mafanikio ya wajasiriamali wadogo nchini Tanzania. Wengine ni Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Mfuko wa Kuendeleza Huduma za Fedha (FSDT), Irene Madeje (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Ltd, Francis Nanai (wa pili kulia) na Mkurugenzi Mshiriki wa KPMG, Antony Nzamu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Jela miaka mitatu mauaji ya kakaye

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imemhukumu Rukia Ally, kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri kosa la kumuua kwa kisu kaka yake wa damu bila kukusudia.

Mahakama hiyo ilitoa hukumu hiyo baada ya kupewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji na kumkuta mshtakiwa na hatia ya kosa hilo.

Hukumu hiyo ilisomwa jana chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Akitoa hukumu hiyo alisema kwa sababu mshtakiwa amekiri makosa yake mahakama yake inamtia hatiani.

"Kwa kuwa mshtakiwa umekiri makosa yako bila kuisumbua mahakama, umekaa mahabusu muda mrefu, mahakama yangu imekutia hatiani na kukuhukumu kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka mitatu kwa kumuua kaka yako bila kukusudia," alisema Naibu Msajili Mazengo.

Awali kabla ya hukumu hiyo kutolewa, upande wa mashtaka uliomba kubadilisha hati ya mashtaka kutoka mauaji ya kukusudia, kuwa kesi ya mauaji ya bila kukusudia.

Ilidaiwa kuwa Januari 23, 2015, Tegeta Mivumoni Madale, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alimuua bila kukusudia kaka yake Saidi Ally.

Mshtakiwa alikiri kosa la kumuua kaka yake kwa kisu bila kukusudia.

Wakili wa Serikali, Mwasiti Ally, alidai kuwa mshtakiwa na marehemu ni ndugu wa damu na kwamba wamezaliwa kwa baba na mama mmoja.

Alidai kuwa walikuwa wakiishi na wazazi wao wote wawili, Mivumoni jijini

INAENDELEA UK.8

# Msako kodi ya pango ardhi watua Geita

**Na Munir Shemweta,** GEITA

OPERESHENI maalum inayofanywa na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, kupita ofisi moja hadi nyingine kuzibana taasisi na kampuni zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi imeangukia Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML) ulioko mkoani Geita.

Katika operesheni hiyo, imebainika kuwa mgodi huo hauna hati miliki ya eneo hilo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 196.27 sawa na takriban hekta 19,927 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, hivyo kushindwa kulipa kodi ya pango la ardhi.

Akiwa katika ziara yake ya siku moja mkoani Geita juzi, Dk. Mabula alitembelea mgodi huo wa dhahabu kwa lengo la kufuatilia ulipaji kodi ya pango la ardhi sambamba na kuangalia kama mgodi huo una hati miliki ya ardhi katika eneo hilo.

Dk. Mabula alielezwa na Mshauri wa Masuala ya Sheria ya Mgodi huo, Elizabeth Karua, kuwa GGML imekuwa ikilipa kodi mbalimbali serikalini lakini haijawahi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kuwa ina leseni maalum ya uchimbaji madini. Kwa mujibu wa Karua, mgodi wa Geita ambao uko chini ya kampuni ya Ashanti AngloGold ya Afrika Kusini, katika kipindi chote cha shughuli zake haujawahi kupewa wito wa kutakiwa kulipa kodi ya pango la ardhi na umekuwa ukizingatia mkataba wa uendelezaji uchimbaji madini.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, alisema kodi ya pango la ardhi inapaswa kulipwa na haina uhusiano wowote na leseni za uchimbaji madini kwa kuwa mmiliki wake anakuwa kama amepangishwa eneo. Pia alisema sheria ya Tanzania imetamka bayana kuwa ardhi itakuwa chini ya Rais na kusisitiza kuwa kodi ya pango la ardhi inalipwa kama zinavyolipwa ankara za umeme na maji.

Kwa mujibu wa Masami jambo la muhimu katika suala la kodi ya pango la ardhi ni umilikishwaji na kwamba mgodi wa Geita unatakiwa kutambulika kwa kuwa na nyaraka sahihi za umiliki na kusisitiza tafsiri ya sheria ya madini si sehemu ya ardhi.

Pamoja na kuipongeza GGML kwa kuwa mlipaji mzuri wa kodi za serikali, Dk. Mabula alisema eneo la mgodi huo linapaswa kipimwa kutokana na kuwa katika mipango miji na sheria yake inaelekeza maeneo yote ya mipango miji kipimwa na kupangiwa matumizi.

"Eneo la mgodi lazima lipimwe na kupangwa kwa kuwa ndani ya mgodi kuna maeneo ya makazi, ofisi na matumizi mengine. Vyote hivyo lazima vionyeshwe katika ramani," alisema.

Pia alisema upimaji katika mgodi huo una faida kubwa kwa kuwa utaondoa migogoro ya ardhi ambayo baadhi yake husababishwa na wananchi kuingia maeneo ya mgodi. Alitolea mfano mgodi wa Nyamongo ulioko Tarime mkoani Mara baada ya kupimwa umeepusha migogoro iliyokuwa ikitokea sambamba na kulipa kodi ya pango la ardhi na kuutaka mgodi wa GGML kueleza ni lini utakuja na majibu wa kutaka kupimwa eneo lake. Kutokana na kauli ya Naibu Waziri, Karua aliomba mgodi huo kupewa wiki mbili kushauriana na uongozi wa juu kuhusiana na suala hilo kwa kuwa ujio wake ulikuwa wa kushtukiza.

Kutokana na ombi hilo, Dk. Mabula aliupa mgodi huo hadi Julai 29, mwaka huu kuja na majibu kuhusiana na suala hilo. Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Richard Jordison, alisema ofisi yake iko tayari kushirikiana na wizara kuhakikisha suala hilo linafikia mwafaka ili kuondoa migogoro.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**KESI YA MADAI 73 YA MWAKA 2019**
**HELLMAN WORLDWIDE LOGISTICS (T) LIMITED.........MDAI**
**DHIDI YA**
**DAVE IMPEX LIMITED ...........MDAIWA**

**KWA:**
THE MANAGING DIRECTOR
DAVE IMPEX LIMITED - POPOTE ULIPO

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo Unahitajiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au kwa Wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe **01/08/2019 saa 07:00 mchana**.

**ANGALIA:**

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, itaweza kutoa hukumu bila uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **04** Mwezi wa **JULAI 2019.**

**HAKIMU MKAZI MKUU**
**KISUTU -DAR ES SALAAM**

215320402

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tusiishie katika ununuzi wa magari ya Zimamoto

**KUNA** taarifa kuwa Serikali ipo kwenye mazungumzo na nchi mbalimbali kwa ajili ya kupata mkopo nafuu wa kununua magari na vifaa vingine vya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kukabiliana na majanga ya moto nchini.

Mpango huo ulibainishwa juzi jijini Dodoma na Kamishna wa Utawala na Fedha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, Mbaraka Semwanza, wakati akifungua kikao cha ndani cha kiutendaji, ikiwamo kutoa maelekezo kwa maofisa, askari na watumishi raia wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Alisema serikali inajua umuhimu wa jeshi hilo hapa, ndiyo maana inafanya mazungumzo ili kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana kwa ajili ya kusaidia katika majanga mbalimbali ya moto yanayotokea. Aliongeza kuwa Serikali inatambua kazi linazofanya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, hivyo wanajitahidi kuhakikisha vifaa hivyo vinapatikana kusaidia utendaji kazi kwa urahisi zaidi. Alisema upande wa changamoto wa sare za jeshi hilo, tayari mkataba umeshasainiwa na zinaendelea kushonwa ili ziweze kutumiwa na jeshi hilo. Kwamba sare zimeanza kushonwa, na kwamba ana imani changamoto kwa upande huo muda si mrefu itakuwa imekwishwa.

Hatua ya ununuzi wa magari ni ya umuhimu mkubwa wa wananchi, ingawa kusema ukweli utekelezaji wake umechelewa sana, kwa kuwa wananchi wamekuwa wakililalamikia Jeshi hilo kutokana na kukosekana kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Wengi wamekuwa na uelewa kuwa ni Jeshi la Zimamoto, hivyo jukumu lake ni kushughulikia majanga yatokanayo na moto bila kuelewa kuwa jina lake halisi ni Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; kwa maana kwamba lina jukumu la kushughulikia majanga mengine yanayohitaji uokoaji.

Kimsingi, katika suala zima la majanga ya moto kuna uhaba mkubwa wa magari, hivyo Jeshi hilo kutokumudu kukabiliana nayo inavyostahili. Mara kadhaa kunapokuwapo ajali za moto, wananchi wamekuwa wakilalamikia uchelewaji wa magari na wakati mwingine kutofika kabisa katika maeneo ya matukio hayo, hivyo majengo kuteketea kabisa.

Lakini pia hata yanapowahi, wananchi wamekuwa wakilalamikia kasi ndogo ya kuudhibiti moto kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na maji ya kutosha, na magari hayo kuonekana kukosa baadhi ya vifaa.

Kamishna Jenerali wa Jeshi hilo, Thobias Andengenyae, aliwahi kusema kuwa magari waliyonayo hayatoshi, hivyo kusababisha kukosekana ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Tunaamini kuwa yatanunuliwa magari ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya nchi nzima. Pia ugawaji wake uzingatie mahitaji kwa mfano ngazi za mikoa, na halmashauri.


Ni uamuzi mzuri kushughulikia uhaba wa sare kwa askari wa Jeshi hilo, lakini tunaona kuwa kuna mambo mengine zaidi yanayohitajika katika mpango mzima wa kuliboresha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Baadhi ya mambo yanayohitaji kupatiwa kipaumbele ni uboreshaji wa maslahi ya askari kwa maana ya posho, mishahara na mahitaji mengine. Kadhalika, vinahitajika vifaa vya kutosha na vya kisasa vya kukabiliana na majanga mengine zaidi ya moto.

Kwa kuwa kuna ongezeko kubwa la shughuli za uzalishaji na huduma katika sekta mbalimbali kama migodi, viwanda, mashamba makubwa, ujenzi wa majengo marefu, usafirishaji ambazo ni rahisi kutokea kwa majanga, tunaona kwamba ni wakati mwafaka kuwa na vifaa vya kisasa kama helkopta za uokoaji na vingine. Tunashauri uwapo wa mpango maalum madhubuti ambao utabainisha mahitaji ya msingi ya Jeshi hilo kisha uwasilishwe serikalini na mamlaka husika ili fedha zitengwe kwa ajili ya utekelezaji. Bila shaka kwa kufanya hivyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaweza kutekeleza majukumu yake kwa tija na ufanisi mkubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

### Sawa mabasi usiku lakini...

Na Salome Kitomari

**UAMUZI** wa serikali kuruhusu mabasi kusafiri kwa saa 24 ni habari njema kwa wasafiri wa mikoa ya kanda ya ziwa ambao walilazimika kulala njiani ili kufika mwisho wa safari zao.

Hali hiyo ilikuwa ngumu kwa wasafiri na madereva kwa kuwa maeneo waliyolala hayakuwa na huduma muhimu na wote walilazimika kulala kwenye mabasi kwa kuwa safari huendelea alfajiri ya siku inayofuata na wakati mwingine hakuna malazi ya kutosheleza.

Kwa anayekwenda Mwanza, Bukoba, Kahama au Kigoma kwa shughuli za kikazi alitakiwa kusafiri siku mbili kabla ili aweze kupata muda wa kupumzika na kuwahi kikao au mkutano vinginevyo angekwama.

Kwa sasa magari ya njia hizo yameruhusiwa kusafiri muda wote, hakuna kulala njiani, ni jambo zuri lakini linahitaji ufuatiliaji wa karibu sana kwa kuwa upo uwezekano mkubwa wa mambo yasiyofaa kwenye sekta ya usafiri kuibuka.

Kwanza ni magari kufanyakazi bila kupumzika wala kufanyiwa matengenezo ya kutosha, kwa kuwa kwa sasa mabasi hayo yalifanyakazi muda wote kwa kuwa baada ya kufika mwisho wa safari madereva huyakabidhi kwa msimamizi ambaye huyapeleka kwenye matengenezo.

Hiyo ni pamoja na kuyajaza mafuta kwa ajili ya safari siku inayofuata.

Yaani gari inayotoka Mwanza ikifika Dar es Salaam saa 7:00 usiku baada ya kushusha abiria inapelekwa kwenye matengenezo na kujazwa mafuta kwa ajili ya safari siku inayofuata.

Aidha, madereva huenda kupumzika wakati magari yakifanyiwa matengenezo na kuandaliwa kwa ajili ya safari za siku inayofuata

**Yaani gari inayotoka Mwanza ikifika Dar es Salaam saa 7:00 usiku baada ya kushusha abiria inapelekwa kwenye matengenezo na kujazwa mafuta kwa ajili ya safari siku inayofuata.**

na hapo hupumzika kwa saa nne pekee na kuanza safari nyingine ndefu.

Licha ya kwamba wanapokezana lakini bado wanahitaji kupumzika kiliko kila siku kuwa barabarani jambo ambalo ni hatari kwa kuwa yapo mambo yanaweza kutokea kutokana na uchovu wa binadamu unaombatana na kukosa usingizi.

Jingine ni suala la mwendo, licha ya kuwapo kwa ving'amuzi au GPS zinazofuatilia mwendo wa basi la abiria usizidi kilomita 80 kwa saa, lakini Mamlaka ya Usafiri wa Ardhini (Latra), imeeleza baadhi ya mabasi yanachezea vifaa hivyo ili yatembee kwa mwendokasi.

Jingine ni suala la kukosa uadilifu kwa askari watakaokuwa na wajibu wa kusindikiza au kulinda maeneo yanayoonekana kuwa hayana usalama wa kutosha na kwamba ili kuepusha ajili na makosa mengine ya barabarani wanahitajika askari wenye maadili ya kutosha katika kutekeleza majukumu yao. Jingine ni uzembe wa madereva wa mabasi na malori yatakayokuwa yanasafiri usiku na kwa wakati huo ni muda wa malori kusafiri na kwakuwa hakutakuwa na udhibiti wa mwendo hasa kwenye maeneo ya kilomita 50 kwa saa.

Ni jambo jema kwa mabasi kusafiri muda wote lakini ni vyema tahadhari ikachukuliwa kuhakikisha kwamba huduma za usafiri kwa nyakati hizo inakuwa salama na siyo chanzo cha kuteketeza maisha ya Watanzania na kuacha majeruhi na wategemezi wengi.

Hasara inayotokana na ajali za barabarani ni kubwa kwa kuwa familia huwa na mzigo mzito wa kuuguza ndugu, kulea, kusomesha na kuwapatia mahitaji maalum watoto wa marehemu.

Aidha, ikumbukwe ajali husababisha wenye ulemavu na wategemezi ambao hufilisika kutokana na kupoteza uwezo wa kufanyakazi.



Mshtakiwa Rukia Ally, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, kwa kosa la kuua bila kukusudia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbaroni tuhuma za kubambwa na meno ya tembo ya mil. 30/-

**Na Ibrahim Yassin,** SONGWE

WATU watatu, wakiwamo wawili raia wa Malawi, wamekamatwa na polisi kwa tuhuma za kukutwa na vipande 17 vya meno ya tembo vyenye uzito wa kilo 33.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alisema jana ofisini kwake kuwa watuhumiwa hao wamekamatwa katika kijiji cha Lungwe B Wilaya ya Ileje mpakani na nchi ya Malawi, huku ikidaiwa kuwa meno hayo yametolewa Malawi.

Kyando alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa na mzigo huo kwenye nyumba ya Mtanzania chumbani kwake na kwamba ulidaiwa kuuzwa kwa Sh. milioni 30.

Sambamba na watuhumiwa hao, Kamanda Kyando alisema polisi pia wamewakamata watu wanne wakituhumiwa kwa mauaji ya watu wawili wilayani Momba na Mbozi ambao walikuwa wamekatwa kichwa, mikono na tumbo.

"Tumewakamata watu wanne majina yao tumeyahifadhi kwa sababu za kiuchunguzi. Wamefanya mauaji ya watu wawili ambao waliwaua na kuwakata sehemu za miili yao," alisema Kyando.

Kamanda Kyando ametoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Songwe kutoa taarifa ya biashara hizo haramu pamoja na matukio mbalimbali ya kihalifu huku akisisitiza kuwa Jeshi la Polisi litaendelea kupambana kuhakikisha mkoa unakuwa salama.

Wananchi kwa upande wao, wamepongeza hatua hiyo wakisema kuwa iko haja jeshi hilo kuendelea kufanya msako wa mara kwa mara ili kubaini matukio zaidi ya biashara haramu na mauaji ya kinyama.

# Mambosasa aanika chanzo uhalifu Ukonga

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam limesema matukio ya uhalifu yanayoendelea Ukonga jijini humo, yanasababishwa na historia ya eneo husika kuwa wananchi wake ni baadhi ya wahamiaji wahalifu kutoka Tarime na Rorya mkoani Mara.

Kamanda wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukamatwa kwa watuhumiwa wa ujambazi saba Ukonga.

Akijibu swali lililotaka kujua kwa nini matukio Ukonga, Mambosasa alisema historia ya maeneo hayo ni ya wahamiaji.

"Ukonga kuna historia inayofahamika. Maeneo yale ni ya uhamiaji, nimepata bahati kufanya kazi wanakotokea kule Tarime na Rorya kama kamanda wa polisi. Watu walihama kule wakahamia Ukonga na wahalifu wanapotenda makosa kule wanakuja Ukonga kufikiria ni mahali salama kwa kujificha," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema Jeshi la Polisi limekuwa likiendelea kuwachambua.

"Afanye uhalifu mahali popote aje kujificha popote, iwe Ukonga au sehemu yoyote, tunaendelea kufuatilia. Hakuna mahali ambako mhalifu atajificha akabaki salama. Tutaendelea kuwafuatilia lakini na kushughulika na mmoja mmoja mpaka kieleweke," alisema.

Mambosasa alisema kikosi kazi, kamanda wa kanda maalum na wa mikoa ya kipolisi ndani ya mkoa huo ya Temeke, Kinondoni na Ilala, wote wako kazini ndiyo maana kuna hali ya usalama.

Alisema Dar es Salaam ya awali ilikuwa na vurugu, watu walikuwa wanapigwa risasi ovyo, wanavamiwa kienyeji na kuporwa lakini sasa kikosi kazi kiko kazini.

Kuhusu kukamatwa watuhumiwa saba wa ujambazi, Kamanda Mambosasa alisema walikutwa na bajaji mbili za wizi pamoja na vifaa mbalimbali.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Said Salum (27), Amo Kefas (30), Said Ahmad (38), Mohamed Musa (31), Mboke Samwel (26), Abdallah Kipaneli (25) na Mfaume Mussa (25).

"Walikamatwa Jumanne wiki hii saa nane usiku maeneo ya Kibeberu na Magole Ukonga. Walivunja maduka matatu na kuiba bidhaa mbalimbali, fedha na bajaji mbili zenye namba za usajili MC 312 CFB aina ya TVS na MC 540 CED aina ya TVS zote zikiwa na rangi ya bluu," alisema.

Mambosasa alisema siku iliyofuata, watuhumiwa hao walikamatwa maeneo ya Hondogo Gogoni, Kiluvya wilaya ya Ubungo.

Kamanda Mambosasa alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakifanya matukio ya uhalifu kwa kutumia gari aina ya Toyota Harrier lenye namba za usajili T 666 DJG lenye rangi nyeusi ambalo alisema linashikiliwa na polisi ili kumbaini mmiliki wake.

Katika tukio lingine, Kamanda Mambosasa alisema wamemkamata Michael Nina, mkazi wa Tangi Bovu, akiwa na bastola FATIN 13- TURKEY yenye namba T.0622010J00535 ikiwa na risasi tisa ndani ya Magazine ambayo inasadikika kutumika katika uhalifu.

Alisema mtu huyo alipohojiwa alidai silaha hiyo alipewa na mwenzake ambaye anamfahamu kwa jina la mama mdogo ambaye naye Jeshi la Polisi linamsaka.

Kuhusu tukio lililotokea jengo la Quality Centre hivi karibuni, Kamanda Mambosasa alisema walipokea taarifa kuwa kuna watu wamevamia hapo lakini polisi wa kikosi cha Tazara na Uwanja wa Ndege vilifika hapo na wakati akitaka kumkamata mtuhumiwa huyo, mhalifu huyo alipiga kelele za wizi.

"Huyu mhalifu alipowaona askari hao akaanza kupiga kelele za mwizi, akimaanisha polisi ni wezi ili ajihami nao, lakini alikamatwa," alisema.

# Polisi wavujisha siri wawekwa mtegoni

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amewaagiza makamanda wa polisi nchini kuwachukulia hatua askari wanaoshirikiana na wahalifu kwa kuvujisha siri za watoa taarifa.

Masauni aliyasema hayo wakati akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Kangeme Kata ya Uloa wilayani Ushetu mkoani Shinyanga.

Naibu Waziri huyo amekwenda mkoani humo baada ya kukithiri kwa matukio ya uhalifu yakiwamo ya uporaji wa fedha, uvunjwaji wa nyumba na ubakaji.

"Haiwezekani tunapambana na uhalifu halafu leo anatokea askari anakuwa wakala wa wahalifu. Askari hao wachache wanalichafua Jeshi la Polisi. Naagiza ma-RPC (makamanda wa polisi wa mikoa) wote nchini kuwachukulia hatua askari polisi wachache wanaotoa taarifa wanazoletewa na wananchi kwa wahalifu," alisema.

Masauni alisema wananchi wamekuwa waoga wa kupeleka polisi taarifa za uhalifu kwa kuhofia kuvujishwa kwa wahalifu.

"Askari mmekula viapo vya maadili na utiifu, mnalipwa mishahara kwa kodi za wananchi hawa. Wasaidieni ili wafanye shughuli zao kwa amani na salama na si kujawa na hofu," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Richard Abwao, aliwaomba wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kuzuia uhalifu na kuwataka wasikatishwe tamaa na askari wachache ambao si waadilifu.

"Njooni leteni taarifa hata kwangu nitazifanyia kazi na ninawaahidi sitamvumilia askari yeyote katika mkoa huu atakayethibitika kuvujisha taarifa za siri kwa wahalifu. Vijana unganeni kutengeneza vikundi vya sungusungu mje tuwape elimu ya kupambana na uhalifu," alisema. Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakazi wa kijiji hicho walisema wanaogopa kutoa taarifa za wahalifu kwa polisi wakihofia usalama wa maisha yao.

# Jela miaka mitatu mauaji ya kakaye

INATOKA UK. 5

Dar es Salaam.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa siku ya tukio jioni, wakati wa uhai wake marehemu alirudi nyumbani kutoka kwenye shughuli zake na kumkuta dada yake (mshtakiwa) amerejea baada ya kutoweka nyumbani kwa siku tatu.

Ilidaiwa kuwa Saidi (marehemu) alimgongea mshtakiwa chumbani kwake na alimhoji alikuwa wapi siku zote tatu, lakini mshtakiwa hakujibu chochote.

Saidi alianza kumchapa miguuni dada yake huku akiwa ameshika kisu mkononi.

Hata hivyo, mshtakiwa alifanikiwa kumpokonya kisu kaka yake na kujihami kwa kumchoma kifuani upande wa kushoto na kisha kukimbia.

Ilidaiwa kuwa baada ya kuchomwa kisu alitokwa na damu nyingi na alipofikishwa Hospitali ya Mwananyamala vipimo vilionyesha amefariki dunia.

Mama mzazi na majirani walitoa taarifa polisi na mshtakiwa alikamatwa na kufunguliwa mashtaka.

Mshtakiwa alikiri maelezo ya Jamhuri kwamba tukio lilikuwa hivyo kama upande wa Jamhuri ulivyoeleza.

Upande wa utetezi ukiwasilisha hoja za mshtakiwa kupunguziwa adhabu, ulidai unaomba mshtakiwa apunguziwe adhabu kwa sababu bado mdogo anategemewa kwenye ujenzi wa taifa.

Ulidai kuwa mshtakiwa aliyekaa mahabusu tangu mwaka 2015 mpaka jana ameshajutia na amejifunza muda wote aliokaa mahabusu.

Mshtakiwa alikuwa anajitetea hakumuua kaka yake kwa makusudi kwa kuwa kisu kilichotumika kutenda kosa kilikuwa mikononi mwa marehemu mwenyewe.

Upande huo wa utetezi ulidai kuwa wazazi wa mshtakiwa walijaliwa kupata watoto wawili na kwamba baada ya mmoja kufariki mshtakiwa ni mtoto pekee akifungwa familia itabaki na simanzi.

Naibu Msajili alisema mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka mitatu.

## Mfumo utoaji vitambulisho taifa kuboreshwa

INATOKA UK. 4

kwenye utambulisho wa maeneo mbalimbali, ikiwamo kwenye biashara.

"Tangu alfajiri nipo kwenye foleni kwa ajili ya kupiga picha na kuchukuliwa alama za vidole. Watumishi wa hapa wanajitahidi lakini ni wachache sana ukilinganisha na wananchi waliopo," alisema Neema John.

Aidha, kwa wanaofuatilia vitambulisho, walisema vinachukua muda mrefu kuvipata na kwamba hali hiyo inakwamisha utekelezaji wa majukumu mengine kama kubadili namba za simu za biashara za fedha kwa elektroniki.

Nipashe ilitembelea tovuti ya Nida ili kupata taarifa mbalimbali ikiwamo uwezekano wa kutoa nakala ya kitambulisho kwa aliyekwisha kujiandikisha, lakini hakukuwa na taarifa za kumsaidia wananchi wa kawaida.

Aidha, Nipashe ilimtafuta Ofisa Habari wa Nida, Thomas Willium na alipoulizwa juu ya uandikishaji, upatikanaji wa vitambulisho vya taifa na idadi ya waliopatiwa vitambulisho, alisema yuko kwenye maonyesho ya Sabasaba hawezi kuzungumza.

## Utata kutekwa kwa msaidizi wa Membe



Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Bernard Membe.

INATOKA UK. 4

Salaam na watu wenye silaha akiwa na mke wake, Veronica Kundya, Jumanne iliyopita alipatikana Mombasa nchini Kenya. Kamanda Mambosasa alisema kuna shaka fulani katika tukio hilo la Allan na kueleza kuwa watu wanataka ujiko.

"Kama kweli alitekwa tunaendelea na upelelezi, lakini hizo ni kasoro ambazo zinatia shaka kwa mtu anayesikiliza," alisema.

Jumanne, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Musa Taibu, aliliambia Nipashe kuwa Allan alikwenda polisi siku moja usiku kuwaeleza kuwa alikuwa ametekwa na watu wasiojulikana na kwamba wamemuachia huru.

"Allan aliyetekwa amepatikana, alikuja mwenyewe polisi jana (Jumatatu) usiku na akasema kuwa alitekwa na watu ambao mpaka wakati huo hajawafahamu kwa sababu wakati wakimchukua walimfunga kitambaa usoni na hata huko alipopelekwa hakujui," alisema.

Jumapili, kulizagaa taarifa mitandaoni ikidai Allan alitekwa na watu wasiojulikana maeneo ya Mbezi Jogoo, jijini Dar es Salaam nje ya nyumba ya rafiki yake aliyejitambulisha kwa jina moja la Magreth ambaye alisimulia namna alivyotekwa Allan.

# Ufaulu kidato cha sita 2019 wapanda

INATOKA UK. 2

Dar es Salaam), Mery Samwel (Weruweru, Kilimanjaro), Glory Danny Kadonga (Weruweru, Kilimanjaro), Merciana Msechu (Mpanda Girls Katavi), Getruda Didoris Ndongo (St. Christina Girls, Tanga) na Othmani Magadura Willian (Umbwe, Kilimanjaro).

**WANAFUNZI BORA MASOMO YA BIASHARA**

Waliotangazwa kufanya vizuri katika masomo ya Biashara ni Noreen M. Lyimo (Baobab, Pwani), Aston Stevin Ngaeje (Kibaha, Pwani), Doreen A. Lipamba (Benjamin Willium Mkapa, Dar es Salaam), Gift Mwakikusi (Tusiime, Dar es Salaam) na Emmanuel P. Chila (Alpha, Dar es Salaam). Wengine ni Mery D. Samwel (Weruwetu, Kilimanjaro), Glory Danny Kandonga (Weruweru, Kilimanjaro), Merciana A. Msechu (Mpanda Girls, Katavi), Getruda Didoris Ndongo (St. Christina Girls, Tanga) na Athumani Magadura Willium (Umbwe, Kilimanjaro).

**WAVULANA 10 BORA BIASHARA**

Walioshika 10 bora kwa upande wa wavulana somo la Biashara ni Aston Stevin Ngaeje (Kibaha Pwani), Gift Mwakikusi (Tusiime, Dar es Salaam), Emmanuel P. Chila (Alpha, Dar es Salaam), Athumani Magadura Willium (Umbwe, Kilimanjaro) na Stephano Y. Dismas (Kibaha Pwani).

Wengine ni Robert John Tano (Scolastica, Kilimanjaro), Shabani H. Shabani (Kibaha, Pwani), Dotee A. Zuberi (Galanos, Tanga), Ernest P. Game (Kibaha, Pwani) na Deogratias Ladislaus Msilanga (Kibaha, Pwani).

**10 BORA WASICHANA BIASHARA**

Wasichana waliong'ara kwenye somo la Biashara ni Noreen Lyimo (Baobab, Pwani), Doreen Lipamnila (Benjamin William Mkapa, Dar es Salaam), Mery Samwel (Weruweru, Kilimanjaro), Glory Danny Kadonga (Weruweru, Kilimanjaro) na Merciana Msechu (Mpanda Girls Katavi).

Wengine ni Getruda Didoris Ndongo (St. Christina Girls, Tanga), Irene Ishael Bakaeli (Ngaza, Mwanza), Rahel Kyokola (St. Mary Goreti, Kilimanjaro), Salma Shekimweri (Kibasila, Dar es Salaam) na

Grace Hayrod Ng'ondya (Weruweru, Kilimanjaro).

Jumla ya wanafunzi waliosajiliwa kufanya mitihani hiyo ya kidato cha sita ni 91,298.

## Shahidi adai kubaini kuhamishwa fedha kwenda akaunti ya Aveva

INATOKA UK. 5

Alidai kuwa maombi hayo ya klabu ya Simba aliyelipwa ni Aveva.

Hata hivyo, kwa mujibu wa kikao cha Kamati ya Utendaji cha Machi 14, 2016 cha klabu ya Simba kilielekeza fedha zitumike katika ujenzi Bunju, kwa ajili ya kumlipa Zakaria Hans Poppe alizoikopesha klabu hiyo.

Aidha, kikao hicho kilielekeza ifunguliwe akaunti maalumu itakayohusika na ujenzi wa Bunju.

"Uchunguzi wangu ulibaini baada ya kikao hicho akaunti maalumu haikufunguliwa na Machi 15, 2016 fedha zote zilitolewa katika akaunti ya klabu," alidai shahidi Mukilanya.

Katika kesi ya msingi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shadrack Kimaro, alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 Aveva na Kaburu walikula njama ya kutenda kosa la matumizi mabaya ya ofisi.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe tofauti kati ya Machi 10 na 16, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva na Kaburu walifanya matumizi mabaya ya madaraka kwa kuandaa hati ya kuhamisha Dola 300,000 kutoka akaunti ya Simba benki ya CRDB tawi la Azikiwe kwenda akaunti binafsi ya Aveva iliyoko benki ya Barclays tawi la Uhio.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa shtaka la tatu, Machi 15, 2016 Aveva na Kaburu, wote kwa pamoja walighushi fomu ya kuhamisha fedha ya tarehe hiyo wakionyesha kwamba Klabu ya Simba inalipa deni la Dola 300,000 kwa Rais wake Aveva.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa Machi 15, 2016 katika benki ya CRDB tawi la Azikiwe, Ilala, jijini Dar es Salaam, Aveva aliwasilisha fomu ya kuhamisha fedha zilizoghushiwa ya terehe hiyo akionyesha kwamba Simba imeomba kuhamisha Dola 300,000 huku akijua si kweli.

Katika shtaka la tano, ilidaiwa kuwa kati ya Machi 10, 2016 jijini Dar es Salaam,

Aveva alijilipa na kutakatisha Dola za Marekani 187,817 kutoka benki ya Barclays tawi la Uhio, huku akijua zimetokana na kughushi.

Kimaro alidai katika shtaka la sita, kati ya Machi 10 na 16, 2016 Kaburu alitakatisha fedha baada ya mshtakiwa huyo wa pili kumsaidia Aveva kupata Dola 187,817.

Katika shtaka la saba, kati ya Machi 10 na Mei 30, 2016, jijini Dar es Salaam, Aveva, Kaburu na Poppe walighushi hati ya malipo wakidai wamenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua si kweli.

Ilidaiwa katika shtaka la nane kuwa kati ya Machi 10 na Mei 30, 2016 kwa makusudi alionyesha nyaraka za kughushi kwa Levison Kasulwa akionyesha kuwa klabu hiyo imenunua nyasi bandia kutoka Kampuni ya Nina Guangzhou Trading Limited huku akijua si kweli.

Katika shtaka la tisa, kati ya Machi 10 na Septemba 30, 2016 jijini Dar es Salaam, Aveva, Kaburu na Poppe, walitoa maelezo ya uongo na kuwasilisha nyaraka za kughushi wakionyesha kuwa Klabu ya Simba imenunua nyasi bandia kutoka Kampuni ya Nina Guangzhou Trading Limited zenye thamani ya Dola za Marekani 40,577 huku wakijua si kweli.

Washtakiwa walikana mashtaka yao kwa nyakati tofauti.

Poppe anayekabiliwa na mashtaka ya kughushi yuko nje kwa dhamana wakati Aveva na Kaburu wako mahabusu baada ya kukabiliwa na mashtaka ya kutakatisha fedha.

# TPSF yahimiza maadili, sheria kwa sekta binafsi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeendelea kuwahimiza wadau waliopo kwenye sekta binafsi kufuata sheria, taratibu na uzalendo ili kuepukana na vitendo vya rushwa kwa manufaa ya taifa.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte, wakati wa mkutano wa majadiliano kwa sekta binafsi kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa uliofanyika jijini hapa.

Shamte alisema serikali kwa muda mrefu imekuwa ikilalamikia kukosekana kwa maadili katika sekta binafsi, hivyo sasa ni wakati wa wadau hao kuanza kukabiliana na tatizo hilo mapema kwa ajili ya ukuaji wa maendeleo ya nchi.

Alisema upungufu katika sekta binafsi ndio sababu serikali inaamua kufanya udhibiti mkubwa ambao alidai unasababisha hasara kwenye sekta binafsi kutokana na ukosefu wa maadili ndani.

"TPSF na sekta binafsi nzima tuna jukumu la kuhamasisha uadilifu ndani ya sekta binafsi ili kuwe na kanuni za maadili ambazo zinalenga kupunguza udhibiti uliopitiliza unaofanywa na serikali," alisema na kuongeza:

"Jambo hili kwa hakika limechangia sana kwa pande mbili hizi kutokuaminiana, hivyo tujadiliane suala hili na hatua gani zichukuliwe ili kurudisha imani kwa serikali yetu na sisi wenye tuweze kunufaika."

Pia Shamte aliwataka wadau na washiriki wa mkutano huo kujadili mambo yenye tija ikiwamo mapendekezo ya namna ambavyo sekta binafsi itashiriki katika utekelezaji wa mwongozo wa marekebisho ya kanuni za udhibiti ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kufanya majadiliano yenye tija kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, ambayo alisema yameleta mafanikio makubwa ikiwamo katika sekta ndogo ya zabibu kupunguziwa tozo kwenye mchuzi wa zabibu zinazolimwa nchini.

Simbeye aliyataja mafanikio mengine kuwa ni kuanza kwa utekelezaji wa mpango kazi wa kuboresha upatikanaji wa leseni na mazingira ya biashara kwa ujumla kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2019/2020 ilioanza kutumika Julai 1, mwaka huu.



Mkulima wa alizeti katika Kijiji cha Masinono, Kata ya Bugwema, Musoma Vijijini, Peteris Olelyo, akionyesha zao lake akiwa shambani kwake juzi. Kilimo cha zao hilo kinashamiri baada ya wananchi kuhamasishwa na kugawiwa mbegu bure na Mbunge wa Jimbo hilo, Prof. Sospeter Muhongo. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Ushirika kujenga kiwanda kubangua korosho

**Na Sabato Kasika**

CHAMA Kikuu cha Ushirika la Runali, chenye makao yake makuu wilayani Nachingwea mkoa wa Lindi, kinakusudia kujenga kiwanda cha kubangulia korosho ikiwa ni njia mojawapo ya kuwa na vyanzo mbadala vya mapato.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako ndiye aliyeliambia gazeti hili jana kwa njia ya simu na kusema kiwanda hicho kitajengwa Liwale baada ya kumalizika kwa ujenzi wa maghala, katika wilaya za Ruangwa na Nachingwea.

"Kwa sasa ujenzi wa ghala kubwa la kukusanyia mazao ya wakulima unaendelea wilayani Ruangwa na kisha tutajenga ghala lingine Nachingwea, baada ya hapo utafuatiwa ujenzi wa kiwanda Liwale," alisema Mpako.

Mpako alisema hiyo ndio mikakati ya muda mrefu, ambayo chama hicho kimejiwekea kwa lengo la kujiongezea vyanzo mbadala vya mapato badala ya kutegemea ushuru kutoka kwenye mazao ya wakulima.

"Mkakati mwingine tulionao ni kuanzisha eneo la kuchapia vitabu mbalimbali vya kukusanyia mazao ya wakulima na kuanzisha duka la pembejeo na pia kuwa na wakala wa huduma za kifedha," alisema.

Alisema, chama hicho kinazidi kuwa kikubwa tangu kilipoanzishwa mwaka 2013, hivyo wameona ni vyema kiwe na mikakati ambayo itakifanya kiendelee kujiimarisha na kuhudumia wanachama wake vizuri.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema chama chake kina mpango wa kununua ardhi ekari 500 ambayo itakuwa ni kitegauchumi cha baadaye na ikiwezekana wataanzisha shamba darasa kwa ajili ya kilimo, ili wakulima wajifunze.

"Unajua huku kwetu wakulima wamezoea korosho na ufuta kuwa ndio mazao ya biashara, lakini sasa tumeamua kuongeza zao lingine la alizeti, hivyo hatuna budi kufanya kila njia ili walizoee," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kilimo cha alizeti ni muhimu kwa vile hakitegemei masoko ya nje ya nchi, hivyo wakulima wakihamasishwa kitaleta tija kwao na kwa chama hicho kinasimamia ununuzi wa mazao ya wakulima wa wilaya tatu.

"Yakiwapo mapato ya ziada tutanunua mbegu za alizeti na kuzigawa katika shule za msingi, sekondari na ofisi za serikali za vijiji ndani ya wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale kwa ajili ya mashamba darasa," alisema.

Aidha, alisema ingawa msimu wa 2018/2019 hali ya uchumi na uzalishaji wa kwenye chama hicho vilishuka kutoka tani 52,000 hadi 40,000 kwa zao la korosho, hilo haliwakatishi tamaa.

"Hiyo ni kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa na tatizo la kutopatikana pembejeo kwa wakati na wakulima kukosa utaalamu wa matumizi sahihi ya dawa na upuliziaji," alisema.

Mpako alisema, ili wakulima wapate mavuno mazuri na mengi, Runali itashirikiana na wataalamu wa kilimo wa halmashauri tatu za Ruangwa, Nachingwea na Liwale kuondoa changamoto hizo zisijirudie msimu ujao.

# Tahadhari yatolewa dhidi ya vipodozi

**Na Faustine Feliciane**

WATANZANIA wameshauriwa kuachana na matumizi ya vipodozi vinavyotengeneza kwa kutumia kemikali na badala yake watumie vipodozi vinavyotengenezwa kwa matunda na miti asilia ili kutunza ngozi zao.

Ushauri hu umetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oriflame kwa nchini za Afrika Mashariki, Piyush Chandra, katika hafla ya uzinduzi wa bidhaa mpya ya Novage kutoka kampuni hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Piyush, alisema watu wengi wanapata madhara ya matumizi ya vipodozi vilivyotengenezwa kwa kemikali ambapo husababisha ngozi zao kupata madhara.

"Ni vyema kwa Watanzania kupunguza au kuacha kabisa matumizi ya bidhaa hizi zenye kemikali na badala yake sasa wageukie matumizi ya vipodozi au mafuta ambayo yatengenezwa kwa kutumia mimea na matunda asilia," alisema Piyush.

Alisema kampuni yao imefanya utafiti na kubuni bidhaa ambazo zinatumia matunda ya asili kama machungwa, maembe na malimao katika kutengeneza vipodozi vya mafuta ya aina mbalimbali.

"Bidhaa zetu zinawalenga watu wenye rika mbalimbali, tunaamini matumizi ya mimea na matunda asilia kwenye mafuta na vipodozi ni njia moja wapo ya kutunza ngozi za watu," alisema Mkurugenzi wa kampuni hiyo ya Sweden.

Kwa upande wake, Meneja wa kampuni hiyo kwa upande wa Tanzania, Fortunata Nkya, alisema bidhaa hizo mpya tayari zimeingia sokoni na ni baada ya kuboreshwa zaidi.

"Niwaombe Watanzania wenzangu, tuthamini ngozi zetu, tutumie bidhaa ambazo ni rafiki na zenye afya kwa ngozi zetu," alisema Fortunata.

Uzinduzi huo wa bidhaa mpya ya Oriflame ulienda sambamba na utoaji wa zawadi kwa baadhi ya wanachama wa kampuni hiyo hapa nchini.

# Waziri aonywa bidhaa za nje soko la Tanzania

NAIBU Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, amesema lipo tishio la Watanzania kuendelea kuwa walaji wa bidhaa zinazozalishwa kutoka nje ya nchi kutokana na wazalishaji wa ndani kushindwa kupata teknolojia zenye kutatua changamoto za vyakula vya asili ya Mtanzania.

Amesema utafiti na bunifu nyingi zinazogunduliwa nchini zimebaki kuwekwa katika makabati na kuonyeshwa kwenye maonyesho pekee, hivyo kuwakatisha tamaa wabunifu chipukizi.

Alisema hayo katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa (DITF) yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam katika Siku Maalum ya Sayansi, Teknolojia na Bunifu kwa biashara endelevu.

Alisema kutokana na hali hiyo, wabunifu chipukizi wanaona hakuna manufaa katika suala la ubunifu kwa kuwa kazi hizo zimebakia makabatini na katika maonyesho.

"Bunifu nyingi zimekuwa hazitatui changamoto zilizopo katika makabila na asili yetu kama Watanzania, na kama hali ndiyo hii naona kuna hatari ya kuendelea kuwa walaji wa bidhaa zinazozalishwa katika nchi nyingine," alisema Ole Nasha.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Amos Nungu, alitoa wito kwa halmashauri nchini kutekeleza agizo la kujenga kumbi za ubunifu katika maeneo yao, ili kuimarisha upatikanaji wa maarifa na ujuzi kwa vijana. Alisema katika maonyesho hayo, COSTECH imepeleka bunifu 15 ili kuionyesha jamii uwezo walionao Watanzania katika ubunifu.



Ofisa Masoko wa Kampuni ya Gf Trucks & Equipment, George Hahn (kulia), akitoa maelezo kuhusu ubora wa mashine za kutengenezea barabara kwa wateja waliotembelea banda lao, katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea kwenye Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# VETA: Sabasaba imewaachia Watanzania funzo viwanda

MAMLAKA ya Ufundi Stadi (VETA) imesema Maonyesho 43 ya Kimataifa Dar es Salaam (DTIF) yameacha funzo kwa Watanzania kuchukua hatua ya kuchangamkia fursa ya kuanzisha viwanda na kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la Veta katika viwanja vya Sabasaba, Ofisa Habari wa Veta, David Edward, alisema maonyesho hayo yameondoa visingizio kwa baadhi ya wenye mtazamo wa kushindwa kuanzisha viwanda kwa kuwa yameonyesha wazi kwamba Watanzania wamejipanga kuanzisha viwanda.

"Mbali na sisi Veta kuwa na vifaa vinavyojitosheleza kwa viwanda, lakini tumezunguka katika mabanda hususani ya washiriki kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kujifunza teknolojia mpya, kiukweli mambo ni mazuri, vifaa vyote ambavyo vinahitajika kwa viwanda vimesheneni, ambao watashindwa kuanzisha viwanda katika kipindi hiki basi hakuna kipindi kingine watakachoweza," alisema Edward na kuongeza:

"Kwa mfano ukija hapa kwetu Veta, sisi tuna machine za aina zote kwa ajili ya viwandani na tumetumia maonyesho haya kujifunza teknolojia mpya ili tuzidi kupanua wigo. Tofauti na maonyesho yaliyopita kadri miaka inavyokwenda, yanazidi kuboreka zaidi na mwaka huu yameendana kabisa na mambo ya viwanda, watu wameimprove kuboresha zaidi bidhaa zao na fursa zimeongezeka."

Edward alisema mbali na mashine, pia Watanzania kupitia maonyesho hayo wameonyesha kwamba pia wamejipanga na upande wa malighafi.

"Sisi Veta katika kuunga mkono serikali ya awamu ya tano katika ujenzi wa uchumi tumejipanga vya kutosha na ndiyo maana tunajenga vyuo Tanzania nzima, tunataka asiwepo kijana yeyote anayebaki mtaani bila kazi ya kufanya, tunataka tuwapatie ujuzi ili wachangamkie fursa hii kwa sababu tunaamini kwamba ndiyo wenye nguvu kubwa," alisema Edward.

# Njia ya kisasa upasuaji wa ubongo yaja

NAIBU Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amesema serikali ina mpango wa kuanza kufanya upasuaji wa ubongo nchini kwa kutumia matundu ya ubongo ili kupunguza athari za kiharusi.

Ndugulile aliyasema hayo jana, baada ya kutembelea mabanda yaliyo chini ya wizara hiyo, katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa (DITF) yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba.

Alisema Taasisi ya Mifupa ya MOI inafanya operesheni hizo na wapo wataalamu waliokwenda China kwa ajili ya kuongeza ujuzi zaidi na wanatarajiwa kurudi hivi karibuni.

Alisema operesheni hizo zitakuwa za tundu dogo, ambapo watakuwa wakiziba damu katika mishipa na kupunguza athari za kiharusi.

Pia alisema tayari serikali imeiagiza Muhimbili kufanya utafiti kwa magonjwa yanayosambazwa na mbu kutokana na tabia za mdudu huyo kubadilika badilika kitabia.

"Kuna mbu anaitwa Aedes anaeneza ugonjwa wa dengue, mwingine Anopheles akisambaza malaria na yule wa matende na mabusha, lakini mbu hao hubadilika, mbu ambao walikuwa wakiuma mchana wamebadilika na kuuma usiku na vivyo hivyo kwa wale waliokuwa wakiuma usiku wamebadilika wanauma mchana," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema mabadiliko hayo ya mbu yanatakiwa kufanyiwa utafiti ili kurahisisha kubaini namna wanavyoeneza magonjwa na namna ya kuyatibu na kwamba hata mbu waliokuwa wakikaa ndani kwa sasa wamehamia nje na walifikiriwa kwamba wanauma ndani tu kwa sasa wamehamia nje.

"Nafikiri kuna mbu wa ndani tuliokuwa tukiwakinga kwa chandarua, lakini ikabainika kwa sasa wanauma nje hivyo jitihada za kuhamasisha matumizi ya chandarua yakawa hayana tija, mbu wengine waliokuwa wakiruka juujuu sasa wanaruka chinichini," alisema Dk. Ndugulile.

Aliongeza: "Kwa hiyo tumewaagiza watafiti hao wafanye utafiti kuangalia tabia hizo pamoja na dawa zinazoweza kuua mbu, hata Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa yanayosambazwa Binadamu (NIMR) tumeshawaambia katika kutekeleza suala hili."

HABARI ZOTE NA ELIZBETH ZAYA

# Majeruhi wa ajali iliyoua wanahabari Azam wanena

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MMOJA wa majeruhi ya ajali iliyoua na kujeruhi wafanyakazi wa Azam Media, Mohamed Mainde, amesema kuwa ajali hiyo ni moja ya mitihani ya maisha ambayo Mungu humpa kila binadamu.

Ajali hiyo ilitokea mkoani Singida, wakati wakielekea Chato, mkoani Geita Jumatatu.

Mainde aliyasema hayo jana akiwa katika chumba cha wagonjwa mahututi

(ICU), baada ya Naibu Waziri, Wizara ya Viwanda na Biashara, Stella Manyanya, alipokwenda kuwapa pole, majeruhi wawili kati ya watatu waliolazwa Hospitali ya Arusha Lutheran Medical Centre (ALMC) jijini hapa.

Mainde alimshukuru Manyanya kwenda kuwajulia hali na kusisitiza ajali ile ni mtihani ambao mwenyezi Mungu humpa kila binadamu kwa wakati wake na muda husika.

"Nashukuru kwa kuja kutuona huu ndio moyo wa upendo uliyotuonyesha, tumepata mtihani na leo tupo hapa na tunawashukuru madaktari kwa kutuhudumia na leo hii najisikia nafuu," alisema.

Majeruhi mwingine, Artus Massawe, alishukuru kujuliwa hali na Naibu Waziri huyo, huku akisema anajiskia nafuu baada ya kufanyiwa upasuaji wa mdomo na miguu.

"Nashukuru kwa hili na naendelea vema nimetoka salama katika chumba cha upasuaji nashukuru sana, Mungu ni wa pekee," alisema.

Naye Manyanya alisema tukio hilo la ajali liliwashtuka sana sababu waliokufa na majeruhi hao ni watu waliojituma katika kufanya kazi. Manyanya alisema kujitoa kwao katika kazi kuliwafanya watambulike maeneo mbalimbali na anamshukuru Mungu kuwaona wanajitambua na kuongea.

"Nawapa pole sana na nimewapa mkono wa pole ambao utawasaidia kugharamia vitu vidogo vidogo, mkiwa hapa hospitalini... nawashukuru sana madaktari kwa kutoa huduma kwa wagonjwa hawa na wengine hakika Mungu ni mwema," alisema.

Mmoja kati ya madaktari aliyewafanyia upasuaji, Dk. Peter Makanza, alisema Mainde amefanyiwa upasuaji tatu kati ya tano, katika maeneo ya miguu na jana wameanza kuwafanyia mazoezi madogo madogo, wakati akisubiri wiki mbili zijazo kufanyiwa upasuaji mbili zilizosalia.

Alisema Massawe alifanyiwa upasuaji miguuni pamoja na mdomo wake, ambapo mtaalamu wa kinywa na meno pia ataanza naye mazoezi ya kinywa, lakini anaendelea vizuri na anaongea kwa sasa.

# Japan yatoa mil. 196.2/- kujenga madarasa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

UBALOZI wa Japan nchini, umetoa Sh. milioni 196.2, kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa madarasa, katika Shule ya Sekondari ya Sokoni ll, Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, wilayani Arumeru.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema jana kuwa ubalozi huo, umetoa fedha hizo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa ili kupunguza uhaba wa madarasa shuleni hapo.

Mahera alisema shule hiyo ni miongoni mwa shule za sekondari katika Halmashauri ya Arusha, ambayo imepata neema ya pekee ya kujengewa vyumba vinne vya madarasa na vyoo kwa ufadhili wa ubalozi huo.

Alisema ubalozi wa Japani umetoa fedha hizo ili kukamilisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, vyoo vya wanafunzi na samani za madarasa hayo, hadi ujenzi huo utakapokamilika.

Aidha, alisema kiasi hicho cha fedha watatumia kujenga msingi wa jengo la ghorofa la sakafu tatu, kukamilisha vyumba vinne vya madarasa na kuweka sakafu.

"Kutokana na changamoto ya uhaba wa ardhi, jengo hili litakuwa la ghorofa lenye vyumba 12 na kiasi hiki cha fedha kitatumika kujenga msingi wa ghorofa, kukamilisha vyumba vinne vya madarasa na vyoo vya wanafunzi pamoja na kuweka samani madarasani," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Sokon II, Mwamvita Kilonzo, alisema kukamilika kwa vyumba hivyo vya madarasa, kutapunguza msongamano wa wanafunzi darasani kwa asilimia 36.

Alisema pia hali hiyo itapunguza uhaba wa vyumba vya madarasa 11 hadi kufikia vyumba saba. Kilonzo aliongeza kuwa vyumba hivyo wanavitegemea wanafunzi 189, kusomea kwa uwiano wa wanafunzi 45 kwa kila darasa moja.

Awali, shule hiyo ilikuwa na wanafunzi 1,013 kutokana na wanafunzi kuongezeka na kusababisha upungufu wa vyumba vya madarasa 11 na baada ya kukamilika vyumba vinne kutakuwa na upungufu wa vyumba saba, lakini tayari kumeshawekwa mpango mkakati wa ujenzi wa vyumba vingine vya madarasa.



Mtoto akiwa amejitwisha ndoo lukuki kichwani tayari kwenda kisimani kuchota maji, mkoani Kigoma jana. **PICHA: MAGRETH MAGOSSO**

## Wazazi Arusha yapata mwenyekiti mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUTANO Mkuu Maalumu wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, umemchagua Hezron Mbise kuwa mwenyekiti mpya wa jumuiya hiyo.

Mbise alibuka mshindi katika uchaguzi huo baada ya kupata kura 289 na kuwashinda wagombea wenzake wawili.

Akitangaza matokeo hayo juzi jijini hapa, msimamizi mkuu wa uchaguzi huo, Deogratius Ruta, ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, alisema kura zilizopigwa zilikuwa 535.

Ruta alisema Mbise alipata kura 289, Navoi Mollel

kura 181 na Fadhili Maganya kura 44 na hakuna kura iliyoharibika.

Akitoa nasaha zake, aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Dk. John Pallangyo, aliyechaguliwa kuongoza jumuiya hiyo kipindi cha mwaka mmoja na miezi minane, kabla ya kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Arumeru

Mashariki, alisema alipoondoka katika nafasi yake aliacha jumuiya hiyo ikiwa moja.

Dk.Pallangyo alisema jumuiya pia haikuwa na makundi wala mpasuko, hivyo anategemea mrithi wake ataendeleza mshikamano huo na kumtaka ahakikishe hazalishi makundi.

Alisema kuwa sifa ya kiongozi ni pamoja na kusikiliza kwa kuwa unapokuwa kiongozi, watu wote ni wako hivyo akamtaka atumie nguvu zake kujenga jumuiya hiyo.

Pallangyo alisema alipokuwa kiongozi katika jumuiya hiyo, alijitolea samani za ofisi, hivyo mrithi wake asibaki nyuma katika kuiwezesha jumuiya kadri anavyoweza.

Alisema kwa sasa anaelekeza nguvu zake jimboni ambako kuna changamoto nyingi, zikiwamo za miundombinu kwa kutambua kuwa jimbo hilo lilikuwa upinzani na miundombinu yake ni mibovu.

Waliokuwa wagombea, Maganya na Mollel, waliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa jumuiya hiyo.

# DC azuia laki 5 za Mfuko wa Jimbo

**Na Godfrey Mushi,** HAI

FEDHA za Mfuko wa Jimbo kiasi cha Sh. milioni 41 zimezua utata baada ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kuzuia Sh. 500,000 zinazodaiwa kupangwa kugawanywa kwa kila kijiji.

Ole Sabaya alizuia fedha hizo na kuelekeza zitumike katika utekelezaji wa mradi mkubwa unatakaowanufaisha wananchi wote wa Hai, akidai kwamba Mbunge wa jimbo hilo, Freeman Mbowe, mwaka jana hakugawa fedha hizo kama sheria ya mfuko wa jimbo inavyotaka.

Alikuwa akizungumza jana na wananchi wa Roo Sinde, Kata ya Romu, wilayani hapa.

"Fedha hizo zilikuja mwaka jana (2018), shilingi milioni 41.52 kwa mbunge mliomchagua ninyi (Mbowe), lakini sheria inasema katika kipengele namba 15 cha Sheria ya Fedha za Mfuko wa Jimbo, kifungu kidogo cha kwanza kimeweka ukomo kwamba kama utavuka mwezi Desemba kila mwaka bila fedha kutumika ni lazima itafutwe idhini ya waziri wa wizara husika.

"Mwaka jana umepita wote hajaja kugawa fedha hizi, barua hii hapa (akionyesha wananchi), tumemwandikia hajaja, halafu anapeleka Sh. 500,000 kila kijiji, nimeshatoa maelekezo kwamba fedha hizo hazitakwenda kijiji chochote," alisema na kuongeza:

"Tutatafuta mradi mkubwa utakaowasaidia wananchi wote, naelekeza hakuna kugawanya fedha iliyotolewa na serikali hii ya Rais John Magufuli kwa ajili ya kujipatia umaarufu, fedha hizo zitakwenda kwenye mradi mkubwa utakaoipatia heshima wilaya hii."

Vile vile, alieleza kuwa hakuna mjadala katika jambo hilo na akaunti zilizoandaliwa kwa ajili ya kulipa kupitia watendaji wa vijiji, amefuta mpango huo.

Pia, Ole Sabaya ameagiza fedha hizo kupelekwa kwenye mradi utakaowasaidia watu wengi wakiwamo kinamama.

**AAGIZA KATIBU WAKE KUKAMATWA**

"Nimeshatoa maelekezo kwako OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), kuanzia sasa na ikifika leo (jana) jioni mkamateni (Katibu wa Mbunge Jimbo la Hai) mwekeni ndani atoe maelezo, fedha za umma msigawe, msifanye kama sandakarawe jamani," alisema.

Alipotafutwa kwa njia ya simu kuzungumzia uamuzi huo, Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, alisema inawezekana ama Mkuu huyo wa Wilaya, hajui sheria au anafanya makusudi.

"Lazima Sabaya ajue kwamba fedha za mfuko wa jimbo ziko kisheria na mbunge huziomba kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa jimbo husika. Yeye (Sabaya) siyo mjumbe wa hiyo kamati, lakini kama haitoshi asitafute kiki, kwa kuonyesha hajui sheria. Tunamshauri akasome upya sheria iliyoanzisha mfuko wa jimbo," alisema Lema.

Alipoulizwa kama ni kweli Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Hai, Irene Lema, alikamatwa kwa amri ya Mkuu wa Wilaya, Basil alikiri katibu huyo kukamatwa na kushikiliwa kwa muda na kuachiwa.



Wahudumu wa afya katika Kituo cha Afya Buzuruga, jijini Mwanza, wakitoa huduma ya kliniki ya watoto kwa watu waliohudhuria kituoni hapo kwa ajili ya kupata huduma hiyo. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# Mwalimu Mkuu kizimbani tuhuma za kubaka

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MWALIMU Mkuu Msaidizi wa Shule ya Sekondari ya Sawe iliyopo Kata ya Masama Mashariki, Solomon Sirikwa (36), amepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Hai, akikabiliwa na tuhuma za kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wake wa kidato cha nne.

Sirikwa anatuhumiwa kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 17 na baadaye kutoroka na kukimbilia kusikojulikana kwa miezi kadhaa, kabla ya kukamatwa juzi.

Mwalimu huyo alifikishwa katika mahakama hiyo jana na kusomewa makosa hayo mbele ya Hakimu Mkazi, Devotha Msofe.

Katika hati ya mashtaka iliyosomwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lobulu Mbise, ilidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda makosa hayo katika Kijiji cha Sawe, Januari 29, mwaka huu, huku akijua kufanya hivyo ni kosa la jinai.

Kwa mujibu wa hati hiyo, Sirikwa anashtakiwa kwa kutenda kosa la kwanza la ubakaji, kinyume na kifungu cha 130 (1) na (2), na kifungu 131 cha Kanuni ya Adhabu, Sura 16 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Wakati kosa la pili, Sirikwa anashtakiwa kwa kutenda kosa la kumpa ujauzito mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa), kinyume na Sheria ya Elimu, Kifungu cha 60 (A), (2) na (3) kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Baada ya mshtakiwa kusomewa mashtaka hayo, alikana kutenda makosa yote na hakimu Msofe ambaye anasikiliza kesi hiyo, aliahirisha hadi Julai 23, mwaka huu, itakapotajwa tena.

Upelelezi wa shauri hilo kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka wa Serikali, bado haujakamilika.

Hakimu Msofe alisema dhamana ya mshtakiwa huyo imezuiwa kwa sababu ya kutafutwa muda mrefu, hivyo atalazimika kukaa siku 14 mahabusu ya Gereza Kuu la Karanga, lililopo Moshi Mjini.

## Ujuzi, ubunifu kilimo kuinua mnyororo wa thamani

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MRADI wa mkulima mbunifu unaotoa elimu ya kilimo na ufugaji nchini, umeshauri serikali na wadau wa sekta hiyo kufikiria upya kuwekeza zaidi kwenye ujuzi na ubunifu katika mnyororo wote wa thamani kama inataka kujitosheleza kwa malighafi za viwandani.

Akizungumzia umuhimu wa uwekezaji huo kwa Wilaya ya Siha, Ofisa Mwandamizi wa mradi huo na Mhariri Mtendaji wa Jarida la Mkulima Mbunifu, Ayub Nnko, alisema bado wakulima wa Tanzania hawajajikita sawa sawa kwenye maeneo hayo, hali ambayo inachangia kukosa fursa za masoko ya kimataifa.

"Wakulima sasa ni vyema wakate bima ya mazao kwa ajili ya ulinzi wa athari za mabadiliko ya tabia nchi na serikali iwekeze katika tafiti ili kupata taarifa zinazoshawishi vijana kutumia fursa za kilimo.

"Pia ili kufikia lengo la kuifanya Tanzania kuwa ya uchumi wa viwanda kama ilivyo sera ya serikali kwa sasa, tunaishauri kurejesha vyuo vya shamba darasa katika kila kijiji kote nchini, lakini

taasisi za kifedha nazo zibanwe kuongeza mikopo kutoka asilimia nane hadi angalau kufikia asilimia 25 kwenye sekta ya kilimo."

Vile vile, alipendekeza sera ijayo iweke masharti ya mkulima kunufaika kwa asilimia 50 ya thamani ya mazao yake sokoni.

Alisema kwa sasa yako mabadiliko ya kimtazamo katika sekta ya kilimo ambayo kama serikali itayatilia maanani hakika ni mtaji mkubwa zaidi ya rasilimali fedha.

"Aidha, ukichilia mbali ushauri huo tunaoutoa kwa serikali, wakulima wenyewe kwa upande wao tunawahimiza kufuatilia taarifa za masoko katika kuwekeza kwenye zao husika," alisema Nnko.

Alisisitiza kwamba kwa kuwa kilimo hakihitaji usaili, ila utayari na maandalizi ya kunufaika na fursa lukuki za mahitaji ya nchi, kuna kila sababu mwaka ujao wa fedha 2020/21, serikali ikaweka kipaumbele cha kwanza katika sekta ya kilimo kwa vile ndiyo inaajiri wananchi wengi zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa uendeshaji wa kampuni ya usambazaji wa pembejeo za kilimo ya Amka Feader Ltd, Goodluck Makupa, ameishukuru serikali kwa kupunguza vikwazo na tozo 54 katika mnyororo wa thamani, akidai kuwa uamuzi huo utaongeza tija katika uzalishaji wa kilimo.



Bandari Dar kimataifa zaidi

Ukurasa 19


# BUFE

Ijumaa Julai 12, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




UCHUMI

## Bezos alivyoibuka tajiri zaidi duniani

Ukurasa 14




DODOMA MPYA

## RC, Katibu Tawala walivyosimama kuanika fursa kibao za uwekezaji

Ukurasa 16


UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

**Na Sabato Kasika**

RUNALI

# Ushirika unaopania kua




jengo jipya la ofisi ya Runali. **PICHA: SABATO KASIKA.**

WAKATI vyama vingi vya ushirika nchini, vinaanguka na kusambaratika vipo vingine vinavyojitahidi kujiimarisha kimapato, kuongeza wanachama, kiuwekezaji na kubadili sura ya maisha ya wanachama wake.

Kimojawapo ni Chama Kikuu cha Ushirika kinachoundwa na wilaya tatu za Ruangwa, Nachingwe na Liwale mkoani Lindi (Runali), ambacho kimeanza kuwekeza kwenye majengo kikianza na kujijengea ofisi kwa gharama ya Sh. milioni 139.

Ofisi hiyo imejengwa makao makuu ya Runali yaliyopo mjini Nachingwea na kukifanya chama hicho kuondokana na utaratibu wa kufanya shughuli zake kwa kutumia ofisi za kupanga.

Mwenyekiti wa chama hicho Hassan Mpako, anasema Runali ilianzishwa mwaka 2013 imeshapata usajili wa kuwa chama kikuu cha ushirika wenye namba 5597, kutoka Ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania.

Anasema baadhi ya vyama vya ushirika kutoka wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale vilijitoa katika Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Lindi (Ilulu) vikiwa 55 lakini sasa vimefikia 104.

Mpako anasema sasa wanachama wa Runali wamekuwa wakipata huduma kupitia ofisi hiyo iliyokamilika tangu mwaka jana, na kwamba chama kinaendelea na mikakati mingine ya kuboresha shughuli zake.

"Mbali na ofisi, tumejenga kituo cha maandalio ya malipo ya wakulima na tunaendelea na ujenzi wa ghala dogo la kuhifadhia pembejeo na magunia, ambavyo gharama yake ni Sh. milioni 280," anasema Mpako.

Anasema Runali pia inajenga ghala kuu la kuhifadhia mazao ya wakulima wilayani Ruangwa, litakalokuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za korosho kwa wakati mmoja, na hadi kukamilika litagharimu Sh. bilioni moja.

**RAI YA MRAJISI**

Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Tito Haule akizungumzia hatua hiyo ya Runali kujenga ofisi yake, anasema inaonyesha chama hicho kimedhamiria kufanya kazi za ushirika.

Hata hivyo, anatoa wito kwa vyama vya ushirika nchini kuanzisha miradi ya kiuchumi ili viweze kupata mafanikio na kufikia maendeleo yaliyokusudiwa wakati vinaanzishwa.

Anasema vyama vya ushirika vina kila sababu ya kuanzisha miradi ya kiuchumi li viweze kutimiza dhamira ya kuanzishwa kwake, ambayo ni kujiletea maendeleo kwa faida ya wanachama wake, ambao ni wakulima.

"Vyama havina budi kufikiria njia bora ya kuwekeza ili viendelee kupiga hatua kwenda mbele badala ya kutegemea vyanzo vichache ikiwamo ushuru unaotokana na mauzo ya mazao," anasema Haule.

Mrajisi huyo anasema uanzishaji wa miradi ya uchumi ni jambo la muhimu kwa manufaa ya vyama na wanachama wake kwa ujumla, na kwamba ndio siri kubwa ya mafanikio iwapo hilo litazingatiwa.

Vyama visiishie kuanzisha miradi ya kiuchumi tu bali viangalie hatua nyingine ya kuwekeza kwa kuzingatia mnyororo wa thamani, ambapo kwenye kanda ya kusini mnyororo wa thamani upo katika zao la korosho," anasema. Anasema vyama vinaweza kuwekeza kwenye maeneo mengine ya kijamii, lakini kwenye mnyororo wa thamani kunaweza kurahisisha na kuongeza kasi ya mafanikio ya kufikia maendeleo ya vyama hivyo.

> "Mbali na ofisi, tumejenga kituo cha maandalio ya malipo ya wakulima na tunaendelea na ujenzi wa ghala dogo la kuhifadhia pembejeo na magunia, ambavyo gharama yake ni Sh. milioni 280," anasema Mpako.

Aidha, anavitaka vyama vya ushirika kufikiria namna ya kuanzisha viwanda ili viongeze thamani ya mazao ya wanachama wake kwa ajili ya kuuzwa na kununuliwa kwa bei nzuri yenye manufaa kwao.

**UZALENDO**

Haule anaendelea kutoa somo kwamba viongozi wa vyama vya ushirika wanatakiwa kuwa waadilifu na waaminifu na weledi kwa vile uadilifu na uaminifu ni nyenzo kuu ya kuu ya uwazi na uwajibikaji.

"Kwa maana hiyo viongozi wa vyama hivyo wanatakiwa kutambua kuwa uandilifu na uaminifu ni msingi mkuu wa utawala bora unaosababisha taasisi kupiga hatua kubwa ya maendeleo," anasema Haule.

Pamoja na uadilifu na uaminifu, mrajisi huyo anasema viongozi wa vyama vya ushirika ni lazima wawe na weledi, na kwamba hawawezi kuwa weledi iwapo hawajui sheria, taratibu na kanuni.

"Ninaamini hayo yakizingatiwa, kila chama cha msingi cha ushirika kitatimiza mambo ya msingi ikiwamo kutenga asilimia kumi ambayo ipo kisheria kwa ajili ya kuwapa wanachama wake elimu, mafunzo na habari," anasema mrajisi huyo.

Kiongozi huyo anasema, kwa kuzingatia hayo, vyama pia vinaweza kuwekeza kwenye maghala ya kuhifadhia mazao na kununua magari ya kusafirishia mazao yao badala ya



Kaimu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Tito Haule

# ndika historia



kukodisha.

Vilevile anaongeza kuwa vyama hivyo vinatakiwa kufanya mikutano kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 ili kuimarisha Utawala Bora katika vyama na



“Hatua ya chama kumiliki ofisi na kujenga maghala ndani ya miaka michache tangu kujiondoa Ilulu, inaonyesha viongozi wa Runali wanajua kusimamia shughuli za ushirika. Niwapongeza kwa hilo,” anasema Muwango.

kuondoa manung'uniko kwa wanachama wao.

Haule pia anasema vinatakiwa kuitisha mikutano iliyoainishwa kisheria na kutokuingia mikataba, ambayo haikupata ridhaa ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na kwa mujibu wa sheria.

**DC APONGEZA**

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango anapongeza uongozi wa Runali kwa jinsi unavyosimamia shughuli za ushirika hadi kufikia kujenga ofisi na maghala ya kuhifadhia mazao ya wakulima.

“Hatua ya chama kumiliki ofisi na kujenga maghala ndani ya miaka michache tangu kujiondoa Ilulu, inaonyesha viongozi wa Runali wanajua kusimamia shughuli za ushirika. Niwapongeza kwa hilo,” anasema Muwango.

Muwango anasema wakiendelea kufanya hivyo wataifanya Runali kuwa moja ya vyama vikuu vya ushirika vyenye uwezo mkubwa kiuchumi kwenye mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara.

“Kwa kawaida ushirika unabebwa na dhana ya umoja... ninaamini kwamba hata Runali inazingatia dhana hiyo, kwani sijawahi kueletewa malalamiko kwamba ndani ya ushirika huo kuna mgogoro,” anasema.

# Bezos alivyoibuka tajiri zaidi duniani

MIAKA 25 iliyopita Jeff Bezos, aliona kuwa hapo baadae mambo yatabadilika , maduka yatapoteza umaarufu na yatalazimika kutoa burudani ili yasifungwe.

Kutokana na wazo lake hilo alitengeneza kampuni ya Amazon, inayofanya biashara kwa njia ya mtandao iliyoanzishwa mwaka 1994, ikawa kampuni ya pili duniani yenye matrilioni ya dola kufikia Septemba 2018 ikipitwa kidogo na kampuni ya Apple.

Ni vigumu kuamini ilianza kama kampuni ya kuuza vitabu vya mtumba.Lakini sasa mmiliki wake Bezos ni mtu tajiri zaidi duniani, akiwa na mipango mikubwa katika kuibadili dunia ya biashara. Anamiliki gazeti maarufu la Washington post.

Kampuni yake ya masuala ya anga, iitwayo Blue Origin, ina malengo ya kupeleka vifaa na binaadamu mwezini ifikapo mwaka 2024.

Mwezi Septemba mwaka 2018 aliahidi kutoa dola bilioni 2 kutoka kwenye utajiri wake kuwezesha kifedha mtandao wa shule za msingi na kusaidia wasio na makazi Marekani.

Mke wake wa zamani Mackenzie Bezos aliyahidi dola bilioni 37 kwenye mradi huo.

Miaka kadhaa iliyopita , rafiki wake wa kike wa shuleni alisema kuwa alitegemea siku zote kuwa atakuwa tajiri , na kuweza kufikia ndoto za kufika kwenye anga la mbali.

Suala halikuwa kuhusu fedha. Ilikuwa kuhusu nini fedha hizo angezifanyia kwenye kuibadili kesho yake,” aliliambia gazeti la Wired.

**KUMILIKI ANGA**

Dalili za ndoto za Jeff ziliibuka miongo mingi iliyopita, mtoto wa wazazi ambao walimpata wakiwa na umri mdogo na kuachana haraka baada ya kuzaliwa, alilelewa hasa mjini Texas na Florida na mama yake Jackie, na baba yake wa kambo Mike Bezos, aliyekuja kuwa ofisa mwanadamizi wa kampuni kubwa ya Exxon aliyekimbia Cuba akiwa kijana mdogo .

Alionyesha kipaji cha uhandisi na sayansi toka akiwa na umri mdogo, akifungua kwa bisibisi kitanda chake kidogo akiwa na umri wa miaka mitatu, na katika hotuba yake ya kumaliza sekondari alizungumzia ndoto yake ya kuanzisha makoloni kwenye sayari za juu.

Kamari aliyoicheza Bezos kwa kuanzisha kampuni kwa mtaji wa Dola 100,000 ambazo zilikuwa ni zake na kusaidiwa na familia ililipa kwa haraka.

Ndani ya mwezi mmoja tangu kuzinduliwa kwa Amazon mwaka 1995, tayari ilikuwa imesafirisha kazi za wateja wa majimbo 50 ya Marekani na katika nchi mbalimbali 45 kwa mujibu wa kitabu cha maisha ya bilionea huyo.

Miaka mitano ya kwanza ya Amazon, wateja waliongezeka kutoka 180,000 kufika milioni 17. Mauzo yakapanda kutoka Dola 500, 000 mpaka milioni 1.6. Akawa miongoni mwa wawekezaji wenye majina makubwa kutoka kwenye wimbi la kizazi cha ‘dot com’.

Mwaka 1997 kampuni hiyo ikaingia kwenye soko la hisa na kuweza kupata kiasi cha Dola milioni 54 na kumfanya Bezos kuwa mmoja kati ya matajiri wakubwa duniani kabla ya miaka 35.

Mwaka 1999, gazeti la Time lilimtaja kuwa mfanyabiashara mdogo wa mwaka akiitwa “mfalme wa biashara ya mtandaoni.’

**BBC**



UCHUMI

DODOMA MPYA

# RC, Katibu Tawala walivyosimama kuanika fursa kibao za uwekezaji

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

KAULIMBIU ya "kuweka Dodoma mpya' ili tukuinue kiuchumi, ndio inatumika jijini hapa, kufanyia kazi fursa mbalimbali zilizotangazwa kwa wawekezaji, kila mmoja akiwa na maono kusaka panapomfaa.

Katibu Tawala wa Mkoa, Kessy Maduka, anataja sehemu ya fursa kuwa ni kilimo na mazao ya misitu, ambako kuna maeneo mbalimbali yaliyotengwa kwa wawekezaji kama moja ya nyenzo ya kuinua uchumi wa nchi kupitia viwanda vijavyo na vinavyoendelea kujengwa.

Anataja maeneo yaliyotengwa kwa wawekezaji kuchangamkia, yapo katika wilaya za Kondoa na Chemba, ambako kuna zaidi ya hekta 17,640 kwa ajili ya mashamba ya kilimo cha mkataba, huku Chamwino kuna hekta 245 za kilimo cha maembe.

Pia, kuna hekta 294 zilizotengwa kwa ajili ya ubia kwenye skimu

ya umwagiliaji ya kijiji cha Zepisa, wakati wilayani Bahi kuna miundombinu ya umwagiliajiwa kilimo cha mpunga na nafaka ambapo kuna hekta 200, katika kijiji cha Kongogo kata ya babayu hekta 500 hadi 1,000 zimetengwa.

Maduka anasema, wilayani Chemba, kunahitajika ujenzi wa bwawa la

umwagiliaji wa mazao ya bustani na viungo kama pilipili; Kata ya

Kidoka kuna hekta 600 ya kilimo cha umwagiliaji wa mpunga; hekta 300; na jogolo kuna hekta 3,000.

Anasema hizo zote ni fursa za uwekezaji zinazohitaji wawekezaji wa kuendeleza uchumi wa nchi na kulifanya jiji la Dodoma kuwa la kimataifa.

Mengine anayataja kuwa ni mizinga ya kisasa ya ufugaji nyuki, yote yakilenga kumfanya mwekezaji kupata nafasi ya kufuga na kuwauzia wakazi wanaokaa jirani na pori la Swagaswaga.

Pia, Maduka anataja eneo la uwekezaji mizinga ya kisasa na ufugaji nyuki katika uwanda wa Salanga na Isabe.

Taarifa ya Katibu Tawala, inataja fursa katika vijiji, vitongoji, kata na miji yake, ambako kuna jumla ya hekta 3,000 za kilimo cha umwagiliaji mazao ya bustani eneo la Mongoroma;

**MIUNDOMBINU, MASOKO, UTALII**

Katibu Tawala anawakabiribisha wawekezaji katika ujenzi wa miundombinu na masoko, ikiwamo ujenzi wa vituo vya mabasi katika Halmashauri za Chamwino, Mpwapwa, Bahi, Kondoa Mji na Chemba.

Anataja katika miundombinu ya masoko, wanapaswa kuwekeza katika ujenzi wa soko la mazao ya kilimo eneo la Haneti, Mpwapwa mjini, Chipogolo, Mlembule na Pawaga, Kondoa Mji, Soko la Mazao ya Kilimo na Mifugo eneo la Kingale, na Chemba mjini.

Anataja maeneo yaliyotengwa kwa ujenzi wa hoteli ni Chemba na Kongwa Mji



Baadhi ya wawekezaji wakimsikiliza Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (hayupo pichani) kwenye Kongamano la Uwekezaji Dodoma.

**UFUGAJI & UVUVI**

Maduka anasema, ranchi ya unenepeshaji mifugo, Chemba imetengwa kuhudumia mifugo katika eneo lenye hekta zaidi ya 692 katika kijiji cha Kelema na Paranga, wakati eneo la Kondoa, mwekezaji anakaribishwa kuwekeza katika unenepeshaji mifugo, kulima nyasi za malisho na kutoa huduma za mifugo.

Anatangaza kuwa wawekezaji wanakaribishwa katika ufugaji samaki na kuzalisha vifaranga vyake na kwamba eneo limetengwa kwenye vizimba vya bwawa la Dabaro na wilayani Kongwa kumetengwa hekta 19 kwa ajili ya kuingia ubia na watu binafsi.

**VIWANDA**

Maduka anaeleza serikali mkoa inawakaribisha kuwekeza katika utengenezaji wa vifungashio vya bidhaa za viwandani na mazao ya kilimo, uvuvi na misitu katika halmashauri zote za mikoa, kwani kila halmashauri imetenga eneo lake la viwanda.

Katibu Tawala anasema, kiwanda cha maziwa kimetengewa hekta 2,000 eneo la Mtumba, mwekezaji anakaribishwa katika kuchakata maziwa na kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na maziwa.

Ili kufanikisha hilo, anasema anatakiwa kuwa na vituo vya kukusanyia maziwa katika kila halmashauri; kwani Dodoma inazalisha maziwa zaidi ya lita 11,000 kwa mwaka.

Hiyo inaendana na kuwekezwa kiwanda cha ngozi, eneo la Mpunguzi kulikotengwa hekta 3,663 na Nala zimetengwa hekta 851 kwa ajili ya kiwanda cha kulainisha ngozi.

Pia mwekezaji anakaribiswa kuchakata na kuongeza thamani ya zabibu, akitengeneza bidhaa kama juisi na nyinginezo.

**RC DODOMA**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, anasema fursa zilizopo zitainua uchumi wa jiji la Dodoma na taifa kwa ujumla, kwa sababu mwekezaji ana uwezo wa kuchagua wapi pa kujielekeza kibiashara na kuboresha jiji na nchi kwa jumla.

Anasema fursa zilizoainishwa katika kongamano la uwekezaji lililomalizika hivi karibuni, ni nyenzo tosha kwa wawekezaji kusaidia kuinua uchumi wa nchi kupitia sekta ya viwanda wanavyotarajia kuwekeza kwa ajili ya kuendeleza jiji la Dodoma ambalo ni kitovu cha biashara kwa sababu lipo kati kati ya nchi.

"Hakuna sababu ya kuchelewa, wawekezaji jitokezeni kuchangamkia fursa zilizopo, miundombinu imeboreshwa uwezekano wa usafirishaji wa bidhaa pindi viwanda vitakavyokamilika hautakuwa na shida yoyote," anasema Dk. Mahenge.

Mkuu wa Mkoa anafafanua kuwa Dodoma ipo katikati ya nchi, hivyo usafirishaji wa bidhaa za biashara ndani ya nchi na nje, si tatizo na mkoa umejipanga kuboreshwaji miundombinu, ikiwamo barabara, reli na usafiri wa anga.

**WAZIRI MKUU**

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye sasa ni mkazi wa Dodoma, anasema hakuna sababu ya kuchelewa, kwa sababu jiji lina fursa nyingi zinazohitaji uwekezaji mkubwa.

.Majaliwa anataja ardhi ya Dodoma ina maeneo yaliyokwishapimwa na kutengwa kwa lengo la uwekezaji katika sekta ya viwanda vya uchakataji thamani za mazao, yanayohitaji uwekezaji.

"Jiji la Dodoma lina kila kitu. Ardhi ipo ya kutosha, maeneo yamepimwa, kwa hiyo wawekezaji jitokezeni kuwekeza ili muinue uchumi wa nchi na kuitangaza Dodoma, ambayo ni makao makuu ya nchi," anasema Majaliwa.

Anafafanua, lengo lao ni kuona kila mwekezaji anawekeza pale anahisi ana uwezo wa kuwekeza na kutoa faida kwa wakazi wa eneo, akiwaikaribisha wachangamkie fursa zilizopo.

Majaliwa anataja mazao hayo ni uchakataji karanga na vyakula vya mifugo, ili kuongeza thamani, ni fursa kwa wawekezaji kuwekeza kwa sababu maeneo yametengwa, yanayohitaji kuboreshwa na kuendelezwa, ikiwa ni nyenzo ya kuinua uchumi wa viwanda na kufungua fursa za ajira zinazoongezeka kulingana na fursa zinbavyopanuyka

**TCCIA**

Rais wa Chama cha Wafanyabishara, Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Octavian Mshiu, anaipongeza Dodoma kwa kuandaa kongamano la uwekezaji, kwa sababu limesaidia kujua fursa zilizopo.

Mshiu anasema, kongamano hilo limefungua changamoto yao ya kujua kinachotakiwa katika kuipaisha Dodoma kiuchumi, hivyo anaihakikishia serikali kuwa TCCIA iko pamoja nayo kupitia sekta ya viwanda

"TCCIA tuko pamoja na serikali kuhakikisha tunaimarisha uhusiano katika kuinua uchumi. Kongamano hili limetusaidia kujua fursa nyingi ambazo zinahitaji uwekezaji,"anafafanua Mshiu.

**WAZIRI MKUU MSTAAFU**

Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, anasema wanahitaji wawekezaji watakaofanya Dodoma kuwa bora kibiashara, kiuchumi na wakazi wake kunufaika na uwekezaji huo.

Pinda anasema, katika maeneo yaliyotengwa kwa viwanda vya uchakataji thamani ya mazao ya alizeti, zabibu na mengine, anaamini wakazi watanufaika na ajira zitakazotolewa wakati wa ujenzi wa viwanda na baada ya kukamilika, lengo la kwanza ni uchakataji bidhaa hizo.

"Karibuni wawekezaji mje uwekezaji, tunahitaji mje kutoa chachu ya maendeleo katika maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya uwekezaji," anasema Pinda.

Anasema lengo ni kuifanya Dodoma jiji la kimataifa, kupitia maendeleo yatakayofanywa na wawekezaji.

**WAKAZI DODOMA**

Mkazi wa Dodoma, Michael Sarufi, anasema kongamano la uwekezaji limewasaidia kuwafumbua macho ya kuwa nini wanatakiwa kufanya ili kujiinua kiuchumi ikiwemo kuinua mkoa wa Dodoma.

Sarufi anasema anaamini wawekezaji watakaojitokeza kuwekeza katika maeneo mbalimbali yaliyotengwa, yataifanya Dodoma jiji la kibiashara, akijivunia kuwapo fursa nyingi, hivyo ni 'kazi kwao' wakazi kujiandaa kisaikolojia kuchangamkia fursa.

"Tumefurahishwa sana na kongamano hili la uwekezaji. Limetufumbua macho kwa kiasi kikubwa,"anasema Michael.

Stella Pius anasema,wao kama wakazi wa jiji la Dodoma wanafurahishwa na waandaaji wa kongamano hilo kwa sababu limewasaidia kwa kiasi kikubwa kutangaza fursa zilizopo ambazo zinahitaji kuendelezwa kupitia wawekezaji, hivyo anawaomba wawekezaji kuchangamkia fursa za Dodoma yao

**AGIZO LA JAFFO**

Waziri wa nchi Ofisi ya Rais (Tamisemi), Suleiman Jaffo, anaagiza mikoa mingine ambayo haijafanya kongamano za uwekezaji, ifanye hivyo mara moja, kwa sababu inasaidia kujua fursa za kimkoa zilizopo katika uwekezaji.

Anasema kila mkoa unapaswa kuandaa kongamano la uwekezaji ili kuweza kubaini fursa zilizopo katika eneo husika. Jaffo anaendelea: "Naomba mikoa ambayo haijaandaa kongamano la uwekezaji ifanye hivyo, kwa sababu ni mikoa michache ambayo imeandaa."




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (katikati), akizindua Kongamano la Uwekezaji Dodoma. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

## BIASHARA KATIKA PICHA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ndege nchini (ATCL), Mhandisi Ladslaus Matindi (kushoto), akisalimiana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mawakala wa Shirika la ndege Tanzania (TASOTA), Moustafa Khataw, katika kikao cha Menejimeti ya TASOTA na Mkurugezi huyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Wachuuzi wa madafu wakiyahesabu kabla ya kuanza safari ya kusaka wateja, Mbagala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mchuuzi akinadi mapanga na majembe madogo kwa abiria walio kwenye foleni ya magari katika eneo la Tabata, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

BIASHARA

Na Reginald Taabu



Bidhaa zilizo ghalani zinalazimu kila mara kuhesabiwa. **PICHA:MTANDAO.**

# Ukifanya haya utafanikisha kuhesabu, kuhakiki mali

KUHESABU na kuhakiki mali au kwa Kiingereza stock-taking ni kazi ya kuhesabu mali za kampuni, shirika au taasisi na kulinganisha na nyaraka za kuhifadhia mali hizo zilizoko mikononi mwa mamlaka ya taasisi husika.

Kuhesabu na kuhakiki mali hufanywa kwa vipindi maalum kutokana na aina na shughuli za kampuni, shirika au taasisi husika. Mara nyingi zoezi hili hufanywa mara moja kwa mwaka, yaani, mwisho wa mwaka wa fedha.

Aidha hufanyika, mara mbili kwa mwaka yaani, kila nusu ya mwaka wa fedha au mara nne kwa mwaka , kila robo ya mwaka wa fedha, kutegemeana na asili ya kazi ya kampuni, shirika au taasisi.

Madhumuni ya kuhesabu na kuhakiki mali ni kama yafuatayo:

Mosi ni kubaini wizi au upotevu wa mali. Pia ni kutambua iwapo kuna mali zilizozidi.

Aidha ni kuwezesha kuboresha mfumo wa uagizaji mali kwa kuzingatia idadi sahihi ya mali zilizopo, pia ni kusaidia kufanya ulinganifu kati ya mali halisi na nyaraka za mali, hivyo kuboresha mifumo ya udhibiti wa utunzaji mali.

Lengo la kufanya stock taking ni kusaidia katika kutengeneza hesabu sahihi za kihasibu za mwisho wa mwaka kwa kutoa idadi sahihi ya mali zinazomilikiwa na kampuni, shirika au taasisi.

Kazi hiyo ni muhimu kwa kuwa inawezesha kubaini mali zilizochakaa ambazo hazifai tena kwa matumizi au mali zilizoharibika ambazo zinahitaji matengenezo au marekebisho.

Hatua za kufuata ili kuwa na matokeo bora katika zoezi la kuhesabu na kuhakiki mali linaweza kuwa linachosha, linatumia nguvu na muda mwingi kufanyika kama watendaji hawatajipanga vizuri.

Pia jukumu hilo kama lisipofanywa kwa uangalifu, linaweza lisitoe matokeo bora kutokana na makosa mengi ya kibinadamu yanayoweza kufanyika.

Katika utekelezaji wake kampuni, taasisi au shirika linapaswa kufuata njia sahihi katika kuendesha zoezi zima ili kuweza kupata matokeo bora na kuleta ufanisi.

**HATUA**

Ili kukamilisha kazi hiyo zifuatazo ni hatua sahihi za kufuata wakati wa kuendesha zoezi la kuhesabu na kuhakiki mali ili kupata matokeo bora:

Mosi ni kupangilia vizuri ratiba ya zoezi la kuhesabu na kuhakiki mali ili shughuli husika zisiingiliane na shughuli zingine za kiutendaji za kila siku za kampuni, shirika au taasisi. Ili kuleta ufanisi na kupunguza mwingiliano wa kimajukumu, zoezi linapaswa kufanyika kipindi ambapo kazi za kawaida si nyingi au lifanyike masaa ya ziada baada ya muda wa kazi

Suala jingine ni kusafisha na kupangilia vizuri chumba cha kuhifadhi mali kabla ya kufanya zoezi la kuhesabu na kuhakiki mali. Usafi na mpangilio mzuri wa chumba cha kuhifadhi mali hurahisisha ufanyaji kazi, huongeza ufanisi na hupunguza makosa ya kihesabu. Hali kadhalika ili kurahisisha zoezi unapaswa kuweka mfumo mzuri wa mpangilio unaoonesha sehemu bidhaa ilipo kwa kuweka alama (label) mahali bidhaa ilipo na pia idadi ya bidhaa zilizopo katika kila kifungashio

> **Kazi hiyo ni muhimu kwa kuwa inawezesha kubaini mali zilizochakaa ambazo hazifai tena kwa matumizi au mali zilizoharibika ambazo zinahitaji matengenezo au marekebisho.**

Ni vizuri kupanga na kuweka tayari vifaa vya kufanyia zoezi kabla ya muda wa kazi ya kuhesabu na kuhakiki mali. Kabla ya kuanza kwa zoezi hakikisha watendaji wote wana vifaa vyote muhimu vya kufanyia kazi kama; karatasi za kuhesabu mali (stock sheet), karatasi za kuondolea mali (stock write off sheet), kalamu, kikokotoo (calculator), kitambazo (scanner) au vifaa vingine vitakavyohitajika katika kazi hiyo muhimu.

Ili kufanikisha kazi hiyo mpatie kila mhusika malengo na majukumu yake ya kutekeleza katika zoezi la kuhesabu na kuhakiki mali. Msimamizi wa zoezi anapaswa kuwapangia watendaji wa zoezi majukumu ili kuwezesha kufanikisha zoezi kwa ufasaha na kwa wakati bila kuwapo kwa mwingiliano wa majukumu.

Mhesabu mali anatakiwa kujua anahesabu vitu vya aina gani na vinahesabiwa kwa njia gani. Hili ni muhimu kwa sababu baadhi ya vyumba vya kuhifadhia mali mara nyingi huwa na vitu tofauti tofauti ambavyo vinapimwa aidha kwa uzito, urefu au ujazo.

> **Kwa kufuata hatua zilizotajwa kazi ya kuhesabu na kuhakiki mali itafanyika kikamilifu na kutoa matokeo bora. Hatua hizi pia zitarahisisha ufanyikaji na kuongeza ufanisi wa zoezi na hivyo kupunguza ugumu usio wa lazima,**

Fungua na kuhesabu kwa umakini kila kitu bila kukisia. Mathalani, kama kuna kifungashio kilichoandikwa kuna bidhaa 10 ndani yake, thibitisha kwa kuzihesabu bidhaa husika.

Aidha, linganisha idadi za vifaa vilivyohesabiwa dhidi ya nyaraka zenye orodha na idadi ya vifaa ili kugundua tofauti, kisha rudia kuhesabu sehemu zenye tofauti ili kujiridhisha.

Kwa kufuata hatua zilizotajwa kazi ya kuhesabu na kuhakiki mali itafanyika kikamilifu na kutoa matokeo bora. Hatua hizi pia zitarahisisha ufanyikaji na kuongeza ufanisi wa zoezi na hivyo kupunguza ugumu usio wa lazima,

Ni muhimu kampuni, taasisi na mashirika kufuata sheria, kanuni na miongozo inayohusika katika kuendesha zoezi zima la kuhesabu na kuhakiki mali ili kuleta ufanisi na kupunguza makosa ya kimahesabu na hoja za ukaguzi.

***Dokta Regnald Taabu ni mtaalamu wa Ununuzi na Ugavi - Chuo Kikuu Mzumbe-Moro-***

UCHUMI



Sehemu ya ujenzi wa gati katika Bandari ya Dar es Salaam. **PICHA:MTANDAO**

# Bandari Dar kimataifa zaidi

## Vigogo usafirishaji duniani waikubali

**Na Mary Geofrey**

JITIHADA za kuiboresha bandari ya Dar es Salaam, zimeanza kuzaa matunda baada ya wafanyabiashara wakubwa wa madini na wamiliki wa meli za shehena za kimataifa kuanza kuitumia.

Katika kuhakikisha wasafirishaji wa kimataifa wanatumia bandari za Tanzania hivi karibuni, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, anakutana na wachimbaji wakubwa wa madini na wamiliki wa meli duniani kwa lengo la kuwashawishi kutumia Bandari ya Dar es Salaam na Tanga, kupitisha shehena zao.

Anasema bandari ya Dar es Salaam, imefanyiwa ukarabati mkubwa na kuwa na kina kirefu cha mita 16, kinachoweza kupokea meli zenye ukubwa wowote.

Anakutana na kampuni zaidi ya 10 za uchumbaji madini nazo ni pamoja na Bridge Shipping, Access World, Impala Terminals, Trafigula and Reload Logistics ambazo zinasafirisha madini kwenda nchi mbalimbali duniani ikiwamo China.

"Tumekutana na wachimbaji hawa wakubwa wa madini kwa lengo la kukaa pamoja kujadiliana changamoto zilizopo kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ambazo zinasababisha washindwe kupitisha shehena zao. Tunataka tuzifanyie kazi na wao waanze kupitisha mizigo yao hapa," anasema Waziri.

Anaeleza kuwa kwa kiasi kikubwa bandari hiyo imefanyiwa maboresho makubwa yakiwamo ya kuongezewa kina na sasa ni mita 16, ili meli kubwa za kimataifa ziweze kutia nanga.

### MAPENDEKEZO

Waziri Kamwelwe, anataja mambo ambayo wafanyabiashara wa madini waliomba yafanyiwe kazi na bandari hiyo kuwa ni mizigo kucheleweshwa kutoka bandarini.

Wanashauri kuwapo kwa sera ambazo zinazokuwa na uwiano na nchi nyingine wanazoshirikiana nazo hasa usawa wa mizigo.

Kamwelwe anaahidi kuwa serikali inafanyia kazi changamoto hizo na kuwaahidi kuwa itashirikiana na taasisi nyingine kufanya kazi kwa saa 24 katika bandari hiyo.

Aidha, wamekubaliana kukutana tena mwezi ujao kujadili kama wameridhishwa na maboresho yanayofanywa.

### WAFANYABIASHARA

Watendaji wa kampuni hizo, halikadhalika wanakutana Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, mkutano uliohusisha kampuni za meli Maersk, MSC, CMA na PIL ambazo kwa pamoja zimekubali kutumia Bandari ya Dar es Salaam, kwa sharti kuwa mapendekezo waliyotoa yanafanyiwa kazi.

"Tumefanya mkutano mwingine na wamiliki wa meli kubwa duniani ikiwa ni muendelezo wa mikutano yetu na wachimbaji wakubwa wa madini duniani awali, wito wetu kwa matajiri hawa ni kuwaomba watumie bandari yetu kwa sababu sasa tumeboresha huduma," anasema Waziri Kamwelwe.

Waziri huyo, anawaeleza wanahabari kuwa kwa kuthibitisha kuwa maboresho yamefanyika katika bandari hiyo, kwa mara ya kwanza wiki iliyopita meli iliyosajiliwa Panama kwa jina la Kouyou Tonnage 33126 yenye urefu wa mita 197 na upana mita 32.26, ilitia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam kushusha shehena ya mbolea, ambayo itasafirishwa kwenda nchi nyingine ikiwamo ya Zambia.

### CHANGAMOTO

Licha ya kuwapo kwa foleni ya malori yanayotoka katika bandari hiyo, Waziri Kamwelwe, anaahidi kuwa ufumbuzi wa kudumu, utapatikana wakati wowote kuanzia sasa.

Anasema Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari(TPA), inafanya kazi saa 24 lakini taasisi nyingine zinazoshirikiana nayo hazijaanza kufanya kazi kwa muda huo.

Kuanzia Septemba 2017 serikali ilipitisha sheria ya taasisi za umma, kufanya kazi saa 24, lakini Waziri huyo anasema katika bandari hiyo zipo ambazo hazijatii sheria hali inayosababisha kuchelewa kutoka kwa mizigo.

Baadhi ya taasisi hizo zinazofanya kazi na TPA ni Mamlaka ya Chakula na Dawa(TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA).

"Kumekuwapo na upotoshaji mkubwa kuwa mzani uliopo katika Bandari ya Dar es Salaam unasababisha foleni ya malori kutoka bandarini jambo ambalo si kweli kwa sababu zipo mizani mbili na zinafanya kazi bila matatizo yoyote na kwa sekundi 55 malori mawili yanapimwa jukumu linalofanyika kwa saa 24," anasema Waziri.

Anaongeza:" Kinachosababisha foleni ni changamoto zetu wenyewe watu wa TPA na TRA na wengine wanaofanya kazi na bandari, ambao wanatakiwa kufanya kazi kwa saa 24 lakini hazifanyi hivyo."

Anaitetea TPA kuwa imetii agizo na inakamilisha majukumu yake na kubakiza yale yataasisi nyingine na ndicho chanzo cha malori kulundikana.

### KUCHUKUA HATUA

Kamwelwe anaeleza kuwa ili kumaliza changamoto hiyo, ameiandikia barua Wizara wa Fedha na Mipango, ili watumishi wa wizara hiyo waweze kufanya kazi katika bandari hiyo ambayo ina ofisi za kutosha kwa ajili ya watumishi wa idara zote.

Anasema TPA ina ofisi za kutosha kutumiwa na wafanyakazi wa mamlaka zote zinazofanya kazi katika bandari hiyo, hivyo wanashughulikia suala hilo ili kuboresha ufanisi wa bandari.

### USHIRIKIANO KIMATAIFA

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Palamagamba Kabudi, katika mkutano huo, anawataka wafanyabiashara hao wakubwa duniani kupitisha mizigo yao Dar es Salaam na Tanga.

Anawaambia si kwa sababu tu zina kina kirefu, bali uhakika wa usalama wa mali zao na Amani wakati wote.

Anasema sababu za kuhudhuria mkutano huo ni kwa vile Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Afrika Mashariki na wanashirikiana katika nyanja mbalimbali za kukuza uchumi wa mataifa yao.

"Niko hapa kuwahakikishia wamiliki usalama wa meli na wafanyabiashara wanaopitisha mizigo yenu katika bandari zetu. Kwanza tumefanya jitihada kubwa za kuboresha bandari pamoja na kumaliza changamoto, jambo jingine amani na usalama uliopo katika nchi yetu," anaeleza Prof. Kabudi.

### MABORESHO

Aidha, Mkurugenzi wa TPA, Deusdadus Kakoko, anasema upanuzi wa magati matatu umekamilika katika bandari hiyo yenye kina cha mita 16. Kila moja, lina uwezo wa kupokea meli yoyote kubwa duniani.

"Tayari gati namba moja, namba saba na namba mbili yamekamilika na tayari meli zimetia nanga, tofauti na hapo awali bandari zetu zilikuwa zikitumika kupitishia mizigo kwa sababu tulikuwa na kina kifupi," anasema Mkurugenzi Kakoko.

Anasema upanuzi wa bandari hiyo umegharimu Sh. bilioni 336.7 na kazi zinazofanyika ni kuongezea uwezo gati hiyo yenye urefu wa mita 192 ili kubeba meli kubwa mbili zenye uzito wa kati ya tani 45,000 hadi 60,000 kwa wakati mmoja.

Kuhusu ujenzi wa gati ya magari au 'RoRo Berth' pamoja na yadi ya kuegesha magari, anasema utaiwezesha bandari hiyo kupokea magari 10,000 kwa siku mara nne zaidi ikilinganishwa na magari 2,500 hapo awali, na kwa mwaka itakuwa magari 200,000 kutoka magari 90,000.

"Kukamilika kwa gati hii kutaleta mapinduzi makubwa kwani tunaweza kupokea meli ya magari 3,000 hadi 5,000 na ikapakuliwa kwa siku moja tu," anasema Kakoko.

Anasema wananchi na wadau wakiwamo mawakala wa meli wanatakiwa kuwa tayari kwa sababu kuna meli 12 tu na zilishawahi kufika meli 18.

Anaongeza kuwa ujenzi wa gati hiyo, utaenda sambamba na upanuzi wa lango la bandari kwa kuongeza kina kutoka mita 10 hadi 16 ikiwa kwa sasa unafanyika usanifu na ifikapo Juni mwakani uchimbaji utaanza rasmi.

"Nia yetu ni hadi kufikia Disemba mwakani tuwe na gati kuanzia sifuri hadi namba tatu na upanuzi wa lango uwe umekamilika ili tuweze kupokea meli za kimataifa zenye kina cha mita 15 na uwezo wa kubeba hadi makasha (makontena) 6,000 kutoka meli za sasa zinazoweza kubeba makasha 2,500 tu," anasema Mhanidisi Kakoko.

BIASHARA

# “Tatizo siyo mtaji ni kutambua unacholenga”

Na Faustine Feliciane

LICHA ya kuongezeka kwa wajasiriamali wengi ambao wanafanya biashara ndogondogo na za viwango vya kati wanaolalamikia kukwama kimtaji, washauri wa biashara wanasema tatizo linalowakabili si mitaji.

Wanaeleza kuwa kinachowachanganya kushindwa kubaini na kusimamia kile wanachokikusudia kukitimiza au kukifanya, elimu hiyo inakosekana.

Hivi karibuni serikali ilianza kutoa vitambulisho kwa wajasiriamali nchini ili watambulike na kufanya biashara zao kwa uhuru zaidi.

Hata hivyo changamoto za kulalamikia mitaji midogo zinaelezwa kuwa sio kikwazo kikubwa kwa watu wanaotaka kuingia kwenye ujasiriamali.

Mwanzilishi na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Area Code Creative Minds, Nahuja Hatibu, anasema.

Anaongeza kuwa wanaotaka kuanza ujasiriamali wasitishwe na mitaji midogo waliyonayo, badala yake waanze kwanza kutafuta ufahamu ni biashara gani wanayotaka kuanza kabla ya kujitosa kwenye uwekezaji.

Nahuja ambaye kampuni yake inajihusisha na utoaji wa elimu na mafunzo ya biashara kwa kampuni kubwa na ndogo, wafanya biashara binafsi na wajasiriamali, anasema:

“Watanzania wengi wamekimbilia kwenye mitaji kuwa ndiyo kikwazo kwao katika kuanzisha na kuendeleza biashara kitu ambacho kwetu si kikwazo.”



Mjasiriamali lazima afahamu anataka nini, kuuza nyanya kama hivi au chakula. Ni muhimu kuwa na eneo moja unapojielekeza siyo kushika kila kinachokuja mbele yako. **PICHA: MTANDAO**

**CHANGAMOTO**

Nahuja anasema tatizo kubwa linalowakumba watu wengi hasa wale wanaotaka kuanzisha biashara au ambao tayari wamezianzisha, ni uelewa mdogo wa kile ambacho wanataka kukifanya au wameshaaza kukifanya.

“Watu wengi wanaanzisha biashara bila kufanya utafiti wa kile wanachotaka kukifanya na matokeo yake biashara nyingi zinaishia njiani. Wengi tumekuwa wavivu wa kujisomea, wa kutafuta maelezo ya biashara zetu,” anasema Nahuja.

“Hili ni tatizo kubwa, wengi wanaanzisha biashara kwa kuiga kwa marafiki au ndugu. Mjasiriamali kama huyu hata akiwa na mtaji na pesa nyingi bado anaweza akaishia njiani na biashara yake ikafa. Tatizo kubwa watu wengi hatupendi kutafuta maelezo ya kina au kufanya utafiti wa kutosha wa kile tunachotaka kuanzisha,” anabainisha Nahuja.

“Wapo watu hata ukimpa milioni 50 afungue biashara, kama hana uelewa wa biashara pesa hiyo yote itapotea. Lakini kuna mwingine atakuwa na 500,000 kwa mfano, akasaka maelezo ya biashara anayotaka kuanzisha na kufanya tafiti atakuta anafanikiwa na biashara yake inakua,” anasema.

SHIKA ULICHONACHO

Nahuja majasiriamali na mbobezi wa masuala ya masoko, anasema kitu kikubwa kwa mtu anayetaka kuanza ujasiriamali anapaswa kujitambua na kufahamu nini anachotaka kufanya.

Hatua nyingine ni kuanza kutafuta maelezo ya kina kuhusu biashara “anayotaka kuianzisha.

“Unaweza ukawa na Sh 1,000,000 ukadhani ni ndogo sana kuanzisha ujasiriamali. Sisi tunasema hapana, unaweza ukanza na kiasi hicho na ukapata mafanikio kama tu utafanya utafiti wa biashara unayotaka kufanya, ambao utahusisha kujua soko la bidhaa yako unayotaka kuanzisha liko wapi,” anasema.

> **“Hili ni tatizo kubwa, wengi wanaanzisha biashara kwa kuiga kwa marafiki au ndugu. Mjasiriamali kama huyu hata akiwa na mtaji na pesa nyingi bado anaweza akaishia njiani na biashara yake ikafa...**

Anafafanua kuwa kampuni yake inatoa huduma hizo za elimu na tafiti kwa wajasiriamali na kuwapa ushauri kuhusu biashara wanayotaka kuanzisha.

Nahuja anasema kampuni hiyo ni ya wajasiriamali ambapo kazi yao kubwa ni kutoa elimu ya biashara kwa Watanzania ambao wanataka kuingia kwenye ujasiriamali wa kiushindani.

Aidha, anasema kampuni hiyo pia inafanya kazi na wadau na wafanyabiashara wakubwa katika kuendeleza biashara zao.

“Mimi mwenyewe kama mwanzilishi wa kampuni hii, nilikuwa mwajiriwa, lakini nilikuwa naona namna watu wanavyopata tabu kwenye biashara, nikatamani kuanzisha kampuni itakayowafikia na kuwasaidia kutimiza malengo yao,” anasema Nahuja.

Anaongeza “Nashukuru mafanikio ninayaona kwa wale wanaokuja kwenye kampuni yetu kupata elimu na ushauri wa biashara.”

Anasema watu wasione aibu kutafuta taarifa za biashara zao kwa kuwa huo ndiyo msingi wa kuelekea kwenye mafanikio ya kile wanachotaka kukianzisha.

> **“Taifa limeendelea kwenye teknolojia .Wajasiriamali wajitahidi kuwa kwenye mitandao. Hata sisi tupo kwenye platform zote za mitandao ya kijamii na pia tuna website ambayo watu wanaweza wakawasiliana.” Anahimiza.**

Anasema :”Lengo letu ni kufikia Watanzania wengi zaidi, Area code tunataka kuona wazawa wengi zaidi wanakuwa wawekezaji, wanawekeza kwenye biashara, karibu kila mkoa Bara na Visiwani,” anasema Nahuja.

Anasema wananchi wanatakiwa kuchangamka bila kujali maana kinachokutoa ni kile unachowaza kukifanya na si kuwaza mitaji.

Lakini pia anawakumbusha watu kutafuta ushauri na ujuzi zaidi kuhusu biashara zao kupata elimu ya kile wanachotaka kukifanya , lakini pia kampuni na wafanyabiashara wakubwa kujua namna ya kuboresha na kuendeleza biashara zao.

“Taifa limeendelea kwenye teknolojia .Wajasiriamali wajitahidi kuwa kwenye mitandao. Hata sisi tupo kwenye platform zote za mitandao ya kijamii na pia tuna website ambayo watu wanaweza wakawasiliana.” Anahimiza.

Anasisitiza kuwa Area Code iko tayari kuwapa maelekezo mbalimbali kuhusiana na biashara zao, na kutaka watu waache kulalamikia tatizo la kukosa ama kuwa na mitaji midogo.

Anawahimiza kuanza kufanyakazi na kile walichonacho na baadaye watafanikiwa kwenye biashara kwani , kila kitu kinaanza na msingi.

Nahuja, anasema Watanzania wanapaswa kufahamu njia kubwa ya kuendana na kasi ya maisha ni kufanya kazi kwa bidii, kuwa na utamaduni wa kuweka akiba huku pia wakiwekeza kwenye biashara.



# Wapewa miezi 2 kukamilisha ujenzi hospitali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, ametoa miezi miwili kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya hiyo inayojengwa katika Kata ya Inyala.

Dk. Mwanjelwa alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo ambao ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa kwa kutumia mfumo wa account ya dharura (Force account).

Alitoa muda huo baada ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, kudai kuwa ujenzi huo utakamilika baada ya wiki mbili huku Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme nchini (Tanesco), kuahidi kupeleka umeme baada ya mwezi mmoja na nusu.

Alisema muda huo unatosha kukamilisha shughuli zilizobaki na kwenye ujenzi imebakia kuweka malumalu na Tanesco wanatakiwa kutumia nguzo 12 kufikisha umeme.

"Mpaka kufikia mwezi Septemba huduma zinatakiwa ziwe zinatolewa hapa na wananchi waachane na kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu mjini na mimi ni mfuatiliaji lazima nitakuja kuangalia," alisema Dk. Mwanjelwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Katemba alisema maelekezo ya serikali ilikuwa ujenzi huo ukamilike kabla ya Juni 30, mwaka huu, lakini walikwama kwa sababu baadhi ya vifaa vilikuwa bado havijaingia.

Alisema vifaa vilivyokuwa havijanunuliwa ni malumalu na kwamba tayari zimeshanunuliwa na imebaki kuviweka ili kazi yote ikamilike ibaki nyumba za watumishi.

"Kwa sasa nakuhakikishia kuwa baada ya wiki mbili kazi zote za ujenzi zitakuwa zimekamilika na hospitali itakuwa tayari kwa kufunguliwa na huduma kuanza kutolewa," alisema Katemba.

Kwa upande wake Ofisa Uhusiano wa Tanesco Mkoa wa Mbeya, Christina Shoki, alisema ili kufikisha umeme katika hospitali hiyo inahitajika zaidi ya Sh. milioni 200.

# Zaidi ya walimu 400 wapatiwa mafunzo ya KKK

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ZAIDI ya walimu 420 kutoka halmashauri zote za Mkoa wa Songwe wameanza kupatiwa mafunzo ya kuwawezesha kufundisha kwa umahiri stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa darasa la awali.

Mafunzo hayo ambayo yalianza jana katika Chuo cha Ualimu Mpuguso, wilayani Rungwe, yatafanyika kwa awamu mbili kwa muda wa siku 10 mfululizo.

Ofisa Elimu Mkoa wa Songwe, Juma Kaponda, alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuipatia uzito elimu ya awali na kufuta aibu ya wanafunzi kuhitimu darasa la saba wakiwa hawajui kusoma, kuandika au kuhesabu.

"Serikali imeanza kuipatia uzito elimu ya darasa la awali ili kuhakikisha watoto wanafundishwa kwa umahili stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu ili wanapoingia darasa la kwanza wawe wanajua vizuri stadi hizo," alisema Kaponda.

Alisema kwa Mkoa wa Songwe, mafunzo hayo ni muhimu na kwamba kila shule ni lazima iwe na mwalimu mmoja aliyepata mafunzo hayo kwa ajili ya kufundisha darasa la awali.

"Mkoa wetu tunazo shule 420, tutaendesha mafunzo haya kwa awamu mbili, katika awamu ya kwanza tunao walimu 205 kutoka halmashauri tatu za Ileje, Tunduma na Momba, hawa watahudhuria mafunzo haya kwa siku tano na wakimaliza watakuja walimu kutoka halmashauri zilizobaki kwa ajili ya kuhitimisha," alisema Kaponda.

Alisema kuwa kutokana na umuhimu wake kama kuna shule imeanzishwa yenye darasa la kwanza na ina mwalimu mmoja, itabidi shule hiyo ifungwe kwa siku tano ili kutoa muda kwa mwalimu huyo kupata mafunzo hayo.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila alisema msingi wa maarifa kwa Watanzania upo mikononi mwa walimu ambao ndio wenye mchango mkubwa katika kuwawezesha Watanzania kupata uelewa wa kuliletea taifa lao maendeleo. "Maarifa kwa sasa ndiyo sarafu ya dunia, nchi zinashindana kwa teknolojia, nguvu za kijeshi, uchumi na hata michezo, lakini yote hayo msingi wake ni maarifa na wenye jukumu la kutoa maarifa kwa Watanzania ni walimu, hivyo walimu mnao mchango mkubwa wa kulifanya taifa letu lipate maendeleo," alisema Kafulila. Kafulila alisema elimu ya msingi kwa Watanzania ina umuhimu wa kipekee hivyo aliwataka walimu hao kuzingatia mafunzo hayo na kwenda kuiyafanyia kazi kwa vitendo ili dhamira ya serikali ya kuwapata vijana wenye maarifa ya kutosha katika kulijenga taifa lao iweze kutimia.

Baadhi ya walimu ambao wanapewa mafunzo hayo walisema kuwa changamoto kubwa walizonayo katika kufundisha watoto wanaoingia darasa la awali watoto hao kutojua Kiswahili na badala yake wanazungumza lugha za makabila yao.

Mwalimu Martin Stanford kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Ileje alisema kuwa ikiwa mwalimu ni mgeni katika mazingira fulani na hajui lugha za makabila ya eneo hilo inamuwia vigumu kuwafundisha watoto wa darasa la awali.

"Tunayo changamoto kwamba watoto wengi wanapokuja kujiunga na darasa la awali huwa hawajui kuongea Kiswahili na badala yake wanazungumza lugha za makabila yao, sasa ikiwa mwalimu unayepaswa kuwafundisha ni mgeni katika eneo hilo unapata shida sana kuwafundisha," alisema Mwalimu Martin.

Mafunzo hayo ambayo yanahusisha mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Songwe, katika vyuo vya ualimu tofauti vilivyopo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, yamefadhiliwa na Shirika la Watoto Duniani Unicef kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.



Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa (katikati), akitoa maelekezo kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, kuhusu ujenzi wa hospitali ya wilaya hiyo, alipofanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi huo, jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakwepa kifungo kwa kulipa mil. 10/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

RAIA watatu wa kigeni waliokuwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, wamekwepa kifungo baada ya kukubali kulipa faini ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

Watu hao ni Clive Rooney (62), raia wa Ileland, Ross Harris (34) na Robert Chalres (59), wote raia wa nchini Uingereza walikuwa wameshtakiwa kufuatia kutorosha madini aina ya dhahabu bila kuwa na kibali kinyume cha sheria ya madini namba 14 ya mwaka 2010.

Inadaiwa kuwa watu hao walikamatwa Julai 3, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (Sia), wakiwa na dhahabu yenye uzito wa gramu 1,043 na thamani ya Sh. milioni 98.5 wakiwa wanataka kusafiri kuelekea jijini Dar es Salaam.

Walifikishwa mahakamani Julai 8 na kushtakiwa kwa kosa la uhujumu uchumi na hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na uwezo wa kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na hivyo wakarejeshwa rumande na kutakiwa kuanza kusikilizwa tena Julai 22, mwaka huu.

Akitoa maelezo mahakamani hapo mbele ya Kaimu Hakimu Mfawidhi wa Mkoa wa Mbeya, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Jacqueline Nyantori, alieleza kuwa washtakiwa hao walimwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), wakiomba kupewa nafasi ya kukiri kosa.

Alisema kwenye barua hiyo washtakiwa walimwomba DPP kutoa kibali ili kesi yao ishuke kutoka Mahakama Kuu hadi Mahakama ya Hakimu Mkazi huku wakieleza kuwa wako tayari kulipa faini ama kupewa adhabu yoyote ikiwamo kurejesha madini.


Akitoa hukumu kwa washtakiwa hao, Kaimu Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Venance Mlingi, alisema kutokana na kosa hilo wanastahili kwenda jela miaka mitatu ama kulipa faini ya Sh. milioni 10 kila mmoja.

Hata hivyo, washtakiwa walikubali kulipa faini pamoja na kukubali madini yachukuliwe ndipo mahakama hiyo ikaamuru waachiwe huru na madini yapelekwe Benki Kuu mpaka serikali itakapoamua vinginevyo.

"Kwa kuwa mmelipa faini hii, sasa mnaachiwa huru na hamtakiwi kurudia kufanya kosa kama hili, madini haya yanachukuliwa na kupelekwa BoT," alisema Mlingi.

Wakili wa utetezi, James Kyando, aliiomba mahakama kuwapunguzia adhabu wateja wake kwa madai kuwa ni wageni na pengine wamefanya hivyo bila kujua kuwa ni makosa.

Hata hivyo, upande wa Jamhuri ukiongozwa Jaqueline Nyantori, ulipinga ombi hilo na kuiomba mahakama itoe adhabu kali ili iwe funzo kwa wengine kutokana na serikali kuwa kwenye vita kali ya kiuchumi na kwamba walikuwa wanakwepa kulipa kodi.





# Sumu kuvu yaua watatu Chemba

**Na Augusta Njoji,**
CHAMWINO

MGANGA Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. James Kiologwe, ametoa tahadhari ya uwepo wa ugonjwa wa sumu kuvu katika Wilaya ya Chemba ambao mpaka sasa umesababisha vifo vya watu watatu.

Akizungumza jana katika ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, katika kijiji cha Ilangali wilayani Chamwino, mganga mkuu huyo alisema ugonjwa huo umewakumba watu 17, kati yao watatu wamepoteza maisha.

"Mwaka huu kumenyesha mvua na kusababisha mahindi kuoza, hivyo wananchi muwe makini msitumie mahindi yaliyooza kwa kuwa ni hatari kwa afya," alisema.

"Ugonjwa huu unatokana na fangasi wanaoshambulia mazao, uko wilayani Chemba na mpaka sasa tulikuwa na wagonjwa 17 kati yao 3 wamefariki dunia," aliongeza.

Alitaja dalili za ugonjwa huo kuwa ni kuvimba tumbo, homa ya manjano, kutapika na baadaye kutoka damu maeneo mbalimbali ya mwili.

Kutokana na hali hiyo, Kiologwe aliwataka wananchi kutokula nafaka zilizooza wala kuwapa wanyama.

"Hakikisheni mnachambua nafaka zenu ili kuondoa zilizooza na muoshe na kukausha kabla ya kusaga nafaka zao," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa Dk. Mahenge alisisitiza elimu kuendelea kutolewa kwa wananchi juu ya ugonjwa huo.

"Ni vyema mkaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue namna ya kujikinga na dalili zake," alisema Dk. Mahenge.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Gilles Muroto, akionyesha vidhibiti walivyokamatwa navyo mawakala wanaosajili laini za simu, bila kufuata taratibu za sheria, jijini Dodoma jana. Jeshi hilo, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati, waliendesha msako huo na kufanikiwa kuwakamatwa mawakala 47. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mawakala 47 wa laini za simu wakamatwa

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Kati, limeendesha msako na kuwakamata mawakala 47 wanaosajili laini za simu bila kufuata taratibu za kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto alisema msako huo ulifanyika jana na kufanikiwa kukamata idadi hiyo ya mawakala.

Muroto alisema katika idadi hiyo waliokamatwa mawakala wanaume idadi yao ni 38, huku mawakala wanawake idadi yao ni tisa na hivyo kufanya idadi ya waliokamatwa kuwa watu 47.

Aliyataja maeneo ambayo walifanya msako kuwa ni mitaa ya Majengo Sokoni, Nyerere Square, Nanenane, St. John, Kikuyu, Sabasaba na Chuo cha Mipango. Aliongeza maeneo mengine waliyoendesha msako huo kuwa ni Stendi ya Bahi, Nkuhungu, Chang'ombe na kudai kuwa msako huo ni endelevu kila siku.

Myutoro alisema katika msako huo watuhumiwa walikamatwa na laini za simu 4,667 za mitandao mbalimbali za simu za mkononi na simu za mkononi 50 zilizokuwa zikitumika kusajilia wateja laini.

Alibainisha kuwa katika idadi hiyo ya laini zilizokamatwa, laini za Vodacom ni 1,300, Tigo 1,808, Airtel 716, Halotel 694 na TTCL 144. Kamanda Muroto alisema taratibu zinandelea kuhakikisha watuhumiwa wanafikishwa mahakamani kujibu mashtaka watakayopelekwa nayo.

Meneja wa TCRA Kanda ya Kati, Antonio Manyanda, alisema kabla ya msako huo walishakaa na wenye kampuni za simu za mkononi kuwakumbusha masharti ya kusajili laini.

Manyanda alisema katika msako huo walikuwa wakiangalia kwa msajili laini moja kama ana barua rasmi kutoka kwa kampuni iliyompa uwakala na kitambulisho cha mjasiriamali.

Alitaja matakwa ya kisheria wanayotakiwa kufuata watoa huduma za simu za mkononi kuwa atahifadhi na kutunza orodha ya mawakala wote wanaouza simu na laini.

Aliongeza matakwa mengine kuwa ni kuwa wakala kutouza au kusambaza kwa njia yoyote laini ya simu au simu yenyewe bila kwanza kuwa na kibali kutoa kwa mtoa huduma husika za mawasiliano.

"Yapo mengi lingine ni mwenye leseni ya kutoa huduma za mawasiliano atahakikisha wakala au msambazaji wa laini ana leseni ya biashara, namba ya utambulisho wa mlipakodi (TIN) na anuani ya kudumu ya ofisi," alisema.

Alisema waliokamatwa katika msako huo hakuna hata mmoja mwenye leseni wala barua kutoka kwa mtoa huduma za simu.

# Jafo aongeza muda wa ujenzi hospitali wilaya

**Na Augusta Njoji,** BAHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameongeza muda wa ujenzi wa hospitali za wilaya hadi Julai 30, mwaka huu, huku akizitaka halmashauri kuhakikisha majengo yanajengwa kwa ubora unaotakiwa.

Jafo alisema hayo jana wilayani hapa alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa hospitali hizo.

Akikagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bahi, Jafo alisema awali hospitali hizo ujenzi wake ulitakiwa kukamilika Juni 30, mwaka huu, lakini baadhi ya halmashauri bado hazijakamilisha.

Hata hivyo, alisema Bahi ni miongoni mwa halmashauri bora nchini katika ujenzi unaoendelea wa hospitali hizo.

"Nimefurahishwa kuona ujenzi wa hospitali ya Bahi ukiwa katika hatua za ukamilishaji na majengo yote yakiwa katika ubora wa hali ya juu. Ninyi ni miongoni mwa halmashauri bora katika ujenzi wa hospitali ya wilaya," alisema.

Waziri huyo alisema kazi kubwa imefanyika kutokana na usimamizi makini mbali na changamoto walizokutana nazo.

"Majengo yenu yote saba yako katika hatua ya ukamilishaji nimeshuhudia jitahada zenu za dhati, sababu nyie mlichelewa kuanza ujenzi na mmewahi kumaliza lakini kuna halmashauri zingine hawakuwa na changamoto yeyote na hawajafikia hatua ambayo mmefika Bahi," alisisitiza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alieleza walivyofanikiwa katika ujenzi huo kuwa waligawa majengo yote kwa wakuu wa idara kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji.

"Ujenzi wetu hatukumuachia mhandisi na mganga mkuu pekee katika kazi ya ujenzi wa hospitali, umoja wetu ndio mafanikio yetu hii ndiyo imetusaidia kufanikisha kazi hii kwa wakati. Tumeshirikiana katika kusimamia na kufuatilia na kila jengo hapa unaloliona lina mkuu wake wa idara," alisema.

Waziri Jafo anaendelea na ziara yake katika halmashauri zingine kukagua maendeleo ya ujenzi wa hospitali hizo.



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akiwasha umeme katika moja ya saloni za kiume katika kijiji cha Nyange, wilayani Kibondo, Mkoa wa Kigoma juzi, akiwa katika ziara ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini( REA). Kulia ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Lois Peter Bura. **PICHA: WN**

# Vietnam yataka ushirikiano sasa ujikite kibiashara, uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri Mkuu wa Vietnam, Trinh Dinh Dung, amesema uhusiano wa kidiplomasia uliopo kati ya mataifa ya Vietnam na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unapaswa uelekezwe katika masuala ya uchumi na biashara.

Alisema uhusiano huo ulikuwa umejikita zaidi katika masuala ya kisiasa hasa ikizingatiwa kwamba wakati huo kilikuwa kipindi cha mpito cha mataifa hayo kutoka katika mikono ya tawala za kikoloni.

Naibu Waziri huyo aliyasema hayo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Mjini Zanzibar akiwa nchini kwa ziara rasmi ya kiserikali ya siku nne.

Alisema sekta za uchumi na biashara kwa sasa kutokana na mabadiliko ya dunia ndio fursa pekee itakayoendelea kuunganisha pande hizo mbili kupitia maingiliano ya taasisi za umma na hata sekta binafsi ya watu wa mataifa hayo mawili rafiki.

Dung alisema ipo haja ya kuundwa kwa kamisheni ya pamoja kati ya Tanzania na Vietnam itakayotoa mwelekeo wa kufanikisha ustawi wa wananchi wa pande hizo mbili.

Alisema umadhubuti wa kamisheni hiyo itakayopaswa kuhusisha wataalamu, wafanyabiashara na watu maarufu unaweza kuibua miradi ya kiuchumi na kutoa fursa ya uwekezaji kwa kampuni na wafanyabiashara wa Vietnam na Tanzania.

Aidha, alishauri kwamba masuala hayo ni vyema yakaenda sambamba na mabadiliko ya viwanda yaliyopo ulimwenguni hivi sasa ambayo yatachangia kutoa ajira nyingi hasa kwa makundi ya vijana na wanawake.

Alieleza nchi yake iko tayari kubadilishana uzoefu na utaalamu katika hatua ya kuelekea kwenye maendeleo.

Alisema yapo maeneo ya kushirikiana katika kuimarisha uchumi akiyataja baadhi ni sekta ya utalii ambayo Zanzibar imeshajiimarisha kuwa kituo maarufu cha kuunganisha safari za watalii ulimwenguni.

Naye Balozi Seif alisema Zanzibar na Vietnam zinafanana katika harakati zao zilivyokuwa wakati wa kudai uhuru.

Balozi Seif alisema ziara za viongozi wakuu, waandamizi na wataalamu wakiwamo pia wafanyabiashara za kutembeleana zinaweza kuongeza ukaribu zaidi wa ushirikiano wa pande hizo mbili rafiki.

Alisema Zanzibar na Tanzania kwa jumla zimeweka milango wazi kwa wawekezaji wa nje kuanzisha miradi ya kiuchumi, hivyo aliwaomba wawekezaji wa Vietnam kupitia kiongozi wao huyo kuitumia fursa hiyo.

Balozi Seif alieleza kwamba inapendeza kuona kwamba timu ya wataalamu kutoka Vietnam iliwahi kufika Zanzibar miaka ya nyuma kusaidiana na wataalamu wazalendo kufanya utafiti katika sekta za Baharini na Kilimo, utafiti ambao unaweza kuleta tija hapo baadaye.

Aidha aliipongeza Vietnam kwa jitihada inazochukuwa za kuendelea kuiunga Mkono Zanzibar kitaalamu katika sekta tofauti za maendeleo.

Vietnam na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeanza ushirikiano wa kidiplomasia mnamo mwaka 1965, ambapo mataifa yote mawili yameshasaini mkataba wa ushirikiano katika sekta ya uchumi, biashara, sayansi na teknolojia.

# SMZ yawatunuku nishani madaktari wa China

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Zanzibar, Hamad Rashidi Muhamed, amewatunuku nishani madaktari wa Kichina walio maliza muda wao wa kutumikia kutoa huduma ya afya Zanzibar. Akitoa nishani hizo, Waziri Hamad alisema ni kutokana na kuitumikia Wizara ya Afya kwa juhudi zao za kitaalamu katika kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kuwapa matibabu bora.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeridhika na huduma zao, hivyo hainabudi kuonyesha utu kwa kuwapa nishani hizo za upendo na utendaji bora kwa kazi walizokuwa wakizifanyia kila siku.

Aidha, waziri huyo alisema Serikali za China na Zanzibar ni marafiki wakweli wanaojali hali za wananchi wa Zanzibar, ndio maana kila mwaka wanakuja kutoa huduma za afya Zanzibar tangu mwaka 1964 baada ya kuasisiwa Zanzibar. Naye mkuu wa timu hiyo kwa niaba ya umoja wa madaktari hao wanaoondoka Zanzibar kwenda kwao China, Dk. Zhang Zhen, alisema kuwa wameridhika na juhudi za Serikali ya Zanzibar na ukarimu na kuwajali na kukaa nao kama ndugu hali ambayo inaonyesha wazi kuwa China na Zanzibar ni marafiki wanao thaminiana na kujaliana utu kwa hali na mali.

Hata hivyo, alisema kuwa wanaondoka, lakini tayari ipo timu mpya ya madaktari, anaamini kuwa watafanyakazi kwa ushirikiano kama walivyo kuwa wakifanyakazi wao. Aliomba ushirikiano kwa timu mpya ambayo ipo sasa ili iweze kufanyakazi kwa ufanisi zaidi.

## Tahadhari dhidi ya magendo ya karafuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KIONGOZI wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Mzee Mkongea Ali, amevitaka vikosi vya ulinzi kuongeza doria na kupambana na magendo ya karafuu ambayo imekuwa ikidhoofisha nguvu za uchumi wa Zanzibar.

Mkongea alisema hayo wakati akizungumza na wananchi kisiwani Pemba baada ya kuwasili kwa Mwenge huo kutoka Tanga.

Alisema karafuu ni zao kuu la uchumi ambalo linatakiwa kulindwa ili kupambana na vitendo vya kusafirisha nje ya nchi kwa njia ya magendo.

"Navipongeza vikosi vya ulinzi vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Zanzibar kwa kupambana na magendo ya karafuu, hivyo kulifanya zao la karafuu kuwa na tija kwa taifa," alisema.

Aidha, aliwataka wananchi kuongeza juhudi za kuotesha miche mipya ya mikarafuu katika vitalu ili kuongeza uzalishaji wake.

Aliwataka mabwana shamba na mabibi shamba kutoa elimu zaidi juu ya kuotesha miche mipya ya mikarafuu katika vitalu binafsi.

"Moja kati ya njia nzuri ya kuimarisha zao la karafuu ni kuotesha miche mingi zaidi katika vitalu vipya ili kuchukuwa nafasi ya mikarafuu mikongwe ambayo imezeeka na kupungua uzalishaji wake," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake, Rashid Hadid, alisema wananchi wa Pemba wamejipanga vizuri na kuhamasika kwa ajili ya kuleta maendeleo na kupambana na umaskini.

Alisema wananchi wameitikia wito wa kushiriki katika miradi ya maendeleo ya majisafi na salama pamoja na ujenzi wa shule za msingi na sekondari.

"Tunatarajia kuzinduwa miradi mingi zaidi katika ujenzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na miradi ya usambazaji majisafi na salama vijijini," alisema.

Mwenge wa Uhuru uliwasili mkoani Pemba na unatarajiwa kutembezwa kwa siku nne katika mikoa miwili ya Pemba na kuzinduliwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

# Takukuru yachunguza ubadhirifu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Shinyanga, inafanya uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha za ujenzi wa miradi ya maendeleo, ambayo inatekelezwa na nguvu za wananchi na kusimamiwa na wataalamu wa halmashauri, baada ya kuonekana kuwapo na dosari kwenye manunuzi ya vifaa.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa Takukuru mkoani Shinyanga, Hussein Mussa, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa taasisi hiyo kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu, kuwa wamebaini kuwapo dosari za manunuzi kwenye ujenzi wa miradi ya maendeleo.

Alisema kumekuwapo na dosari mbalimbali kwenye manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa miradi ya maendeleo, ambapo wataalamu wa halmashauri wamekuwa wakishirikiana na kamati za ujenzi kufanya manunuzi ya vifaa hivyo kwa bei ya juu, kuliko bei ambayo ipo sokoni kwa lengo la kujipatia fedha za pembeni.

"Takukuru mkoa wa Shinyanga tunafuatilia ubadhirifu wa fedha kwenye manunuzi ya vifaa vya ujenzi kwenye miradi ya maendeleo, ambayo inasimamiwa na wananchi kwa kushirikiana na wataalamu wa halmashauri, ambapo wanapanga bei kubwa ya manunuzi tofauti na uhalisia ili wapate fedha na kuitia hasara serikali," alisema Mussa.

"Miradi ambayo tunaichunguza ni ujenzi wa kituo cha afya Kambaraga Shinyanga Mjini, jengo la Tanesco wilayani Kishapu, ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Ndule na Nyankende za wilayani Kahama, pamoja na Sekondari ya Chibe ya Shinyanga Mjini, miradi yote inathamani ya shilingi 644,864,180," aliongeza.

Aidha, alisema uchunguzi utakapokamilika na kupata ushahidi wa kutosha, watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka yanayowakabili, na kuwa fundisho kwa watumishi wengine wa umma kujihusisha na masuala ya ubadhirifu wa fedha kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

# Watu 600 kufanyiwa upasuaji wa mabusha

**Na Sabato Kasika**

JUMLA ya watu 600 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa mabusha, kwenye kambi ya upasuaji huo unaoendelea katika wilaya za Kilwa, Nachingwea na Ruangwa mkoani Lindi.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, na kufafanua kuwa katika wilaya yake uzinduzi huo ulifanyika juzi, huku yeye akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi.

Kabla ya kutua Nachingwea, mkuu huyo wa wilaya alisema kambi ilianzia Kilwa na kufanyika upasuaji wa watu 250 na sasa wilayani kwake wanatarajiwa kufanyiwa upusuaji watu 150.

Alifafanua kuwa wakati wa uzinduzi wa kambi hiyo juzi wilayani mwake, watu 130 walipasuliwa mabusha na kwamba jana wengine 20 walitarajiwa kufanyiwa upasuaji huo ili kufikisha idadi ya watu 150.

"Nachingwea watapasuliwa 150 na kisha kambi itahamia Ruangwa ambako watu 200 wanatarajiwa kufanyiwa upasuaji huo wa mabusha na hatimaye jumla yao kufikia 600 kwa wilaya hizo tatu," alisema Muwango.

Alisema, baada ya kumaliza Nachingwea, kambi inatarajia kuhamia Ruangwa leo ili watu 200 waliondaliwa wilayani humo waweze kufanyiwa upasuaji wa mabusha waondokane na ugonjwa huo alioutaja kuwa unaondoa utu wa mtu.

"Tatizo hili ni kubwa, tuhamasishe wana Lindi waitumie fursa hii kwani tiba sahihi inapatikana hospitali tu, na chanzo cha ugonjwa huu ni kuumwa mbu aina ya Ades na pia tuzingatie kanuni za usafi," alisema Muwango.

Alisema ni muhimu watu kufanya usafi wa mazingira na kuteketeza mazalia ya mbu na pia kujitokeza kupata kinga ya mabusha kila wanapotakiwa kufanya hivyo badala ya kujificha. "Kwa niaba ya wananchi wa Lindi ninasema asante Rais wetu Dk. John Magufuli kwa kuwasaidia wanyonge matibabu haya yanayotolewa bure na Wizara ya Afya kupitia mpango wa kutokomeza magonjwa yanayokuwa hayapewi kipaumbele," alisema.




Gari maalum lenye maabara ya kupima afya ya udongo lililozinduliwa jijini Arusha, kwa ajili ya kupima afya ya udongo katika mashamba ya wakulima nchini kwa gharama ya Sh. 25,000 mpaka 30,000. **MPIGAPICHA WETU**

# Maabara ya kisasa kupima afya yazinduliwa

**Na Mwandsihi Wetu,** ARUSHA

TEKNOLOJIA ya maabara ya kupima afya ya udongo kwa kutumia gari maalumu lenye uwezo wa kupima zaidi ya sampuli 100 za udongo kwa siku moja limezinduliwa nchini, ili kupima udongo na kumhakikishia mkulima uzalishaji wa mazao kwa wingi na yenye tija sokoni.

Uzinduzi wa teknolojia hiyo kutoka Uholanzi ulifanyika jijini Arusha kati ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega kwa niaba ya Tanzania na Makamu Waziri wa Kilimo na Ubora wa Chakula wa Uholanzi, Marjolijn Sonnema kwa niaba ya nchi yake ili kufanikisha mageuzi katika sekta ya kilimo.

Akizungumza baada ya kufanya uzinduzi wa teknolojia hiyo, Ulega aliishukuru Uholanzi kwa kutoa teknolojia yake kwa Tanzania na kusema itasaidia kuleta mapinduzi katika uzalishaji mazao.

"Kupima afya ya udongo inatoa majibu juu ya ubora wa ardhi husika, mazao yanayofaa kulimwa katika eneo hilo, kiwango cha mbolea kinachotakiwa na kutoa makadirio ya kiwango cha mavuno katika eneo husika," alisema Ulega.

Aliongezea kuwa gharama ya kupima shamba iliyowekwa ya shilingi 25,000 mpaka 30,000 wakulima wanaweza kumudu na kuwataka kuandaa mapema mashamba yao kabla ya kufanya kilimo ili kujua matatizo yaliyopo kwenye ardhi yake na nini afanye ili tija ya uzalishaji iongezeke.

"Teknolojia hii imeletwa kwetu, hivyo tunakila sababu ya kuhamasisha wakulima nchini kupima mashamba yao ili wajipatie uhakika wa zao linalofaa katika ardhi yake na nini afanye katika kuboresha ili aweze kuongeza tija ya uzalishaji," alisema. Aliesema kuwa mageuzi katika sekta ya kilimo yatapatikana kupitia teknolojia hii ya kupima afya ya udongo na kusababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo hali itakayochochea ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kuongezea thamani ya mazao.

"Ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi kunachochea kasi ya maendeleo kwa kuibua teknolojia na ujuzi mbalimbali katika kuiletea nchi maendeleo, naipongeza Kampuni ya Life Support System Tanzania (LSSL) kwa kuwekeza kwenye teknolojia hii," alisema Ulega.

Mkurugenzi Mkuu wa LSSL, Dk. Edmond Matafu, alisema magari manne yapo tayari pamoja na handheld soil scanner 100 ambazo zitatumiwa na maofisa ugani kwa ajili ya kuchukua sampuli za udongo katika maeneo ya vijiji kote nchini.

"Hii itasaidia kufanya upimaji wa afya ya udongo kwa wakati pasipo kuchelewa kipindi cha kulima ambapo itampa unafuu mkulima kujua mahitaji katika shamba lake ili aweze kupata tija katika uzalishaji mazao," alisema Dk. Matafu.

Aliongezea kuwa juhudi za serikali za kujenga uchumi wa kati na viwanda zitatekelezeka kwa ushirikiano kati ya sekta binafsi na

Serikali kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha vikwazo vyote vinavyokwamisha maendeleo vinatatuliwa ili maendeleo tunayoyatarajia yaweze kufikiwa kwa vitendo.

"Zoezi la kupima afya ya udongo litafanyika kote nchini kwani tumejipanga vizuri katika kutoa huduma hii kwa wakulima, hivyo ushirikiano ndio kitu muhimu katika kufanikisha zoezi hili ambalo litakwenda kuinua hali ya uzalishaji mazao nchini," alisema Dk. Matafu.

HABARI KIMATAIFA

# Bibi kizee akamatwa na bangi gramu 600

**NAIROBI, Kenya**

MWANAMKE mmoja, Lydia Mumbi Ndirangu mwenye miaka 83 amepandishwa kizimbani baada ya kukutwa na gramu 600 za bangi.

Taarifa iliyotolewa na redio ya Capita Fm ilieleza kuwa kibibi kizee huyo alisomewa mashtaka ya awali jana na Hakimu Mkazi, Nelly Kariuki.

Hata hivyo, Ndiragu ambaye ni mkazi wa Muthinga Jimbo la Tetu alikiri kukamatwa na kiasi hicho cha bangi ambayo thamani yake ni Sh. 500.

Mtuhumiwa ataendelea kushikiliwa na anatarajiwa kurudishwa mahakamani Julai 15 wakati atakaposomewa hukumu.

Kukamatwa kwa bibi huyo, kunafanya jumla ya matukio mawili yatokanayo na watu kukamatwa na bangi katika kipindi cha miezi miwili.

Mei mwaka huu, Mahakama ya Nyeri ilimhukumu mwanamke mmoja, kifungo cha miaka 30 kwa makosa ya kusafirisha bangi yenye thamani ya Sh. 2,820 bila faini.

Gazeti la Daily Nation la nchini Kenya limeeleza kuwa inaaminika bibi huyo amekuwa akinunua bangi mjini Nyeri na kuipeleka kwa mtoto wake wa kiume ambaye huwauzia wateja. *BBC*



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May (kushoto), akiwa na Rais wa Marekani, Donald Trump. **PICHA: REUTERS.**

## Uingereza yaishutumu Iran kwa kuzuia meli zake

**LONDON, Uingereza**

UINGEREZA imesema kuwa meli za kijeshi za Iran zilijaribu kuziba njia ili meli ya mafuta inayomilikiwa na Uingereza isiweze kupita.

Hata hivyo, meli hizo zilisambaratishwa na meli za kivita za Uingereza, madai ambayo Iran imekanusha vikali.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Uingereza ilieleza kuwa mkasa huo ulitokea juzi kwenye mlango wa bahari wa Hormuz, muda mchache baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump wa Marekani kurejelea vitisho vyake vya kuongeza vikwazo vikali dhidi ya taifa la Iran.

Awali, kituo cha televisheni cha Marekani, CNN, kiliripoti kuwa boti za Iran zilijaribu kuiteka meli hiyo ya mafuta ya Uingereza, lakini zikasambaratishwa na meli ya kijeshi ya Uingereza.

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi ya Uingereza ilisema kuwa mashua tatu za Iran zilijaribu kuizuilia njia meli hiyo iitwayo British Heritage inayomilikiwa na Kampuni ya Mafuta ya Uingereza (BP).

"Kinyume na sheria za kimataifa, mashua tatu za Iran zilijaribu kuziba njia meli ya kibiashara, British Heritage, kwenye mlango Bahari wa Hormuz. Meli ya kijeshi ya HMS Montrose ililazimika kujiweka tayari kwa mapambano na mashua hizo."

Hata hivyo, Kikosi cha Walinzi wa Mapinduzi ya Iran - chombo chenye nguvu kubwa za kijeshi ambacho Marekani inakilaumu kwa kufanya mashambulizi kadhaa dhidi ya meli za mafuta tangu mwezi Mei, kilikanusha vikali tuhuma za kujaribu kuiteka au kuziwekea vizuizi meli hiyo ya mafuta ya Uingereza.

"Hakujatokea makabiliano yoyote ndani ya saa 24 yaliyopita kati yetu na meli yoyote ya kigeni, zikiwamo za Uingereza." Ilisema taarifa fupi iliyotolewa na kikosi hicho.

Mkasa huo unachochea zaidi uhasama unaoendelea kwenye eneo hilo la Ghuba, ambalo tayari liko kwenye hatihati kutokana na mkwamo baina ya utawala wa Rais Trump na Iran juu ya mpango wa nyuklia wa taifa hilo la Kiislamu.

Jana, Rais Hassan Rouhani aliionya Uingereza kwamba itakumbwa na matokeo mabaya kufuatia hatua ya nchi hiyo kuikamata meli ya mafuta ya Iran kwenye eneo la Gibraltar.

Maofisa kwenye eneo hilo, ambalo linamilikiwa na Uingereza licha ya kuwa kwake Hispania, walidai kuwa meli hiyo ilikuwa ikielekea Syria, ambayo imewekewa vikwazo na Umoja wa Ulaya (EU), huku Marekani nayo ikiwa na vikwazo vyake dhidi ya mafuta ya Iran.

Iran ilikilaani kitendo hicho inachosema ni haramu, huku Uingereza ikikanusha madai ya maofisa ya Gibraltar kuwa imeishikilia meli hiyo kwa maagizo ya Marekani. *DW*

## Watu 30 wahukumiwa kifo kwa usaliti

**SANA'A, Yemen**

WANAFUNZI, wanaharakati na wahubiri takribani 30 wamehukumiwa kifo na Mahakama ya Jinai ya Sanna, nchini Yemen, kwa kusaliti nchi yao kwa faida ya nchi za kigeni zinazoendesha mashambulizi.

Watu hao walihukumiwa kifo Julai 9, mwaka huu na Mahakama ya Jinai ya Sanaa.

Watuhumiwa hao walikutwa na hatia ya kutoa taarifa kwa nchi za muungano unaoongozwa na Saudi Arabia kuhusu maeneo mbalimbali kwa lengo la kutekeleza mashambulizi ya anga. Watu wengine sita waliachiliwa huru.

Mashirika ya haki za binadamu yamelaani hukumu hiyo na kusema inakwenda kinyume na kanuni za sheria ya jinai nchini humo.

Kwa mujibu wa Radhya Al Mutawakel wa Mouwatana wa Shirika la Haki za Binadamu nchini Yemen, alisema hukumu hiyo ni ya ulipizaji kisasi.

Aidha, amelaani hukumu isiyo kuwa ya haki na isio kuwa na msingi wa kisheria na kusema: "Wakati mfumo wetu wa mahakama haupo, mahakama hii ya jinai ya Sanaa inaanza kazi leo na kutoa hukumu zisizofaa, ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu."

**Watuhumiwa hao walikutwa na hatia ya kutoa taarifa kwa nchi za muungano unaoongozwa na Saudi Arabia kuhusu maeneo mbalimbali kwa lengo la kutekeleza mashambulizi ya anga. Watu wengine sita waliachiliwa huru.**

Katika ukurasa wake wa mtandao wa twitter kwa Kiarabu, Shirika la Kimataifa la Haki za Binadamu la Amnesty International nalo limelaani hukumu hiyo na kusema haikuwa ya haki.

Limesema hukumu hiyo imejaa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na kuomba kusitishwa mara moja kwa watuhumiwa. *RFI*

## Kimbunga chaua watalii sita, 30 wajeruhiwa

**ATHENS, Ugiriki**

WATALII sita kutoka nchi za kigeni, wakiwamo watoto wawili wametoweka, huku watu 30 wamejeruhiwa baada ya kimbunga kikubwa, kupiga eneo la Chalkidiki, kaskazini mwa Ugiriki usiku wa Jumatano kuamkia Alhamisi wiki hii.

Imeelezwa kuwa kimbunga hicho kilivuma kwa muda wa dakika tano tu na kusababisha madhara makubwa kwa wakazi wa mji huo.

"Tulijikuta tumeingiliwa na balaa kubwa, kimbunga kilivuma kwa dakika chache tu," alisema Haris Lazaridis, mmiliki wa mgahawa wa Nea Plagia.

Alisema watu wengi walipiga kelele na kukimbilia kujificha ndani. Alisema kuwa watu zaidi ya mia moja wanadaiwa kupotea wakati kimbunga hicho kikitokea.

Alieleza kuwa watu wengi waliangukiwa na paa za nyumba zilizotengenezwa kwa mbao.

Redio ya Taifa (ERT) ikiwanukuu polisi na kikosi cha ulinzi wa umma kwa kueleza kuwa wote waliofariki ni watalii.

Eneo lililoathirika zaidi na hali hiyo mbaya ya hewa ni kisiwa kinachopendwa zaidi na watalii cha Chalkidiki.

Katika mgahawa wa Nea Plagia, mtu mmoja mwenye umri wa miaka 54, kutoka Romania na mwanawe mwenye umri wa miaka nane walifariki kwa kuangukiwa na paa la mgahawa huo lililong'olewa na kimbunga hicho.

Migahawa na baa zilizo kando ya pwani zilikuwa zimejaa wakati huo ambapo ni mwanzo wa msimu wa majira ya joto na ghafla, hali hiyo ikatokea, huku watu wakiingiliwa na hofu.

Eneo hilo ni maarufu kwa utalii, ambapo hali ya dharura ilitangazwa, lilionekana likikumbwa na hali mbaya ya hewa. *RFI*

# Sababu WB kuiwekea vikwazo kampuni ujenzi miradi mitatu

Na Salome Kitomari

BENKI ya Dunia (WB) imeiwekea vikwazo vya miezi 24 kampuni ya Sai Consulting Engineering kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa utekelezaji wa miradi mitatu katika nchi za Tanzania, Msumbiji na Ghana.

Rushwa iliyotajwa ni kuhonga maofisa wa serikali za nchi hizo waliokuwa na wajibu wa wanaosimamia miradi, kwa kutoa fedha taslimu na zawadi ikiwamo kutengeneza nyaraka feki kwa ajili ya malipo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na WB jijini Washngton Marekani, na kusambazwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari duniani, kampuni hiyo ilikuwa inatekeleza mradi wa ujenzi wa vituo vya ukaguzi mipakani, barabara na madaraja nchini, Msumbiji na miradi ya sekta ya ujenzi nchini Ghana.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa moja ya mradi wa Afrika Mashariki uliokwisha mwaka 2015 uliolenga kuboresha sekta ya biashara na usafiri katika kuimarisha shughuli hizo katika eneo la forodha la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujenzi na usimamizi wa ofisi za forodha katika mpaka wa Tanzania.

"Sai ambayo ilikuwa na mkataba wa kujenga na kusimamia ofisi za forodha kwenye baadhi ya mipaka ya Tanzania, walitoa zawadi, fedha taslimu kwa viongozi wa mradi, kuzidisha malipo ya ankara mbalimbali ambavyo vilitafsiriwa kuwa ni rushwa," ilisema.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza kuwa iwapo kampuni hiyo itawajibika kwa makosa hayo, adhabu yake itabatilishwa na ikishindwa haitaruhusiwa kushiriki kwenye miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Kwa upande wa miradi ya nchini Msumbiji, Kampuni hiyo ilikuwa na wajibu wa kujenga barabara na matengenezo ya madaraja mradi uliokwisha mwaka 2007 ukiwa na lengo la kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja nchini humo.

Alisema licha ya kampuni hiyo kuwa na mkataba wa usanifu wa barabara, lakini walitoa fedha taslimu na zawadi kwa viongozi wa miradi na kuwa na stakabadhi feki za malipo.

Kwa upande wa Ghana, mradi ulikuwa wa kuboresha sekta ya usafiri ulikwisha mwaka 2018 na lengo lilikuwa ni kuboresha usafiri wa bidhaa, abiria na kuboresha usalama barabarani.

"Kampuni ya Sai licha ya kuwa na mkataba wa kusimamia ujenzi wa barabara walitoa fedha taslimu na zawadi kwa viongozi wa miradi na kutengeneza nyaraka feki kwa ajili ya malipo vitendo ambavyo ni rushwa," taarifa ilieleza.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Ilala, Ubaya Chuma, akizungumza na wanachama wa chama hicho, tawi la Kisukuru, jijini Dar es Salaam jana, katika mkutano ulioandaliwa na viongozi wa serikali ya mtaa huo, ikiwa ni kuwashukuru viongozi wa halmashauri ya mtaa. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# Balozi Iddi aagiza ujenzi kliniki ya biashara D'Salaam

Na Elizabeth Zaya

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, ameiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kutafuta eneo maalum katika Jiji la Dar es Salaam la kujenga kliniki ya kudumu ya biashara ambayo ndiyo itakuwa inazungumzia changamoto mbalimbali za biashara nchini.

Balozi Idd alisema siyo binadamu pekee anayehitaji kuwa na kliniki bali na sekta ya biashara nayo inahitaji kliniki yake maalum ya kusaidia kuondoa magonjwa yote katika biashara hizo

"Siyo binadamu pekee ambaye anahitaji kliniki, bali hata biashara nazo zinahitaji kuwa na kliniki yake, na hii ndiyo itasaidia watu kujumuika na kuzungumza na itasaidia kumaliza magonjwa yote yanayokuwa katika sekta hiyo na naamini itakuwa na manufaa makubwa, " alisema Balozi Idd.

Pia aliiagiza Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade) Zanzibar na Bara kushirikiana kutafuta wabia ili wawekeze katika ujenzi wa maonyesho ya kisasa katika uwanja uliokwishatengwa Fumba Visiwani Zanzibar

Aliitaka pia Tantrade kuendelea kuboresha thamani ya mazao ili yapate soko ndani na nje ya nchi na kuipongeza kwa kufanikisha kufana zaidi kwa maonyesho hayo

Kwa upande wake, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema serikali itaendelea kuondoa vikwazo na kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara wa ndani

Bashungwa alisema Tanzania imepata faraja kuwa kutokana na idadi kubwa ya ushiriki kutoka nje ya nchi na kwamba lengo la serikali ni kuendelea kuboresha zaidi maonyesho hayo

Pia Bashungwa alitoa wito kwa wafanyabiashara nchini kutumia fursa ya maonyesho ya viwanda yatakayojumuisha nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) yanayotarajia kufanyika Agosti 5 hadi 9 mwaka huu kuonyesha biashara zao na kupanua wigo wao

Balozi Idd alitoa zawadi kwa mabanda bora katika maonyesho hayo ya 43.

# THRDC yatoa tamko utekaji wa watu

Na Beatrice Shayo

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umesema viongozi wa siasa na bunge wanatakiwa kujadili suala la utekaji na kupotea kwa Watanzania na kuja na maazimio badala ya kukaa kimya.

Tamko hilo lilitolewa jana na Mratibu wa Kitaifa wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema utekaji unaoendelea nchini bila kuchukuliwa hatua unaleta taswira mbaya katika nchi.

Olengurumwa alisema mpaka sasa jumla ya matukio 86 ya utekaji yameripotiwa kati ya hayo 23 ni watoto na watu wazima ni 63.

"Kati ya hao 86 ambao wametekwa wengine wamerudi, wengine wamekutwa wamekufa na wengine hawajulikani hadi sasa walipo," alisema.

Alisema wamesikitishwa na ongezeko la watu kutoweka na kwenda pasipojulikana na hakuna chochote kinachofanyika au kuonekana kufanywa kuzuia suala hilo linalozidi kuota mizizi katika jamii.

Alisema makundi ya wanasiasa, waandishi, watetezi na wasanii wameripotiwa kupotea na kutekwa na kati yao wapo ambao wameokotwa wakiwa wameumizwa vibaya na wengine wakiwa na hofu kubwa.

"Jukumu la polisi ni kulinda raia na mali zao linaambatana na kufanya uchunguzi dhidi ya matukio mbalimbali ya ukiukwaji wa haki za rai na kuchukua hatua dhidi ya wahusika," alisema Olengurumwa.

Alisema yanapotokea matukio makubwa ya uvunjifu wa haki za binadamu hatua hazichukuliwi, jeshi linawapa wasiwasi juu ya weledi na utashi wao katika kutekeleza majukumu yao.

Vile vile, alisema viongozi wengine hasa mawaziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, wamekuwa wakitoa kauli za kutia moyo mara tu baada ya kuripotiwa tukio la utekaji ama kupotea mtu.

Alisema muendelezo wa kauli na utekaji wa kauli hizo kwa vitendo imekuwa ni changamoto mfano alipotekwa Ben Saanane, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mwigulu Nchemba, aliahidi kufanyika kwa uchunguzi wa kina kuwatambua watekaji, lakini mpaka sasa hakuna taarifa zozote za kiuchunguzi.

"Alipotekwa Azory Gwanda, ahadi nyingi zilitolewa na mawaziri wa Mambo ya Ndani kwa nyakati tofauti, lakini cha kushangaza mahojiano ya mwisho yaliyofanywa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Kangi Lugola, alisema Azory Gwanda alitoweka na kwenda anapopajua na sio kwamba ametekwa na hivyo jeshi la polisi halishughuliki na uchunguzi wa kutoweka kwake tena," alisema.

Pia, alisema kutokana na matukio ya utekaji yanayoendelea nchini wamekuja na tamko lao lenye mambo saba ambayo ni muhimu kufanyiwa kazi.

Alisema vyombo vya ulinzi na usalama Tanzania lazima lihakikishe kuwa kila raia anaishi kwa uhuru na usalama nchini. Jeshi la Polisi liwe tayari kuwalinda raia na mali zao dhidi ya jambo lolote baya.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008


**PROJECTS GENERATE INCOMES AND CREATE EMPLOYMENT**

*Learn DESIGNING projects *Find DONORS *Establish NGO 0784505108 /0769505108

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

### KUPOTELEWA NA RESULT SLIP



**MERCY ASA KAYANGE** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.0291/0016** iliyotolewa na **GHOMME SEKONDARI** mwaka 2018.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control No. 0782908045.**

115319502

### OMBI LA URAIA



**BW/BIBI. RABIA SHEIKH MOHAMED**
**S.L.P 594 TANGA**

Tangazo limetolewa kwamba, mtu ambaye picha yake imetolewa hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya Ndani ya nchi. Mtajwa kwa sasa ni raia wa SOMALIAN na anatokea nchi ya SOMALIA pia anajishughulisha na Mke wa Nyumbani.

Mtajwa amekuwepo hapa nchini tangu 29/08/2006 pamoja na kuishi TANZANIA pia amewahi kuishi ZANZIBAR kwamba mtu yeyote mwenye taarifa au sababu kwanini mwombaji asipewe uraia apeleke sababu hizo kwa maandishi yaliyosainiwa kwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam.

**Kumb. DN TA/TP/4114**
**Kny.KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI**

115319702

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**RAJABU M.HASSAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 396 CQM** Aina yake **TOYOTA NOAH.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/122140/2019.**

215320202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MESHACK MOSES JOHN** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T. 856 ABJ** aina ya **L/CRUISER.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya Polisi. **KAH/TR/RB/559/2019.**

115320502

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA RUFAA NA. 55 OF 2018**

**THOMAS CHUBWA KAPERA……………MDAI**
**DHIDI YA**
**1. NKAYA CO. LTD**
**2. ACCESS BANK (T) LTD ……………WADAIWA**

**KWA: NKAYA CO. LTD**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe 30/07/2019 saa 3:00 asubuhi, kuja kusikiliza Madai yaliyofunguliwa na Mdaiwa dhidi yako.

Unatahadharishwa kuwa endapo hutafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo hii tarehe 03/07/2019.

115319302

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KOCHA

## BAFANA BAFANA ALIA NA KIPIGO

**CAIRO, Misri**

KOCHA wa Afrika Kusini (Bafana Bafana), Stuart Baxter, amebainisha kuwa ni kawaida kutokubali kushindwa, na kwamba kupoteza mechi dakika za majeruhi kunaumiza zaidi.

Bafana Bafana ilifungwa na Nigeria mabao 2-1 juzi na kuondolewa kwenye mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon).

"Ni wakati mgumu unapopoteza dakika za majeurhi, ni ngumu kuweza kuwa na mawazo chanya.

"Nina uhakika itachukua wiki moja kuweza kurudisha hali yangu ya kawaida, lakini wakati huu najisikia vibaya mno kwa upande wangu," alisema kocha huyo mara baada ya mchezo huo.

Baxter katika mchezo huo hakutaka kubadilisha kikosi chake, kwani alikichezesha kile kile kilichoiondoa Misri kwenye hatua ya mtoano wa timu 16 bora.

Mchezaji Thembinkosi Lorch ambaye alifunga bao la ushindi dhidi ya Misri aliendelea kuanza, licha ya Themba Zwane kumaliza adhabu yake ya kufungiwa mechi.



# TROOST-EKONG:

## NI NDOTO YA KWELI NIGERIA KUTINGA NUSU FAINALI

**CAIRO, Misri**

WILLIAM Troost-Ekong amesema kwamba goli lake la dakika za majeruhi lililoipa Nigeria ushindi wa 2-1 dhidi ya Afrika Kusini na kuipeleka hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka huu (Afcon) ilikuwa ni ndoto iliyotimia.

Beki huyo wa kati alifunga bao hilo dakika ya 89 na kuiwezesha Nigeria kusonga mbele ikiwa ni kwa mara ya 15 kati ya mara 18 iliyoshiriki michuano hiyo.

"Niliota wakati kama ule. Kufunga katika dakika ile na bao lako kuwa la muhimu zaidi ni jambo la kuvutia," alisema Troost-Ekong.

"Sio kazi yangu kufunga, mimi ni beki hivyo nilikuwa na furaha kubwa zaidi kwa kuweza kupata nafasi ya kufunga bao muhimu kama lile. Baada ya wao kufunga, nikajua hapa tupo kwenye wakati mgumu na nilitaka kulipiza kisasi na nikafanikiwa.

"Tulijiamini kwamba tunaweza kufunga tena. Hatukutaka kwenda muda wa ziada kwa sababu tungechoka, na nafikiri hata wao Afrika Kusini hawakutaka hili litokee."

Nigeria, ambao walishinda taji hilo kwa mara ya tatu mwaka 2013, sasa watacheza Jumapili nusu fainali kati ya Algeria au Ivory Coast ambao walicheza jana usiku.

"Nafikiri kwamba kila mchezo kwa sasa ni mgumu kwetu. Tumeona timu kubwa zikiondolewa kwenye mashindano, hivyo timu yoyote itakayoingia nusu fainali ni ngumu kucheza nayo, lakini tutajitahidi," aliongeza kusema Troost-Ekong.

"Tumekuja hapa kushinda taji na si vinginevyo."

# Senegal yatinga nusu fainali baada ya miaka 13

**CAIRO, Misri**

SENEGAL imefuzu hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 13.

Bao la Idrissa Gueye la dakika ya 70, liliwawezesha Senegal kuibuka na ushindi wa goli 1-0 dhidi ya Benin na kufuzu hatua hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2006. Gueye ambaye ni kiungo wa Klabu ya Everton ya nchini England alifunga bao hilo baada ya kutengenezewa pande zuri na Sadio Mane wa Liverpool.

Mechi hiyo ilikuwa ya kwanza kwenye michuano ya Afcon kutumia teknolojia ya maamuzi ya usaidizi wa video (VAR), na hakukutokea utata wowote kwenye mchezo huo.

Benin walilazimika kumaliza mchezo huo wakiwa wachezaji 10 baada ya mchezaji wake, Olivier Verdon kutolewa nje kwa kadi nyekundu ya moja kwa moja kwa faulo. Kocha wa Senegal, Aliou Cisse, alifanya mabadiliko ya mchezaji mmoja tu kutoka kwenye kikosi chake kilichoifunga Uganda, ambapo Keita Balde alianza akichukua nafasi ya mshambuliaji wenzake, Ismaila Sarr.



Huku kocha wa Benin, Michel Dussuyer alifanya mabadiliko matatu kutoka kwenye kikosi kilichoishangaza Morocco ambako walitinga hatua hiyo kwa mara ya kwanza katika historia yao.

Khaled Adenon aliukosa mchezo huo kutokana na kutumia adhabu ya kukosa mchezo mmoja na Seibou Mama na Jodel Dossou waliachwa benchi, huku Seidou Baraze, Sessi D'Almeida na Steve Mounie wakichukua nafasi zao.




# COSTA

## AJIANDAA KUJIUNGA EVERTON

**MADRID, Hispania**

DIEGO Costa yupo tayari kufanya mazungumzo na Everton ili kurudi kwenye Ligi Kuu England baada ya miaka miwili ya kuwa nje ya ligi hiyo, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Ujio wa Joao Felix na Alvaro Morata kusaini mkataba wa kudumu ina maana kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 anaweza kuondoka pale Atletico Madrid kipindi hiki cha majira ya joto.

Mshambuliaji huyo alikaribia kujiunga na Everton mwaka 2017 na sasa inadaiwa kuwa uhusiano yake usiyoridhisha na Atletico Madrid unaweza kumfanya aondoke hapo jijini Madrid.

Costa alifungiwa mechi nane msimu uliopita kwa kumtukana mwamuzi kwenye mchezo dhidi ya Barcelona.

Costa alikuwa na matukia ya ukorofi na mafanikio wakati alipocheza kwa kipindi cha miaka mitatu pale Chelsea.

Alishinda taji la Ligi Kuu chini ya makocha, Jose Mourinho na Antonio Conte, lakini muda wake wa kukaa pale Stamford Bridge ulimalizika baada ya kwenda Brazil na kuituhumu klabu hiyo kuwa inamchukua kama mharifu.

Na sasa Everton wanataka kumchukua kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji katika msimu ujao.

# BENITEZ AWAONYA ARTETA, VIEIRA

**NEWCASTLE, England**

RAFA Benitez amewaonya Mikel Arteta na Patrick Vieira kuhusu mpango wao wa kutakiwa na kuinoa klabu ya Newcastle United.

Na sasa beki wa zamani wa Sunderland, Steve Bruce ametajwa kwamba anapewa nafasi kubwa ya kwenda kukamata kibarua cha kuinoa timu hiyo.

Kocha msaidizi wa Manchester City, Arteta na kocha Nice, Vieira waliripotiwa kuwekwa kwenye orodha ya Newcastle United ya kwenda kurithi mikoba ya Benitez, ambaye hivi karibuni ametimkia China.

Lakini, ripoti zinadai kwamba Arteta ameamua kujitoa kwenye mchakato huo baada ya kuzungumza na Benitez, raia mwenzake wa Hispania, ambaye amekuwa akiwakosoa watendaji wa ngazi za juu katika kikosi hicho chenye maskani yake St James' Park.

Gwiji wa Arsenal, Vieira naye alimpigia simu kocha huyo wa zamani wa Liverpool kumuulizia mazingira ya kufanya kazi kwenye kikosi cha Newcastle na hivyo kuahirisha mpango wa kwenda kwenye timu hiyo.

Newcastle walikuwa na hesabu pia za kumchukua Roberto Martinez, lakini sasa wameamua kuachana na mpango huo kwa sababu kocha huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji anachokihitaji kwa sasa ni kubeba ubingwa wa Ulaya akiwa na chama lake hilo lenye mastaa kibao akiwamo Eden Hazard na Kevin De Bruyne.





# PSG KUMPIGA FAINI NEYMAR

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR ameandaliwa adhabu ya kupigwa fainli ya pauni 340,000 baada ya kushindwa kurudi kwa wakati katika mazoezi ya Klabu ya Paris Saint-Germain wiki hii, kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail.

Nyota huyo wa Brazil hakuwapo kwenye kikosi cha PSG katika siku yake ya kwanza ya mazoezi ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Ufaransa.

Neymar hatapewa bonasi ya pauni 340,000 ya Julai hii kama adhabu ya kuchelewa kuripoti kwenye mazoezi.

Mshambuliaji huyo ambaye ameripotiwa kutokuwa na tabia nzuri hapo PSG alikuwa nchini Brazil wikendi iliyopita akiangalia timu yake ya Brazil ikiwafunga Peru kwenye fainali ya Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 hakucheza michuano hiyo baada ya kuumia kifundo cha mguu na hivyo kulazimika kuondolewa kwenye kikosi cha timu hiyo.

Neymar, ambaye aliondoka nchini Hispania katika Klabu ya Barcelona kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 198, miaka miwili iliyopita, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Barcelona.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ORIGI KUENDELEA KUULA LIVERPOOL

●●●Ni baada ya kusaini mkataba mwingine mrefu wa kuitumikia klabu hiyo...

**LIVERPOOL, England**

STRAIKA Divock Origi amesaini mkataba mpya wa muda mrefu wa kuendelea kuitumikia klabu yake ya Liverpool.

Mchezaji huyo wa kimataifa kutoka Ubelgiji, ambaye ana umri wa miaka 24, alitua Liverpool mwaka 2014 akitokea Lille kwa mkataba wa miaka mitano, lakini akicheza misimu miwili tu kwa mkopo.

Lakini alirejea klabuni hapo msimu uliopita, akiwa ni mchezaji aliyesaidia kuipa mafanikio Liverpool kwa kufunga mabao mawili katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona kwenye mchezo wa hatua ya nusu fainali.

Origi ambaye baba yake ni mchezaji wa zamani wa Kenya alifunga tena katika mchezo wa fainali ya michuano hiyo katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Tottenham.

"Hisia zangu kila siku zilinieleza kuwa ninataka kubakia hapa," alisema Origi. "Kuna mambo maalumu yanaendelea klabuni hapa."

Klabu hiyo maarufu kwa jina la The Reds ililipa kiasi cha pauni milioni 10 kwa ajili ya kumsajili Origi baada ya kufanya vema katika Fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2014 na kumwacha kwa mkopo Lille katika msimu wa 2014-15.

Misimu miwili iliyofuata, Origi aliifungia Liverpool mabao 21 katika mashindano mbalimbali lakini alilazimika kupambana kurejea katika kiwango chake baada ya kuwa na maumivu ya kifundo cha mguu na kupelekea kupelekwa kwa mkopo katika klabu ya Wolfsburg ya Ujerumani katika msimu wa 2017-18.

Origi aliendelea kukaa nje mpaka aliporejea tena uwanjani Desemba mwaka jana na kucheza mechi yake ya kwanza katika msimu wa 2018-19, akitokea benchi na kufunga bao la dakika za majeruhi lililoipa Liverpool ushindi dhidi ya mchezo wa watani zao wa Merseyside, kabla ya kumaliza msimu kwa kumbukumbu njema.

"Ni historia ya ukweli ambayo inaweza kuandikwa katika mpira wa miguu," alisema Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp. "Hakuweza kufanya vema akiwa na Wolfsburg, na kulazimika kurejea, alikuwa akifikiria kuhusu kuondoka.

"Lakini alikuwa na kukua na kukua, katika mazoezi alionekana hivyo, na alifunga mabao muhimu na yasiyotarajiwa.

"Sasa ni mchezaji wa kutegemewa ambaye ni muhimu kuwa naye."

## KWA UFUPI

**MATA AWACHUNIA WACHINA**

KIUNGO wa Manchester United Mhispania Juan Mata (31), amekataa ofa ya mshahara wa pauni 550,000 kwa wiki kutoka kwa klabu ya Shanghai SIPG na kusema atasaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Old Trafford kwa sababu ni moja ya "timu kubwa tatu au nne" duniani. ***(MUTV)***

**MALCOM ANUKIA ARSENAL**

ARSENAL inataka kumsajili winga wa Barcelona, Malcom, wakati tayari Everton imewasilisha ofa ya pauni milioni 31.5 kwa ajili ya kumnunua Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sun)***

**SAUNDERS AMCHULIA SOLSKJAER**

STRAIKA wa zamani wa Liverpool, Dean Saunders anaamini Ole Gunnar Solskjaer "hataweza kumaliza msimu huu" akiwa kocha wa Manchester United. ***(talkSPORT)***

**UNITED KUIPIKU CITY**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnae Solskjaer, anaamini klabu yake itafanikiwa kuwazidi nguvu majirani zao, Manchester City kunasa saini ya beki wa Leicester City na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire (26) kwa dau la pauni milioni 75. ***(Mail)***

**COSTA, EVERTON WATETA**

STRAIKA wa zamani wa Chelsea, Diego Costa (30), amesema kuwa yuko tayari kufanya mazungumzo na Everton ili aweze kurejea katika Ligi Kuu England baada ya Mhispania huyo aliyezaliwa Brazil kuweka wazi kwamba anataka kuondoka Atletico Madrid. ***(Sun)***

**HIGUAIN AKARIBIA WEST**

WEST Ham imeanza mchakato wa kutaka kumsajili kwa mkopo straika wa Juventus, Gonzalo Higuain (31).Nyota huyo raia wa Argentina nusu ya msimu uliomalizika aliitumikia kwa mkopo Chelsea. ***(Sky Sports Italia, via Mail)***

**BRUCE ATAKIWA NEWCASTLE**

KOCHA wa Sheffield Wednesday, Steve Bruce, amesema kuwa tayari ameomba ruhusa kwa mabosi wa timu hiyo ili kufanya mazungumzo na Newcastle ambayo inahitaji kumwajiri katika kikosi chake. ***(Times - subscription required)***

**OLMO KUTUA SPURS**

KLABU ya Tottenham iko mbele ya Atletico Madrid katika vita ya kuwania saini ya kiungo Mhispania, Dani Olmo ambaye ana umri wa miaka 21 akitokea Dinamo Zagreb kwa dau la pauni milioni 27. ***(AS, via Star)***

**JUVE YAIKATALIA EVERTON**

JUVENTUS imekataa kupokea ofa ya euro milioni 30 kutoka Everton kwa ajili ya kumuuza straika wake chipukizi, Mtaliano Moise Kean, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Tuttosport, via Sport Witness)***

**ROMA YAMTAKA TOBY**

ROMA imeweka wazi kwamba inamhitaji beki wa kati wa Tottenham, Toby Alderweireld (30) ambaye dau lake limetajwa kuwa ni pauni milioni 25 huku mwisho wa kumsajili Mbelgiji huyo imetangazwa kuwa ni Julai 26 mwaka huu. ***(Sky Sports)***

**PEPE KUTUA EVERTON**

KLABU ya Everton imesema kuwa inataka kumsajili mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Nicolas Pepe (24) ambaye dau lake ni pauni milioni 58.5 ambalo linatarajiwa kuweka rekodi katika klabu hiyo. ***(Telegraph)***

**LEMINA AGOMBEWA ENGLAND**

KIUNGO wa Southampton, Mario Lemina, ambaye anawaniwa na Manchester United, Arsenal na Leicester, amesema kuwa hataki kuona anaichezea klabu hiyo maarufu Saints katika msimu ujao. ***(France Football, via Daily Echo)***

**CEBALLOS AKARIBIA SPURS**

TOTTENHAM iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mchakato wa kumsajili kwa mkopo kiungo wa Real Madrid, Dani Ceballos ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# NIYONZIMA AREJEA LIGI KUU RWANDA

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA kiungo wa mabinga wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Haruna Niyonzima, amesaini mkataba mpya wa kuitumikia klabu ya AS Kigali inayoshiriki Ligi Kuu nchini Rwanda, imefahamika.

Nahodha huyo wa zamani wa Rwanda (Amavubi), Niyonzima ametua AS Kigali akiwa ni mchezaji huru baada ya mkataba wake wa miaka miwili na Simba kumalizika hivi karibuni.

AS Kigali ilimaliza Ligi Kuu Rwanda msimu uliopita katika nafasi ya saba, lakini ilitwaa Kombe la Amani (Peace Cup) na hivyo kukata tiketi ya kuiwakilisha nchi hiyo kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

Taarifa kutoka Rwanda zinasema kuwa Niyonzima, mchezaji wa zamani wa APR na Yanga, amesaini mkataba wa miaka miwili baada ya kufikia makubaliano nao.

"Ni kweli ametua AS Kigali, ameshasaini na ametambulishwa," chanzo chetu kilisema jana.

Kiungo huyo mkongwe wa Afrika Mashariki na Kati ambaye alikuwa na kiwango kizuri msimu uliopita, aliichezea kwa mafanikio Yanga kwa muda wa miaka mitano na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara kwa misimu minne akiwa na mabingwa hao wa kihistoria.

Baada ya mkataba wake kumalizika, alijiunga na Simba ambayo aliitumikia kwa misimu miwili na yote amebeba taji la Ligi Kuu Bara huku pia akicheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Niyonzima amerejea kwao Rwanda ambako ana historia ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Rwanda mara tatu.

Uamuzi huo wa Niyonzima kuondoka Simba umetokana na kutokuwa katika mipango ya Mbelgiji Patrick Aussems, ambaye anaimarisha kikosi chake huku ikielezwa wanajiandaa kufanya vema zaidi katika mashindano ya kimataifa msimu huu.




Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Dismas Ten, akizungumzia masuala mbalimbali kuhusu usajili na maandalizi ya timu yao kuelekea msimu mpya kwenye makao makuu ya klabu hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wadau waitaka TFF ijirekebishe

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, kushangazwa na kile alichokiita 'kiburi' cha viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kukacha kikao alichokiitisha kujadili masuala ya mchezo huo, baadhi ya wadau wa soka wameshangazwa na kitendo hicho.

Mwakyembe juzi aliitisha kikao kujadili masuala mbalimbali ikiwamo uamuzi wa kuvunja mkataba na aliyekuwa Kocha wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, lakini viongozi hawakuhudhuria.

Tayari Mwakyembe amesema kuwa kikao kijacho na viongozi hao kitafanyika Julai 24 mwaka huu, na kitakuwa ni cha wazi kwa wadau mbalimbali kuhudhuria.

Akizungumza jijini jana, Wakili, Aloyce Komba, alisema kuwa kitendo walichokifanya TFF si kizuri na wameonyesha dharau kwa Serikali ambao ni wadau wakuu wa soka nchini.

"Binafsi nimeshangazwa sana, Serikali ni mdau mkubwa wa soka, na TFF uongozi wake wakati unaingia madarakani ulisema utashirikiana kwa karibu na wadau wao katika kuendeleza soka, sasa inashangaza kuona Waziri mwenye dhamana na michezo anaitisha kikao lakini viongozi wa juu wa TFF hawaudhurii," alisema Komba.

Aliongeza kuwa Rais wa TFF, Wallace Karia, anapaswa kuchukuliwa hatua za kiserikali kwa kuwa yeye pia ni mtumishi wa Serikali na ameigomea Serikali ambayo ni mwajiri wake.

Naye mchezaji wa zamani wa soka, Jemadari Saidi, alisema viongozi wa TFF walipaswa kuitikia wito wa Waziri Mwakyembe iili kufahamu kile walichoitiwa.

Said alisema kuwa waziri huyo ni mwakilishi wa Rais John Magufuli, hivyo kukaidi wito wake, ni kukaidi wito wa kiongozi mkuu wa nchi.

## Stars yapeperusha Tamasha la Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuanza kukiimarisha kikosi chake, timu ya Yanga inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Dodoma FC itakayochezwa Julai 25 mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, imeelezwa.

Uamuzi wa kucheza mechi hiyo na nyingine itakayofuata katika mkoa wa Morogoro, umetokana na kuahirisha tamasha la Siku ya Mwananchi ambalo lilitarajiwa kufanyika Julai 27 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jana jijini, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Dismas Ten, alisema kuwa wameahirisha tamasha lao kwa sababu ya kuheshimu ratiba ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kuhusu programu za Timu ya Taifa (Taifa Stars).

"Tumeahirisha sherehe yetu ya Siku ya Mwananchi kwa kuheshimu mashindano ya CHAN (Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani), siku hiyo Uwanja wa Taifa utakuwa unatumika," alisema Dismas.

Katibu huyo alisema watakuwa na michezo mitano ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu Bara pamoja na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kuhusu maendeleo ya kambi yao iliyopo Morogoro, kiongozi huyo alisema kuwa inaendelea vizuri huku akieleza kwamba wachezaji waliokuwa kwenye kikosi cha Stars wanatarajia kuwasili kambini huko keshokutwa.

## Malindi kutema wachezaji watano

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIKA kuhakikisha inarejesha makali yake, uongozi wa Malindi FC umesema kuwa unatarajia kusajili wachezaji wapya 10 ili kukiimarisha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar, imeelezwa.


Hata hivyo, timu hiyo inatarajia pia kuwaacha wachezaji wake watano ambao wamepata majeraha ya muda mrefu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa makipa wa timu hiyo, Salehe Machupa, alisema kuwa uamuzi wa kusajili wachezaji wapya unalenga kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa msimu ujao .

"Kuna wachezaji watano (majina tunayahifadhi) ambao hawakuisaidia timu kwa kipindi chote cha msimu uliopita, walikuwa majeruhi kwa msimu mzima, walishindwa kuingia uwanjani kucheza, hali iliyopelekea timu kufanya vibaya, tofauti na matarajio yetu," alisema Machupa.

Alisema kuwa wachezaji hao wakipona, wanaweza kurejea kwa sababu wana uwezo mzuri na wanauzoefu na ushindani uliopo katika ligi hiyo.

Michezo
Ijumaa Julai 12, 2019
Nipashe



## Origi kuendelea kuula Liverpool

HABARI UK 30



Nahodha wa Chelsea, Cesar Azpilicueta (kulia), akidhibitiwa na mchezaji wa Bohemian, Andre Wright, katika mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi usiku jijini Dublin, Ireland. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KWENDA SAUZI JUMAPILI

●●●Ikiwa huko inatarajia kucheza mechi za kirafiki dhidi ya vigogo wa...

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba ya jijini Dar es Salaam, wanatarajia kuondoka nchini keshokutwa Jumapili na kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kuweka kambi maalumu ya kujiandaa na msimu ujao, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema kuwa maandalizi ya safari hiyo yako katika hatua za mwisho na wachezaji wote waliosajiliwa watakuwapo kwenye ziara hiyo.

Manara alisema kuwa uongozi wa klabu hiyo uko katika mazungumzo na timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Afrika Kusini ili kupata mechi za kujipima, ambazo wanaamini zitawasaidia kuwaweka tayari wachezaji wao kukabiliana na ushindani kwenye mashindano yote watakayoshiriki.

Alisema kuwa wameamua kwenda Afrika Kusini, kwa sababu wanaamini wachezaji wao watapata muda kukamilisha programu zote za Kocha Mkuu Mbelgiji Patrick Aussems na hatimaye kurejea nchini wakiwa na "makali". "Tunamshukuru Mungu kwa hatua ambayo tumefikia, timu inatarajia kuondoka Dar es Salaam Jumapili usiku, kambi yetu itakuwa Afrika Kusini, itahusisha wachezaji wote na tukiwa huko, itakuwa ni nafasi nzuri ya mwalimu kukisuka kikosi chetu, tunahitaji kuendeleza mazuri pale tulipoishia msimu uliopita," alisema Manara.

Aliongeza kuwa wanajua kila timu imejiimarisha, ndio sababu wameamua kwenda "kujifua" ughaibuni ambapo mazoezi rasmi yataanza Jumatatu.

Alieleza kuwa wachezaji wao wa kimataifa wakiwamo mshambuliaji bora wa msimu uliopita Mnyarwanda Meddie Kagere wataanza kuwasili nchini leo ili kuungana na nyota wazawa kwa ajili ya kukamilisha maandalizi ya safari hiyo.

Wachezaji wengine wapya ambao wanatarajiwa kuelekea Afrika Kusini ni pamoja na Shiboub Sharaf El Eldin, Francis Kahata, Tairone Santos da Silva, Person Fraga Viera, Wilker Henrique da Silva, Deogratius Kanda, Ibrahim Ajibu, Beno Kakolanya, Gadiel Michael na Kennedy Juma.

Nahodha John Bocco, Pascal Wawa, Shomari Kapombe, Erasto Nyoni, Aishi Manula, Clatous Chama, Jonas Mkude, Rashid Juma, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Hassan Dilunga, Said Ndemla na Mzamiru Yassin pia watakuwapo katika safari hiyo.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara waatanza msimu kwa kuvaana na Azam FC katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayochezwa Agosti 17 mwaka huu na itafungua pazia jipya la ligi kwa kuikaribisha JKT Tanzania Agosti 27 kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

# Yanga hesabu matata CAF

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa Yanga umesema umebakiza nafasi nne katika usajili wa kimataifa kwa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa ajili ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Uamuzi huo utawafanya wapate nafasi ya kusajili wachezaji wengine wapya katika kipindi cha dirisha dogo endapo watabaini upungufu kwenye kikosi chao.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Dismas Ten, alisema kuwa klabu hiyo ilikamilisha mchakato wa usajili juzi na kutuma majina ya wachezaji wake itakaowatumia katika mashindano hayo ya CAF kama inavyotakiwa.

Dismas alisema kuwa tayari kikosi chao kinaendelea na mazoezi na wanakiamini kitafanya vema katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Nafasi hizi nne tutazijaza kwenye dirisha dogo, kwa sasa tunaamini majina tuliyoyatuma CAF yanatosha, na kama timu tunaendelea na maandalizi mengine, ni ngumu kuweka wazi majina ya askari wetu, lakini itoshe kusema wale wote tuliowasajili majina yao yapo na siku zijazo watu watajua," alisema Dismas.

Alisema malengo ya klabu yao ni kuhakikisha wanarejesha heshima kwa kushinda makombe mbalimbali na ndio maana wamefanya usajili wa kiwango cha juu kwa kuwanasa nyota wenye uwezo kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Katika kampeni ya kuwania ubingwa wa msimu uajo wa 2019/20, Yanga itacheza dhidi ya Ruvu Shooting ya Mlandizi, mkoani Pwani.

Yanga na KMC FC zimepata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa baada ya mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba kufanya vema katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hivyo Tanzania kupata nafasi ya kuwakilishwa na timu nne kwenye michuano ya CAF.

Timu nyingine zitakazoshiriki mashindano ya kimataifa kutoka Tanzania Bara ni Azam FC na KMC, ambazo zitashuana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >